**17 MEI, 2022**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

**Kikao cha Ishirini na Nne – Tarehe 17 Mei, 2022**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**MHE. YAHYA ALI KHAMIS K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**SPIKA:** Ahsante sana. Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 207

**Hitaji la Kituo cha Afya – Mangopacha Nne Mtwara**

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Afya katika Kata ya Mangopacha Nne ili kuwanusuru Akina Mama na tatizo la ukosefu wa huduma wakati wa kujifungua?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa David Silinde majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetoa fedha Shilingi bilioni 86 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya 234 kwenye kata za kimkakati kote nchini. Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara imepokea Shilingi milioni 250 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Kituo cha Afya Mkunwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga vituo vya kutolea huduma za afya kwenye kata za kimkakati zenye uhitaji mkubwa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa kituo cha afya kwenye Kata ya Mango Pacha Nne.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anastazia Wambura, swali la nyongeza.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza nishukuru sana majibu ya Mheshimiwa Waziri, na nimpongeze, huwa anatembelea sana Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, ninakiri hizo fedha milioni 250 kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Mkunwa, zimefika na zinaendelea kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, nimpe taarifa Mheshimiwa Waziri kwamba wananchi wa Mangopacha Nne, tayari walishaandaa eneo kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya muda mrefu tu, zaidi ya miaka mitano. Kwa hiyo, niombe sasa Serikali itoe kipaumbele fedha zitakapopatikana.

Mheshimiwa Spika, hii Kata ya Mangopacha Nne ni moja ya kata katika Tarafa ya Dihimba, ambapo tarafa hii haina hata kituo kimoja cha

afya lakini kuna zahanati katika baadhi ya vijiji. Kuna tatizo kubwa sana la wanawake…

**SPIKA:** Swali lako Mheshimiwa.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, nauliza swali, katika kutatua tatizo la wanawake kujifungua hasa nyakati za usiku. Je, Serikali itakuwa tayari kuboresha huduma katika hizi zahanati ili kusudi akina mama waweze kupata huduma bora?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ninatambua kwamba anafanya kazi nzuri kwa Mkoa wa Mtwara na ndiyo maana amekuwa akitetea sana katika huduma za afya, hususan wanawake katika mkoa wake. Nimhakikishie tu kwamba Serikali ipo tayari kuboresha huduma katika tarafa hiyo, na tutalifanyia kazi, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa wananchi wa Njombe walishakamilisha ujenzi wa vituo vya afya viwili kwenye Kata mbili, Kata ya Mamangolo na Kata ya Kifanya; na tumekuwa tukiomba sana hapa. Nini kauli ya Serikali kuhusu kutoa vifaa tiba kwenye hospitali ili mama mtoto aweze kupata huduma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, baada ya ukamilishaji wa vituo hivyo kinachofuatia ni kutafuta vifaa tiba na ambavyo vipo katika mpango. Kwa hiyo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tunanunua vifaa tiba kwa ajili ya vituo vya afya ambavyo vimeshakamilika. Vitakapokuwa vimepatikana tutavipeleka pale kwa wananchi, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Vit Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 208

**Kudhibiti magari yanayopakia na kupakua mizigo Kariakoo na Barabara ya Morogoro**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani kudhibiti magari yanayopakua na kupakia mizigo katika maeneo ya Kariakoo, Mtaa wa Msimbazi na Barabara ya Morogoro ili kupunguza kero kwa wakazi wa maeneo hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti magari makubwa yanayopakia na kupakua mizigo katika maeneo ya Kariakoo, Mtaa wa Msimbazi na barabara ya Morogoro, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imeweka utaratibu wa kudhibiti magari hayo kwa kutoa vibali Maalum vinavyowaruhusu kuingia mjini kama ilivyotamkwa kwenye kifungu cha 8 cha Sheria Ndogo za Matumizi ya Barabara za Halmashauri ya Manispaa ya Ilala (ambayo ndiyo Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa sasa) za mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, mtu yeyote atakayeingiza lori au kontena bila kibali atakuwa ametenda kosa, na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua Shilingi elfu hamsini hadi laki tatu kulingana na uzito wa gari, au kifungo kisichozidi miezi 12 jela, au vyote kwa pamoja. Hata hivyo, halmashauri kwa kushirikiana na vyombo vingine, ina utaratibu wa kutoa elimu kwa madereva, wamiliki wa magari makubwa na kwa umma ili kuwapa uelewa wa athari zinazotokana na uingizaji wa magari makubwa kiholela.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ina mpango wa kujenga maegesho ya kisasa katika eneo la Mnazi Mmoja kwa ajili ya magari mbalimbali yakiwemo magari ya mizigo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Pamoja na vibali na eneo lililotengwa, lakini bado kadhia ya magari makubwa hupaki, kupakua na kupakia mizigo katika Barabara kama za Nyati, Faru, Tembo na kadhalika inaendelea.

Je, Serikali inaelewa kwamba wafanyabiashara hawa wa mizigo wanawakosesha haki ya kimsingi wanye makazi ya kulala, pia kuharibu utaratibu mzima wa afya ya akili?

Je, ukitokea moto, wakati barabara zote zimezibwa na magari makubwa haya ya mizigo, Serikali haioni kama hilo janga *in the make,* ina mpango gani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, cha kwanza tunatambua haki za msingi za wananchi wa maeneo hayo wanayokaa na kero wanayoipata. Kwa hiyo, kutokana na umuhimu wake, sisi kama ofisi ya Rais TAMISEMI, tunaomba tulipokee na tuangalie namna bora ambayo tunaweza tukaifanya kuchukua hatua za haraka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la msingi, kuhusu majanga ya moto, tumesema moja ya mkakati wetu na mkakati wa Jiji la Dar es Salaam ni kujenga eneo jipya katika eneo la Mnazi Mmoja kwaajili ya maegesho ya magari. Kwa hiyo, kwa kuuliza hili swali la msingi maana yake sasa tutaiharakisha Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ianze huo mkakati hara iwezekavyo ili muondokane na hiyo kero. Ahsante.

Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Maji, Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya sasa ulize swali lake.

Na. 209

**Mradi wa Maji Safi na Salama Kata ya Rabour-Rorya**

**MHE. JAFARI W. CHEGE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka mradi wa maji safi na salama katika Kata ya Rabour?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jafari Wambura Chege Mbunge wa Rorya kama ifuatavyo: -

Mheshimwa Spika, Kata ya Rabour ina jumla ya Vijiji vitatu vya Oliyo, Rabour na Makongoro. Vijiji vya Oliyo na Rabour vinapata huduma ya maji kupitia visima virefu. Katika kuboresha huduma ya maji katika Kata ya Rabour (Kijiji cha Rabour), Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 inatekeleza mradi wa maji katika kijiji hicho. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa tenki lenye ujazo wa lita 225,000 na ujenzi wa mtandao wa usambazaji maji wenye urefu wa kilometa 12.8. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2022 na utanufaisha wananchi wapatao 4,792.

Mheshimwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi ya maji katika Vijiji viwili vya Oliyo na Makongoro. Kukamilika kwa miradi hiyo kutaboresha huduma ya maji safi na salama katika Kata yote ya Rabour.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali lanyongeza. Ni kweli, nikiri kwamba mradi huu unaendelea na utakapokamilika, tuweke rekodi sawa, utanufaisha wananchi 4,792 badala ya laki moja na kidogo.

Mheshimiwa Spika, nataka niulize maswali mawili ya nyongeza pamoja na haya, kwamba wananchi wa kata ile wako zaidi ya 12,000, mradi huu ukikamilika unakwenda kuhudumia wananchi 4,700. Nataka nijue mkakati wa Serikali walionao ili kuhakikisha angalau wananchi wote waliosalia kwa zaidi ya elfu kumi na mbili na kidogo wanaweza kupata maji safi na salama?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kuna kituo cha afya ambacho kinajengwa kwenye kata ile, hivi ninavyozungumza wananchi wanatafuta eneo kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya. Nilitaka nijue kama mpango huu wa mradi huu nao pia utahakikisha maji yanafika kwenye eneo la kituo cha afya ambacho kinajengwa kwenye Kata ile ya Rabour?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Majibu, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chege kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali ni kuhakikisha vijiji vyote vinafikiwa na maji ya bomba yaliyo safi na salama yakiwa ya kutosha. Hivyo niombe Mheshimiwa Mbunge tuendelee kushirikiana, vijiji hivi vyote vitapata maji.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuhusiana na kituo cha afya, nimekuwa nikiongea hapa mara nyingi, tumeshaelekeza watendaji wetu kwenye mikoa yote na wilaya zote kuhakikisha maeneo yote yanayotoa huduma za afya, kwa maana ya vituo vya afya, zahanati hospitali yote yanakuwa na mitandao ya maji safi na salama ya kutosha. Lakini vilevile eneo lake Mheshimiwa Chege nalo ni moja ya maeneo ambayo tunakwenda kuyafanyia kazi na kituo cha afya nacho ni miongoni mwa vituo vitakavyoenda kunufaika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itachimba visima vya maji katika Kata ya Mwabazuru, Budekwa na Busiriri Wilaya ya Maswa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nipende kumpongeza sana Mheshimiwa Esther, amekuwa akifuatilia hivi visima.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuhakikisha maeneo haya yanayohitaji huduma ya maji kupitia visima yanafikiwa, hivyo hata Wilaya ya Magu nayo ni miongoni mwa wilaya ambazo tunakwenda kuzifikia. Mwaka ujao wa fedha tuna visima vya kutosha tulivyovitenga katika bajeti yetu, hivyo tutahakikisha kwamba Magu nao wanapata.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Omar Issa Kombo, Mbunge wa Wingwi.

Na. 210

### Kujenga Ofisi ya Posta Katika Wilaya ya Micheweni

**MHE. OMAR ISSA KOMBO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Ofisi ya Posta katika Wilaya ya Micheweni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Issa Kombo, Mbunge wa Wingwi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukuaji wa teknolojia ya TEHAMA na mabadiliko yanayoendelea ndani ya Shirika la Posta Tanzania *(TPC)* katika utoaji wa huduma kwa njia za kielekitroniki kupitia mawakala, Shirika halijapanga kujenga Ofisi ya kutolea huduma bali litatumia mawakala katika kutoa na kufikisha huduma zake kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Posta Tanzania limepanga kutumia Kituo cha TEHAMA kilichopo Micheweni kinachomilikiwa na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili kutoa huduma za Posta kwa wananchi wa Wilaya ya Micheweni kwa kutumia wakala. Shirika tayari limewasilisha maombi ya kupatiwa nafasi katika Kituo hicho na kukubaliwa. Shirika linakamilisha taratibu ili huduma za posta zianze kutolewa kabla ya mwaka wa fedha 2021/2022 kukamilika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omar Issa Kombo swali la nyongeza.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kweli nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwa kweli ni matumaini yangu kwamba wananchi wa Micheweni watafarajika pindi watakaposikia majibu haya ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo nina swali moja la nyongeza. Mara nyingi imezoeleka katika Shirika la Posta wakati wanapotoa ajira wanachukua waajiriwa kutoka katika maeneo mengine. Je, Mheshimiwa Waziri ananihakikishiaje, pindi watakapofungua ofisi hii katika ajira ambazo watatoa watazingatia kipaumbele au wataweka kipaumbele kwa wananchi wa Wilaya ya Micheweni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Issa Kombo, Mbunge wa Wingwi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi ambayo anaifanya kwa ajili ya wananchi wa Wingwi. Lakini vilevile ameendelea kuhakikisha kwamba anatupatia changamoto zinazoendelea ndani ya jimbo lake. Sisi kama Serikali tunaendelea kuzipokea na kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini pili suala la ajira linafahamika kabisa kwamba mashirika yetu haya yanaajiri kwa kupitia utaratibu wa utumishi wa umma. Hivyo basi, tunaamini kabisa kwamba mfanyakazi yeyote, au yeyote ambaye ni Mtanzania ana haki sawa kuomba kazi na kupatiwa kazi kulingana na vigezo ambavyo vitakuwa vimewekwa.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Baada ya uzinduzi wa *Royal Tour* kumekuwa na ongezeko kubwa sana la watalii ndani ya Jimbo la Hai, lakini moja ya changamoto inayoikumba sekta hii ni mawasiliano. Hoteli za kitalii zilizoko kwenye geti la kuingia Machame ambapo Naibu Waziri ameshafika hazina mawasiliano kabisa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta mawasiliano ndani ya Jimbo la Hai?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni jukumu la Serikali kwa mujibu wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Ibara ya 61(j) inatuelekeza kuhakikisha kwamba tunafikisha mawasiliano kwa Watanzania wote. Vilevile *specifically* kwa maeneo ya Jimbo la Hai mimi binafsi nimeshafika katika maeneo ambayo ameyataja Mheshimiwa Mbunge na kweli kabisa tayari tumeshayachukua na tayari wataalam wameshafanya tathmini na tunayaingiza kwenye mpango wa utekelezaji wa Tanzania ya Kidigitali. Kwa hiyo naomba tuendelee kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge kuhakikisha kwamba mawasiliano tunayafikisha huko, lakini tuwaandae wananchi wetu tutakapohitaji maeneo kwa ajili ya ujenzi wa minara hiyo, watupatie ushirikiano ili mawasiliano yaweze kufika. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Soud.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Katika Jimbo langu la Donge kuna majengo ambayo yamejengwa zaidi ya miaka 20 iliyopita na wenzetu hawa wa Posta na Simu. Majengo yale mpaka leo hayakutumika na yanaendelea kuzeeka na kuchakaa hivi sasa. Sasa namwomba tu Mheshimiwa Waziri kama yuko tayari aidha tufuatane

na kumwomba awaachie wananchi wa Jimbo la Donge watumie yale majengo kwa shughuli zingine za maendeleo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Soud, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shirika la Posta Tanzania majengo yake mengi ni ya siku nyingi, lakini mpango wa uliopo ndani ya shirika letu ni kuhakikisha kwamba tunaboresha vituo vyetu vya mikoani. Kwa majengo yetu yaliyoko katika upande wa wilaya baada ya kukamilisha awamu ya kwanza ambayo ni mikoa baadaye tutashuka mpaka kwenye wilaya na hatimaye majengo yote yataanza kufanya kazi iliyotajiwa na Watanzania. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Daniel Sillo Baran, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa kuna changamoto kubwa sana ya mawasiliano katika Jimbo la Babati Vijijini hasa Tarafa za Bashnet na Goroa na pia Mheshimiwa Naibu Waziri alishafika. Je, ni lini Serilkali itaanza kujenga minara ili wananchi wetu waweze kupata mawasiliano?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Daniel Sillo, Mbunge wa Babati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Sillo kwa sababu nilifanya ziara katika jimbo lake na tulitembea wote na tulijionea hali halisi, lakini habari njema kwa ajili ya wananchi wa Babati ni kwamba kata ambazo amezitaja tayari zipo kwenye mpango wa utekelezaji wetu. Hivyo basi, wananchi wa Babati wasubiri tu hatua za manunuzi zikamilike. Hatua hizo zikishakamilika basi nimwombe Mheshimiwa Mbunge tuendelee kushirikiana kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanatupa maeneo ambayo hayana migogoro kiasi kwamba tukiweka minara yetu isiingie kwenye migogoro ya ardhi. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, isipokuwa lile swali la Mheshimiwa Soud majengo kukaa muda mrefu wakati ametumia fedha si jambo jema.

Nadhani pamoja na kwamba mna mpango kabambe wa Taifa zima yatazameni yale kwa namna ya kipekee, labda hata mpangishe yawe yanatumika kwa sababu yataharabika kabla hata hamjaanza huo mpango wenu. Tunawakushukuru sana kwa majibu yenu kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, Mbunge wa Malinyi, sasa aulize swali lake.

Na. 211

**Utaratibu wa Kuwaachia Makusanyo *TANAPA***

**MHE.ANTIPAS Z. MGUNGUSI** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kurekebisha utaratibu wa kuwaachia makusanyo ya fedha Jeshi la Uhifadhi hasa *TANAPA?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, Mbunge wa Malinyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kupongeza Serikali ya Awamu ya Tano na Sita kwa kuendelea kutekeleza takwa la kisheria la kuhakikisha makusanyo yote yanaingia kwenye kapu moja (Mfuko Mkuu wa Serikali). Katika kuendelea kutekeleza takwa hilo, Serikali ilibadili Sheria ya Fedha ya mwaka 2020 ambapo jukumu la kukusanya mapato yasiyo ya kodi ikiwemo ya Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania *(TANAPA)* lilikasimiwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2019/2020, mapato ya Jeshi la Uhifadhi *(TANAPA)* yalishuka kutokana na kushuka kwa ukusanyaji wa mapato kulikosababishwa na kupungua kwa wageni kufuatia makatazo ya kusafiri na kufungiwa *(lockdown)* baada ya kuibuka kwa janga la UVIKO-19. Hii ilisababisha Jeshi la Uhifadhi (*TANAPA)* kushindwa kumudu gharama mbalimbali za uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizo za kimapato, Serikali iliamua kugharamia shughuli zote za uhifadhi ikiwemo kulipa mishahara ya watumishi na kutoa ruzuku ya kugharamia matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Aidha, katika kuhakikisha Jeshi la Uhifadhi *(TANAPA)* halikwami katika utekelezaji wa majukumu yake kwa wakati,

Serikali imekuwa ikitoa fedha za matumizi kwa Shirika la Hifadhi za Taifa (*TANAPA)* miezi miwili kabla yaani *advance disbursement*. Hata hivyo, Serikali itaendelea kufanyia kazi hoja ya Mheshimiwa Mbunge wakati ikiendelea na utaratibu huu hadi hapo itakapoona kama kuna uhitaji wa kubadilisha Sheria.

**SPIKA:** Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, swali la nyongeza.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali ambayo sijaridhika sana. Kimsingi nilitarajia nijibiwe swali na Wizara ya Fedha, lakini hamna shida kwa sababu Serikali ni moja. Ilikuwa ni nia njema ya Serikali kuokoa Jeshi la Uhifadhi kwa maana ya kufanya operesheni zake kutokana na uwezo wao mdogo wa kuingiza mapato kipindi cha *COVID*. Sasa hivi kuna jitihada mbalimbali ambazo zinafanywa na Serikali hasa Mheshimiwa Rais katika kuifungua nchi. Tunatarajia wageni watakuwa wengi na Jeshi la Uhifadhi litaweza kujiimarisha. Je, Serikali haioni haja sasa kubadilisha sheria ili *TANAPA* na TAWA waweze kukusanya fedha zao wenyewe na kuendelea kupeleka gawio Serikalini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Antipas Mgungusi, Mbunge wa Malinyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwenye jibu la msingi nimesema wazi kabisa kwamba ni vyema fedha yote inapokusanywa ikaingia kwenye kapu moja ili kuona hata vyanzo vyetu vya mapato tunapataje. Pamoja na yote hayo maelezo yangu yalikuwa ni kwamba kipindi hiki ambacho sasa tumeanza kuimarika, bado tunachechemea, nikimaanisha kwamba Serikali bado inalisaidia hili Shirika la Uhifadhi *(TANAPA)*. Kwa hiyo tutakapofikia mahali ambapo tunasimama wenyewe basi Serikali itaona kama kuna haja ya kubadilisha sheria tutaleta ndani ya Bunge lako Tukufu na sheria itaendelea kurekebishwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Mgogoro kati ya Pori la Usumbwa *Forest Reserve* na Pori la Hifadhi ya Taifa Kigosi Moyowosi umedumu kwa muda mrefu sana. Sasa je, ni lini Serikali itaushughulikia mgogoro huu ili kuwapa nafasi wananchi wa Jimbo la Ushetu hasa wanaozunguka Kata za Idahina, Nyankende, Ulewe pamoja na Ubago waendelee na shughuli zao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cherehani, Mbunge wa Ushetu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote niendelee kuwaomba wananchi ambao wanaishi kwenye maeneo haya waendelee kuwa na subira wakati Serikali inaendelea kuangalia namna iliyo bora ya kutatua migogoro hii.

Mheshimiwa Spika, tuna Kamati ya Mawaziri Nane ambayo ina maelekezo kutoka kwa Mheshimiwa Rais kwamba tuzunguke nchi nzima kuhakikisha kwamba tunatatua migogoro hiyo. Sambamba na hilo tumezielekeza taasisi, endapo kuna migogoro mipya ambayo haimo ndani ya hii migogoro inayotatuliwa na Kamati ya Mawaziri Nane basi tuanze pia kuangalia mchakato mpya kuangalia namna iliyo bora ili tuweze kutatua migogoro hiyo. Kwa hiyo, niwaombe wananchi wote ambao wana migogoro mipya katika maeneo yao Serikali inaendelea kuyafanyia kazi ili tuone njia iliyo bora ya kutatua migogoro hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dokta Charles Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii, nina swali dogo gu. Kwa vile Serikali imetuhakikishia kwamba Mamlaka za Hifadhi za Misitu na Wanyamapori wana wajibu wa kutoa *CSR* kwa vijiji vinavyozunguka hifadhi hizi. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuziagiza mamlaka hizi ziweke bayana kiasi cha ufadhili ambazo zimetolewa kwa vijiji hivyo ndani ya miaka mitatu iliyopita? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kimei, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote niwaombe sana wananchi wanaozunguka maeneo ya hifadhi waamini kwamba Serikali inatambua umuhimu wa mashirikiano ikiwemo miradi ya ujirani mwema.

Mheshimiwa Spika, bajeti zote tunapozileta hapa Bungeni huwa tunaweka kipengele cha miradi ya *CSR*. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba hata bajeti hii tutakayoisoma hivi karibuni itazingatia hilo. Hivyo, niwaombe wananchi wote na Waheshimiwa Wabunge ambao wanazungukwa na maeneo haya yaliyohifadhiwa watarajie kuona *CSR* katika maeneo yao. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cosato Chumi, swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Jitihada za Serikali ni pamoja na kuhakikisha kwamba mapato yatokanayo na utalii yanaendelea kuongezeka kwa kuboresha miundombinu na kufanya *marketing* ya utalii. Je, ni lini Serikali itaanza utekelezaji kikamilifu wa Mradi wa *REGROW* ambao ulizinduliwa tarehe 12 Februari, 2018 na Mheshimiwa Makamu wa Rais ambaye sasa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kama unayo majibu kwa ajili ya swali hilo, lakini unao uhuru linaweza kuja kama swali la msingi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *REGROW* ulianza kutekelezwa mwaka 2017, lakini kutokana na changamoto ambazo zilijitokeza, Benki ya Dunia iliweza kuongeza muda mpaka mwaka 2025, ambapo tutamaliza mradi huu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara imeunda Kamati Maalum ambayo itafanya kazi bega kwa bega kuhakikisha eneo hili tunasimamia vizuri kama ambavyo tunasimamia fedha za UVIKO ili kuhakikisha mradi huu unakamilika haraka na kuhamasisha watalii waweze kufika katika maeneo hayo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Aida Khenani.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, kabla swali hili halijaulizwa naomba kuweka masahihisho. Pale iliposomeka Mbao za Mitikiti isomeke Mbao za Mitiki. Kwa niaba ya Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka naomba swali lake namba 212 lipate majibu ya Serikali.

Na. 212

**Kutumia Mbao za Mitiki Kutengeneza Samani za Serikali**

**MHE AIDA J. KHENANI K.n.y. MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA** aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali isitumie mbao za Mitiki zenye ubora sawa na Mninga/Mkongo kwani tenda za Serikali zinataka Mninga/Mkongo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, shughuli za ujenzi na utengenezaji wa samani ambazo kiuhalisia zimekuwa zikikua sambamba na ongezeko la watu, zinategemea sana rasilimali ya misitu kama chanzo cha malighafi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kukua kwa mahitaji na changamoto ya upatikanaji wa miti migumu kutoka katika misitu ya asili hasa jamii ya mninga na mkongo, Wizara imefanya utafiti kuhusu tabia na sifa za mbao za matumizi kutoka kwenye miti isiyofahamika sana. Utafiti huo uliolenga kutambua tabia na sifa za kimwonekano, kiufundi na kianatomiki za mbao za miti isiyojulikana sana, ulionesha kuwa mti wa mitiki, una sifa ama sawa au zinazokaribiana sana na miti ya mkongo na mninga.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia matokeo ya utafiti huo, Serikali inaangalia uwezekano wa kuongeza miti mipya iliyofanyiwa utafiti katika orodha ya miti iliyoainishwa katika Sheria ya manunuzi inayosimamiwa na *PPRA* ili itumike katika kutengeneza samani za Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Sote tunajua kwamba bado kuna changamoto kubwa sana ya madawati hapa nchini na wananchi wamekuwa ni wahifadhi namba moja wa misitu pamoja na miti mingine ambayo inapandwa na Watanzania wenyewe. Serikali ina mpango gani sasa wa kutumia miti mingine ambayo inataka kufanana na mininga ambayo iko maeneo mengi ili kuweza kuondoa changamoto hiyo ya madawati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kaboyoka, kwa niaba yake ameuliza Mheshimiwa Aida, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza niweze kuifahamisha jamii na Watanzania wote kwamba, Serikali imefanya utafiti wa miti 19 na moja ya utafiti huu ni pamoja na mti wa mtiki. Tunaangalia namna iliyo bora ya kufanya mazungumzo na Wizara ya Fedha kupitia *PPRA* ili kuwe na mwongozo maalum wa kuhakikisha kwamba miti hii sasa inatumika kwenye *furniture*. Kwa hiyo nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba changamoto ya madawati ambayo imekuwa ikijitokeza katika jamii inaenda kupungua kwa sababu aina ya miti 19 kama itaenda kutengeneza haya madawati, basi kutakuwa na aina mbalimbali ya miti ambayo ni mizuri na bora na imefanyiwa utafiti na wataalam kutoka Maliasili na Utalii. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolijia Mheshimiwa Husna Juma Sikiboko, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 213

**Kukithiri kwa Uvujaji wa Mitihani Nchini**

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO** aliuliza:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kukomesha kuvuja kwa mitihani nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kwa lengo la kukomesha tabia ya udanganyifu katika mitihani ya Taifa ikiwemo mitihani ya kumaliza elimu ya msingi, sekondari na vyuo. Hatua hizo ni pamoja na kutoa elimu kwa walimu, wasimamizi wa mitihani na wadau wote wa elimu kuhusu athari za udanganyifu katika mitihani ili kuhakikisha kuwa wanatekeleza jukumu la usimamizi wa mitihani hiyo kwa uadilifu na kwa kuzingatia kanuni, taratibu na miongozo iliyowekwa kwa ajili ya uendeshaji wa mitihani.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine zilizochukuliwa kutokana na udanganyifu katika mitihani ni hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria za nchi. Hatua hizi zimekuwa zikichukuliwa kwa Walimu, wasimamizi na wadau wote wanaohusika katika kusimamia mitihani pale ambapo ilibainika pasina shaka kuwa walishiriki katika kosa hilo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuwachukulia hatua kali kwa mujibu wa sheria wahusika wote wanaojihusisha na udanganyifu wa mitihani ili kuhakikisha kuwa nchi inapata wataalam wenye sifa stahiki. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Husna Sekiboko, swali la nyongeza.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua ambazo zinachukuliwa na Serikali bado tabia ya kuvujisha mitihani

imeendelea. Ni vipi Serikali inaenda kukomesha tabia hii? Nadhani ndiyo swali langu la msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mara nyingi tumeshuhudia wazazi na watoto wasio na hatia kubebeshwa mzigo wa kufutiwa matokeo na muda mwingine shule kufungwa. Ni kwa namna gani Serikali itaondoa mzigo huu kwa wazazi na watoto wasio na hatia?*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, Ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Husna Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum, nitajibu maswali mawili yote kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa suala la uvujaji wa mitihani halipo, mara ya mwisho mitihani ilivuja mwaka 2008 na ulikuwa ni mtihani mmoja wa somo la hisabati Kidato cha Nne. Kutoka mwaka 2008 hakujawahi kutokea uvujaji wa mitihani.

Mheshimiwa Spika, kinachotokea ni udanganyifu katika mitihani kwenye baadhi ya maeneo, kwa sababu suala la mitihani ni suala la mchakato ambayo inahusisha utungaji wa mitihani, ufungaji wa mitihani, usafirishaji wa mitihani lakini baadaye tunakwenda kwenye vituo vya kufanyika mitihani. Kwa hiyo, matukio ya udanganyifu kwenye baadhi tu ya maeneo baada ya mitihani kufunguliwa na kuingia kwenye vyumba vya mitihani, vijana au Walimu au Wasimamizi wamekuwa labda wakiingia na nyaraka ambazo hazitakiwi kwenye ufanyikaji wa mitihani, pale ndipo inatokea udanganyifu wa mitihani. Lakini suala la uvujaji wa mitihani tulishalitokomeza kama Serikali na sasa hivi tunapambana na suala hili la udanganyifu wa mitihani ndipo tunaona kwamba wale wanaohusika kwenye udanganyifu ndiyo wanaochukuliwa hatua.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mliosimama nimewaona lakini niwakumbushe swali la msingi linahusu kuvuja kwa mitihani au udanganyifu kwenye mitihani. Mheshimiwa Maimuna Mtanda.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Serikali ina mpango gani wa kuongeza posho kwa usimamizi wa mitihani, kwa sababu zoezi la usimamizi wa mitihani ni gumu wakati mwingine linagharimu ustawi wa maisha ya msimamizi husika?

**SPIKA:** Mheshimiwa posho inachangia kwenye udanganyifu na kuvuja kwa mitihani. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Maimuna Mtanda Mbunge wa Newala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge. Hivi sasa taratibu za usahihishaji wa mitihani tunakwenda kubadilika kwa sababu tunakwenda kwenye *e-marking*. Tumeanza kwa mitihani ya Darasa la Saba na sasa hivi tuko kwenye *pilot* ya mitihani ya Ualimu na baadae tutakwenda kwenye mitihani ya *Form Four* na *Form Six*. Kwa hiyo kwanza tutapunguza sana gharama za Walimu kusogea kwenye maeneo yale ambayo tunasahihisha mitihani badala yake mitihani itakuwa inasahihishwa huko huko Mikoani.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo wakati tunakwenda kuboresha mifumo hii ya usahihishaji wa mitihani vilevile tunakwenda kuboresha na posho zile za wasahihishaji wa mitihani na wale wataokuwa wanasimamia mitihani hii. Kwa hiyo nimwondoe wasiwasi hili tayari liko kwenye bajeti zetu na linakwenda kukaa sawasawa. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, Serikali inachukua hatua gani ya kudhibiti udanganyifu badala ya kusubiri udanganyifu ndiyo mnatoa adhabu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Maryam kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyozungumza kwenye majibu yangu ya msingi jukumu letu kama Wizara, jukumu letu kama Serikali ni kuhakikisha kwamba tunatoa elimu ya kutosha ya athari za udanganyifu wa mitihani kwa wasimamizi vilevile kwa wale wanafunzi ambao kwa namna moja au nyingine wanaathirika kwa kiasi kikubwa kwenye zoezi hili. Kwa hiyo, jukumu letu ni kuhakikisha kwamba tunatoa elimu watu wasifanye udanganyifu katika mitihani kwa sababu athari zake ni kubwa kwa wao wenyewe binafsi lakini na kwa Taifa kwa ujumla. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi swali la nyongeza.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Serikali inatumia Polisi kusimamia mitihani ya wanafunzi. Je, haioni kwa kutumia Polisi wanafunzi wanapata taharuki na kushindwa kufanya mitihani yao kwa uhuru? ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Yustina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge. Polisi hawaendi kusimamia mitihani, kwa sababu hakuna Polisi ambaye anaingia kwenye chumba cha mtihani. Polisi ni sehemu ya kikosi kazi au ni sehemu ya Kamati zetu ambazo zinaratibu pamoja na kuhakikisha kwamba usalama wa kituo cha mtihani pamoja na uhifadhi wa mitihani yetu. Lakini hakuna Polisi ambaye anaingia ndani ya chumba cha mtihani na kuanza ku-*invigilate* wale wanafunzi wakati wanaendelea na mchakato wa mtihani. Lakini wako pale kwa mujibu wa sheria kuhakikisha kwamba usalama wa kituo pamoja na usalama wa mitihani yetu pale inapohifadhiwa pamoja na ufanyikaji inakwenda sawasawa lakini siyo kuingia ndani ya kituo au darasa ambalo mitihani inafanyika.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Michael Kembaki swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mtihani wa Darasa la Saba mara nyingi unafanyika mwezi wa Tisa na mtaala unapaswa ukamilike mwezi wa Kumi na Moja. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba wanafunzi wale wa Darasa la Saba wanamaliza mtaala wao kabla ya kufanya mtihani wa mwezi wa Tisa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri hilo utaleta majibu kama swali la msingi, Mheshimiwa Mussa Sima.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Suala la uvujaji wa mitihani ni ukosefu wa maadili wa kuanzia anayeandaa, mratibu na anayesimamia. Sasa nataka kujua mkakati wa Serikali ambao unaenda kusaidia suala hili la ukosefu wa maadili ni upi? ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Sima kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye majibu yangu ya swali la msingi kwamba uvujaji wa mitihani kwa mara ya mwisho ulitokea mwaka 2008. Na kama alivyozungumza Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hili ni suala la kimaadili na sisi kama Serikali wajibu wetu ni kuhakikisha kwamba tunakwenda kutoa elimu kuanzia kwa wale ambao wanaotunga mitihani vilevile wale wanaofunga, wanaosafirisha mpaka wale ambao wanakwenda kusimamia zoezi hili la ufanyikaji wa mitihani.

Kwa hiyo tunafahamu ni suala la kimaadili na tumekuwa tukitoa mavunzo ya athari za uvujaji wa mitihani kwa namna moja au nyingine, lakini nimwondoe wasiwasi kwa kiasi kikubwa na kama tukichukua takwimu kwa mara ya mwisho tukizungumza hilo suala la udanganyifu tu mwaka 2011 udanganyifu ulifanyika kwa wanafunzi 9, 736.

Mheshimiwa Spika, lakini mwaka 2021 ni wanafunzi 393 tu ndio ambao walifanya udanganyifu kwenye mitihani. Kwa hiyo tunaendelea kudhibiti na tunaamini baada ya muda si mrefu tunaweza tukapata *achievement* kubwa kuhakikisha kwamba hakuna mtu ambaye atajihusisha na udanganyifu wa mitihani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan Mbunge wa Chakechake sasa aulize swali lake.

Na. 214

**Hitaji la Askari Polisi Kusini Pemba**

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuajiri Askari wa Jeshi la Polisi katika Mkoa wa Kusini Pemba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Ramadhan wewe tayari hapa uko kwa niaba yao kwa hiyo unaenda moja kwa moja kuuliza swali wamekuchagua wewe kwa ajili ya kazi hiyo. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan Mbunge wa Chakechake, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2021/2022, Serikali imetoa kibali cha kuajiri askari wapya wa Jeshi la Polisi 4,103. Kwa sasa askari hao wapo kwenye mafunzo ya awali katika shule ya Polisi Moshi. Watakapomaliza mafunzo yao, watagawiwa kwenye maeneo yenye upungufu mkubwa wa askari ikiwemo mkoa wa Kusini Pemba. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan swali la Nyongeza.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kutokana na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye swali langu la msingi nina swali moja la nyongeza.

Kwenye jibu lake la msingi amekiri kwamba upo uhaba wa Askari Polisi katika Mkoa wa Kusini. Je, ni ahadi gani ya Serikali kwamba watatoa kipaumbele kwenye hizo ajira 4,103 alizozitaja maalum kwa ajili ya Mkoa wa Kusini Pemba? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan Mbunge wa Chakechake kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi ahadi yetu ni kwamba hawa wahitimu wa mafunzo ya Jeshi la Polisi 4,103 watagawiwa maeneo yote yenye upungufu ikiwemo Mkoa wa Kusini Pemba. Kama tulivyokubaliana Mheshimiwa Ramadhan nitakwenda huko baada ya Bunge hili ili kuangalia pamoja na mambo mengine upungufu huo na kiwango kinachohitajika kusaidiwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Haji Makame Mlenge Mbunge wa Chwaka sasa aulize swali lake.

Na. 215

**Mpango wa Kupunguza Msongamano wa Watu Wanaofuatilia Hati za Kusafiria**

**MHE. HAJI MAKAME MLENGE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza msongamano wa watu wanaofuatilia hati za kusafiria?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haji Makame Mlenge, Mbunge wa Chwaka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Idara ya Uhamiaji katika kupunguza msongamano wa waombaji wa Hati za kusafiria, imefunga mifumo ya kielektroniki ya utoaji wa hati za kusafiria katika Mikoa yote ya Zanzibar. Ufungwaji wa mifumo hiyo kumeondosha msongamano kwa wananchi katika Ofisi Kuu kwani kwa sasa wananchi wanaweza kuomba na kufuatilia maombi ya Hati za kusafiria katika Mkoa wowote anaoishi. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Haji Makame Mlenge swali la nyongeza.

**MHE. HAJI MAKAME MLENGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mbali na majibu mazuri ya Serikali naomba niulize masuala mawili ya nyongeza. Kwa kuwa watoa hati ni wanadamu na wanadamu wana kawaida ya wakati mwingine kukosea. Inapotokea kukosea wakati wa kutoa hati *(printing error)* na wakati huo wale wapewa hati wanakuwa wameshalipa. Kwa nini idara inawalipisha tena watu wale wakati wao Uhamiaji ndiyo wamekosea?

Mheshimiwa Spika, swali la pili Je, Serikali ipo tayari kutoa tamko kupitia Waziri la kwamba suala hili wapewa hati hawatalazimika kulipishwa mara ya pili badala yake gharama hizi wachukue Idara? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Haji Makame Mlenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna wakati makosa hufanyika lakini makosa yakichunguzwa yakionekana aliyechangia kufanya makosa haya ni yule mwombaji kwa sababu ya taarifa alizojaza basi mwombaji huyo lazima atalipa. Lakini ikiwa itathibitika kwamba makosa hayo yanatokana na waandaaji ambao ni watumishi wa Idara ya Uhamiaji basi tutaangalia uzito wake ili waweze kufidia wenyewe utoaji wa hati hizo mpya. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwa Wabunge na majibu kutoka Serikalini. Nilete matangazo tuliyonayo kabla hatujaendelea na ratiba yetu. Tunalo tangazo la wageni walioko hapa Bungeni siku ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza ni wageni walioko Jukwaa la Spika na hawa ni wageni wa Mheshimiwa Hussein Bashe, Waziri wa Kilimo ambao ni Watendaji Wakuu wa Wizara hiyo.

Yupo Ndugu Andrew Massawe ambaye ni Katibu Mkuu, karibu sana; yupo pia Profesa Siza Tumbo ambaye ni Naibu Katibu Mkuu, karibu sana; yupo pia Ndugu Gerald Mweli ambaye ni Naibu Katibu Mkuu, karibu sana; wapo Wakurugenzi wa Wizara ya Kilimo, Watendaji Wakuu wa Bodi na Taasisi za Wizara ya Kilimo, Maafisa Kilimo kutoka ngazi ya Halmashauri na Makao Makuu ya Wizara ya Kilimo, hawa wasimame wote kwa pamoja; karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wadau wa maendeleo wa sekta ya kilimo hawa nao wasimame, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunazo taasisi za fedha na sekta binafsi, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye Mwekezaji Sekta ya Kilimo na Mbunge Mstaafu Mheshimiwa Peter Serukamba, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao Wajumbe wa Sekretarieti ya Chama cha Mapinduzi kutoka Makao Makuu, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi wanne wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi kutoka Chuo cha Afya Mvumi, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge kwanza ni wageni sita wa Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde ambaye ni Naibu Waziri wa Kilimo na hii ni familia yake kwanza yupo mke wake Jacqueline Lupasa, karibu sana na ameongozana na watoto wake Atara Mavunde na Allan Mavunde, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Pauline Gekul, Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo na huyu ni mtangazaji wa *Star TV* kipindi cha Kamusi ya Mtaa kutoka Mkoani Mwanza, Ndugu Queen Yusuph, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni 17 wa Mheshimiwa Deo Mwanyika ambao ni Madiwani kutoka Njombe Mjini wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Erasto Mpete, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni 10 wa Mheshimiwa Deo Mwanyika ambao ni wakulima na wazalishaji wa miche ya parachichi kutoka Mkoani Njombe wakiongozwa na Ndugu Rebecca Hopelwa, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni 15 wa Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma ambao ni wajumbe kutoka Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania *(MVIWATA)*, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Nashon Bidyanguze ambaye ni rafiki yake kutoka Sunuka Mkoani Kigoma, Mchungaji Israel Kitambala, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Boniphace Butondo ambao ni viongozi wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi kutoka Kishapu, Mkoani Shinyanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Shally Raymond ambaye ni wifi yake kutoka Musoma Mkoani Mara Ndugu Esther Mushi, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 38 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni Wanamaombi kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Maimuna Mtanda ambaye ni mtoto wake kutoka Tandahimba, Mkoani Mtwara na huyu ni Ndugu Juma Njwayo, yuko upande gani? Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wawili wa Mheshimiwa Neema Mwandabila ambao ni makada wa Chama cha Mapinduzi kutoka Mkoani Songwe, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Zulfa Omar ambao ni familia yake kutoka Mkoa wa Kusini Pemba wakiongozwa na na mama yake mzazi Ndugu Mafunda Rubea, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Salim Mussa Omar ambaye ni Afisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya *Amour Auto Electronic* inayoshughulika na programu ya funguo za *sensor* na *remote* za magari ya kisasa iliyopo Magomeni Mikumi Jijini Dar es Salaam, Ndugu Amour Seif Abdallah, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Cecil Mwambe ambao hapa wameandikwa ni ma-*designer.* Jamani wale wataalam wa Kiswahili inabidi wawe wanatufundisha hapa kidogo. Haya, wabunifu walioshona nguo za Maafisa Ugani Tanzania wakiongozwa na Ndugu Caren Ibrahim (Carenitho) kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Bila shaka Maafisa Ugani ni wale wamevaa kijeshijeshi pale juu, hebu wasimame tuwaone vizuri. *(Makofi)*

Sasa Maafisa Ugani wetu mmebadilisha muonekano, tunataraji na kazi nazo zitabadilika. Tunatarajia utendaji kazi wenu kule tusiwe tunakuta mahindi yamenyauka nyauka halafu ninyi mnayapita tu, mnaona huyu mkulima sijui vipi. Unamwona pale na mahindi hayana tija na unamwangalia tu anapalilia. Kwa hiyo, kwa mavazi haya tunaamini mtakitizama kilimo kijeshi. Tunawatakiwa kila la heri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, niwakumbushe upande Serikali, leo sitazitaja Wizara, lakini ziko Wizara ambazo bado zinaleta majibu ya maswali ya msingi marefu. Ziko Wizara ambazo leo sitazitaja, zinaleta majibu ya maswali ya msingi marefu.

Niwakumbushe kwamba tulikubaliana maswali lazima yajibiwe nusu ukurasa. Mnapitiliza ukurasa au mnaweka maandishi madogo. Sasa ule siyo ujanja. Hapa mbele tunaweza kujua kwamba majibu haya ni marefu au ni mafupi. Nenda moja kwa moja kwenye jibu linalotakiwa.

Waheshimiwa Wabunge, liko jambo lingine la msingi sana ambalo katika juhudi zinazofanywa na Serikali za kubana matumizi, kuna jambo ambalo nimekumbushwa leo asubuhi. Magari ya viongozi ikiwa ni pamoja na Mawaziri na Naibu Mawazi yanaendelea kuwaka hapo nje wakati sisi tupo humu ndani. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mjue, pia upande wa Serikali tunatamani tuone magari ya viongozi yakishamshusha kiongozi, siyo tu hapa Bungeni; nchi nzima, ikishamshusha awe ni Mwenyekiti wa Halmashauri, awe ni Meya, awe ni Katibu Mkuu au Kiongozi yeyote ukiacha wale viongozi ambao kwa itifaki yao inabidi magari yaendelee kuwaka, magari mengine yote inabidi wakishamshusha kiongozi yazimwe na dereva ashuke humo kwenye gari. Kwa sababu matumizi ya pesa kwenye eneo la mafuta yanakuwa makubwa sana kwa sababu ya magari kuendelea kuwaka wakati kiongozi hayupo kwenye gari, ameshashuka, ana Mkutano wa saa mbili au saa moja, gari inaendelea kuwaka. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hilo mlitazame na Mheshimiwa Waziri Mkuu uko hapa, tunatamani tuone mabadiliko kwenye hilo eneo ili matumizi ya Serikali yapungue kwenye eneo la mafuta. Hili ni la muhimu kwa sababu hata sisi tunapokuwa tunaendesha magari yetu binafsi, ukikwama tu kwenye foleni kidogo unazima. Sasa iweje gari ya Serikali Kiongozi umemshusha kwa ajili ya kwenda kwenye Mkutano unamsubiria kwenye gari ukiwa umewasha gari? Ni matumizi mabaya ya fedha za Serikali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Sasa nimesikia watu wawili wakisema Mwongozo wa Spika. Mheshimiwa Jafari Chege.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nasimama kwa Kanuni ya 76 kuomba Mwongozo wako kwa jambo ambalo limetokea muda siyo mrefu ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri akinijibu swali langu la msingi lililokuwa linahusiana na upatikanaji wa maji wa Kata ya Rabour na Vijiji vyake vitatu, kuna *figure* ambayo ameitaja kwamba baada ya mradi ule kukamilika unategemea kuhudumia wananchi 407,092 lakini kiuhalisia kwa mujibu wa…

**SPIKA:** Laki nne na ngapi?

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** …elfu saba na tisini na mbili.

Mheshimiwa Spika, kwa uhalisia kwa mujibu wa Ofisi ya Takwimu ya Kata ile ya mwaka 2016, Kata ile ina watu 12,492 peke yake. Sasa nikataka nipate Mwongozo wako kwa sababu yale yalikuwa ni majibu ya Serikali ambayo yatabaki kwenye kumbukumbu za Bunge kwa maana ya Bunge hili, lakini pia yanaweza yakatengeneza taharuki ndani ya Wilaya yangu, kwa sababu hata idadi ya wananchi wa Wilaya ile bado kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012 ni watu 265,000, hatujafika watu 400,000. Sasa wanaweza wakaamini kwamba kwa majibu ya Serikali ya leo kwamba mradi huu unakwenda kutekeleza idadi ya watu 400,000 na kitu. Maana yake ni Jimbo zima litakuwa *covered* na mradi wa Kata moja ya Rabour.

Mheshimiwa Spika, nataka tu nipate Mwongozo wako kama hii ni sahihi au labda kidogo kulikuwa na makosa kwenye matamshi ya ile namba ili tuweke sawasawa kwenye kumbukumbu za Bunge na pia wananchi nao wajue kwamba mradi ule ume-*target* kuhudumia watu wa kipande kipi?

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya. Ngoja kabla hujakaa. Umesema Naibu Waziri amesema 400,792.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, naam.

**SPIKA:** Nawe unajua wakazi wako 14,000…

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Elfu kumi na mbili mia nne na tisini na mbili.

**SPIKA:** Elfu ngapi?

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Elfu kumi na mbili mia nne na tisini na mbili. Hiyo ni kwa mujibu wa Ofisi ya Takwimu ya mwaka 2016.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Husna Sekiboko.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, nasimama kwa Kanuni ya 76 kuomba Mwongozo wako. Wakati Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu anatoa majibu kuhusu swali langu la msingi, alilieleza Bunge kwamba mitihani haijawahi kuvuja tangu mwaka 2008; lakini Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii tulipewa kazi na Spika ya kujadili mitihani iliyovuja mwaka 2021 mwezi wa Kumi ambayo ni Mitihani ya Vyuo vya Afya inayosimamiwa na vyuo vya *NACTE*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako katika jambo hili. Mitihani iliyovuja mwaka 2021 ambayo inasimamiwa na *NACTE* ilikuwa ni jambo gani kama siyo kuvuja wa Mitihani? *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wamesimama Wabunge wawili hapa wakiomba Mwongozo wa Kiti kwenye hoja zao mbili tofauti. Mheshimiwa Jafari Chege akitaka kujua kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 76 kama takwimu alizozitaja Mheshimiwa Naibu Waziri wakati akijibu swali lake ambalo lilikuwa ni swali namba 209 wakati akijibu swali la nyongeza, kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri amesema wananchi watakaohudumiwa baada ya mradi wa maji ambao aliutaja ukikamilika watakuwa ni wananchi 400,792; lakini Mheshimiwa Mbunge wa eneo husika na mwenye swali na ambaye ndio ameomba Mwongozo amesema eneo hilo ambalo linatarajiwa kuhudumiwa na mradi huu lina idadi ya watu 12,492.

Sasa Kanuni yetu ya 76 huwa inataka, unapoomba Mwongozo unakuwa unauliza kama hilo jambo ambalo limefanyika hapa ndani linaruhusiwa ama haliruhusiwi. Sasa kuhusu hizi takwimu Mheshimiwa amesema anataka kujua sasa hizi zinaweza kuleta taharuki, watu wakasema huu mradi aidha sisi watu wa hapa ndio tumeongezeka sana ama huu mradi unaenda kuhudumia eneo kubwa zaidi.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, hizi takwimu za laki nne ni kubwa sana. Kwa hiyo, hazina uhalisia, lakini hii ya 12,000 huenda ikaongezeka kwa sababu tunaenda kwenye sensa sasa. Kwa hiyo, hakuna takwimu ambazo ni za uhakika hapo. Bila shaka hizi laki nne zimezidi sana kwenye ile idadi.

Kwa hiyo, kwa upande wetu sisi kwa sababu umeliomba hapa ili Taarifa zetu Rasmi za Bunge zikae vizuri, tutalitazama lile jibu alilolitoa Mheshimiwa Naibu Waziri na tutafanya marekebisho ili taarifa zetu zikae

sawasawa kwa takwimu zilizopo sasa kwa huo mradi kuhusu idadi ya watu unaoenda kuhudumia. Kwa hiyo, huo ndiyo Mwongozo wetu, tutafanya hayo marekebisho kama ulivyoomba Mheshimiwa Mbunge.

Pia amesimama Mheshimiwa Husna Sekiboko kwa Kanuni hiyo hiyo ya 76 akiomba Mwongozo kuhusu majibu ambayo yametolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa ELimu, Sayansi na Teknolojia ambayo yameashiria kwamba kuvuja kwa mitihani mara ya mwisho ilikuwa ni 2008; na Mheshimiwa Husna Sekiboko anasema mwaka jana walipewa kazi ya kutazama hoja ambayo ilikuwa inahusu kuvuja kwa mitihani inayosimamiwa na *NACTE*. Mwaka jana maana yake ni 2021. Sasa wakati Mheshimiwa Naibu Waziri akijibu swali hapa kulikuwa na mambo mawili; moja, ni udanganyifu kwenye mitihani, la pili ni kuvuja kwa mitihani.

Sasa kuvuja amesema ilikuwa mwisho 2008, lakini udanganyifu ni ule ambao unaendelea na wanatoa adhabu kulingana na lile linalotokea. Sasa ili kujiridhisha kuhusu hilo ambalo Kamati ya Huduma za Jamii lilipewa kama ilikuwa ni kuhusu kuvuja kwa mitihani au udanganyifu kwenye mitihani, hilo nitalitolea Mwongozo nikishajiridhisha ni jambo lipi kati ya hayo mawili.

Kwa hiyo, Mwongozo wangu kuhusu hoja ya Mheshimiwa Sekiboko nitautoa hapo baadaye nikishajiridhisha hizo tofauti mbili na ni jambo gani ambalo Kamati ilielekezwa ilitizame; kama ilikuwa ni kuvuja kwa mitihani au ilikuwa ni udanganyifu. Kwa sababu kuvuja pia ni sehemu ya kupelekea udanganyifu. Kwa hiyo, sijui ni lipi kati ya hayo mawili. Nikishayatazama nitatoa Mwongozo kuhusu majibu ya swali hilo.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa na ratiba iliyo mbele yetu. Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, namwita sasa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, aje awasilishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nashukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kutukutanisha leo kwa ajili ya kujadili Taarifa ya Utekelezaji kwa mwaka 2021/2022 na Mpango wa Bajeti 2022/2023 ya Wizara ya Kilimo ambayo inagusa maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba nimpongeze Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza mwaka mmoja tangu ashike nafasi ya kuongoza nchi yetu. Katika kipindi hicho Sekta ya Kilimo imeongezewa bajeti katika maeneo ya utafiti wa kilimo, huduma za ugani, umwagiliaji na uzalishaji wa mbegu na kuimarisha masoko ya mazao ya kilimo. Aidha, niungane na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu kuendelea kumwombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumpa afya njema ili awatumikie Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Daktari Philip Isdor Mpango Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu yake ikiwemo kuhimiza kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi na yeye mwenyewe kuwa mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake za kusimamia na kuendeleza mazao ya kilimo na maendeleo ya ushirika nchini na yeye kuwa mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nakupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, niwapongeze Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge; Mheshimiwa Najma Murtaza Giga na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile kwa kuendelea kukusaidia kikamilifu katika kutekeleza majukumu ya kuliongoza Bunge letu Tukufu. Nawapongeza pia Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuniteua kuwa Waziri wa Kilimo. Naahidi kwa Mheshimiwa Rais, Chama cha Mapinduzi, wananchi wa Jimbo la Nzega Mjini na Watanzania wote kwa ujumla kwamba nitatumikia nafasi ya Ubunge na Uwaziri kwa bidii, maarifa, weledi na uadilifu ili kuweza kufikia malengo yaliyoanishwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi na matarajio ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa furaha nampongeza Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, Mbunge wa Jimbo la Dodoma Mjini kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Kilimo. Nitashirikiana naye kikamilifu katika kuleta mageuzi kwenye Sekta ya Kilimo nchini na hivyo kuwaletea wananchi maendeleo na

kuondoa umasikini na kuifanya Sekta ya Kilimo kuwa msingi mkuu wa ajira nchini. Pia namkaribisha Bwana Gerald Mweli, Naibu Katibu Mkuu aliyehamishiwa Wizara ya Kilimo kutoka Ofisi ya Rais, *TAMISEMI*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Uwenyekiti ya Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum na Makamu Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini kwa ushirikiano mzuri na ushauri makini ambao wameendelea kuutoa kwetu wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji ya Mpango wa Bajeti ya mwaka 2021/2022 na Mpango wa Bajeti ya Kilimo ya mwaka 2022/2023. Ushauri wao umezingatiwa na tunaahidi kuendelea kushirikiana kwa ukaribu na Kamati katika kuendeleza kilimo hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Kamati ya Bajeti kwa maoni na ushauri walioutoa wakati wa majadiliano ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo. Napenda kutumia fursa hii kuihakikishia kuwa maoni na ushauri umezingatiwa kwenye mpango na pia utazingatiwa katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa, namshukuru Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba pamoja na timu yake ya wataalam kwa kutupa nafasi ya kutusikiliza, kujadiliana, kushauriana kuhusu namna bora ya kutekeleza vipaumbele vya Sekta ya Kilimo na kuipa Sekta ya Kilimo kipaumbele katika Mpango wa Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ushetu, Shinyanga; Mheshimiwa Lekishon Shangai kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu limepata pigo la kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ushetu na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Elias Kwandikwa; aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji Mheshimiwa William Tate Ole Nasha; na aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa dada yangu Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama. Ninatoa pole kwa Wabunge, familia, ndugu, jamaa na marafiki kwa kuondokewa na wapendwa wetu. Mungu azilaze roho zao mahala pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee nawashukuru viongozi na watumishi wote wa Wizara ya Kilimo kwa ushirikiano wao na bidii yao katika kazi. Namshukuru sana Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Andrew Massawe na Naibu Katibu Mkuu Profesa Siza Donald Tumbo, Wakuu

wa Taasisi na Bodi zilizo chini ya Wizara ya Kilimo kwa kazi nzuri na ushirikiano mkubwa ambao wameendelea kuutoa.

Mheshimiwa Spika, mchango Sekta ya Kilimo katika Awamu zote sita: Serikali ya Awamu ya Kwanza ilitambua Tanzania kama nchi ya Wakulima na Wafanyakazi na kuwekeza katika kilimo hususan katika maeneo Vyuo vya Utafiti na Mafunzo, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Mashirika ya Umma yanayosimamia Kilimo, Bodi za Mazao na Vyama vya Ushirika. Pia ilihamasisha kilimo na lishe kupitia programu na kampeni mbalimbali ikiwemo Ukulima wa Kisasa, Kilimo cha Kufa na Kupona, Chakula ni Uhai, Mtu ni Afya, Elimu ya Kujitegemea na Siasa ni Kilimo.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika kipindi hicho, msisitizo uliwekwa katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara na kufikia kiwango cha kuongoza Kimataifa kwa baadhi ya mazao ikiwemo korosho na mkonge kama inavyoonekana katika kielelezo namba moja ukurasa namba 10.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Pili, ilifanya mageuzi ya uchumi yaliyokuwa kichocheo katika maendeleo ya kilimo ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa Sera ya Kilimo ya mwaka 1983. Aidha, Serikali ilipunguza vikwazo katika biashara ili kurahisisha upatikanaji wa bidhaa kwa ajili ya ustawi wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tatu, iliimarisha taasisi na kusimamia utawala bora, ilibinafsisha Mashirika ya Umma na mashamba ya Umma, iliboresha Bodi za Mazao kwa kuzifanya Bodi hizo kuachana na biashara na badala yake kuwa bodi za udhibiti na uendelezaji wa mazao. Pia kwa kipekee iliunda Wizara ya Masoko na Ushirika na kuimarisha ugatuaji wa madaraka kwa kuimarisha Serikali za Mitaa ambako huduma za ugani za Kilimo na Mifugo zilihamishiwa *TAMISEMI*.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha maendeleo ya Sekta ya Kilimo, Serikali ya Awamu ya Nne ilianzisha na kutekeleza Programu ya *ASDPI*, Programu ya Modenizesheni ya Ushirika, Kilimo Kwanza na *SAGCOT*. Pia, ilianzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo, Mpango wa Ruzuku ya Pembejeo za Kilimo na taasisi mbalimbali ikiwemo Wakala wa Mbegu, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika. Taasisi hizo zilianzishwa ili kuendeleza ufanisi na kutoa huduma kwa wakulima katika upatikanaji wa pembejeo, miundombinu ya wakulima na ushirika.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano, ilianzisha na kuendeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *ASDP II*. Pia, iliboresha na kuwekeza katika miundombinu ya barabara, bandari, nishati, na miundombinu ya wezeshi; na kuchochea uwekezaji katika sekta za uzalishaji. Serikali pia ilihamasisha ukuaji wa uchumi unaotegemea maendeleo ya viwanda vya kusindika na kuchakata mazao ya kilimo *(agro-processing)*.

Mheshimiwa Spika, ukizingatia utekelezaji wa awamu zote tano, Serikali za Awamu ya Kwanza na Awamu ya Nne ziliwekeza katika msingi mkuu wa uzalishaji. Serikali za Awamu ya Pili na ya Tatu zilifanya kazi kubwa ya kufungua biashara na kuweka mifumo ya kitaasisi. Serikali ya Awamu ya Tano ilifanya kazi kubwa ya kujenga miundombinu mbalimbali ambayo ni muhimu katika kuchochea uzalishaji, uongezaji wa thamani na usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imedhihirisha kwa vitendo utashi wa kisiasa kwa kutambua kuwa maendeleo ya uchumi yatatokana na sekta za uzalishaji hasa sekta ya kilimo. Azma hiyo itafikiwa kwa kuwekeza maeneo ya kimkakati ya utafiti, uzalishaji wa mbegu bora, uimarishaji wa huduma za ugani, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, uhifadhi wa mazao na uimarishaji wa upatikanaji masoko ya mazao ya kilimo. Aidha, Wizara inaendelea kutekeleza programu ya *ASDP - II* na kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kuwekeza na kufanya biashara katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mafanikio ya Awamu ya Sita, katika kipindi cha mwaka mmoja wa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali imeongeza bajeti ya utafiti wa kilimo kutoka Shilingi bilioni 7.3 hadi Shilingi bilioni 11.63, huduma za ugani kutoka Shilingi milioni 600 hadi Shilingi bilioni 11.5, umwagiliaji kutoka Shilingi bilioni 17.7 hadi Shilingi bilioni 51 na uzalishaji wa mbegu kutoka Shilingi bilioni 5.2 hadi Shilingi bilioni 10.8.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita imeongeza fedha za ununuzi wa nafaka kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi *NFRA* na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko *CPB* kutoka Shilingi bilioni 19 mwaka 2020/2021 hadi Shilingi bilioni 119 mwaka 2021/2022. Hadi Aprili, 2022 fedha hizo zimewezesha ununuaji wa tani 183,045,384 za mpunga, mahindi na mtama, ambazo zitauzwa katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha huduma za ugani katika kipindi hicho, Serikali imewezesha ununuzi wa pikipiki 7,000 kwa ajili ya maafisa ugani ili kurahisisha usafiri; vishikwambi *(Tablets*) 384 kwa maafisa ugani; visanduku vya *extension kits* 6,700 kwa maafisa ugani; na vifaa vya kupimia udongo *(soil scanner)* 143 kwa Halmashauri 143. Jumla ya Shilingi bilioni 9.29 zimetumika kununua vifaa hivyo.

Mheshimiwa Spika, eneo linalomwagiliwa limeongezeka kutoka hekta 695,045 mwaka 2021 hadi hekta 727,280.6 mwaka 2022, ambapo ni sawa na asilimia 60 ya lengo la kufikia hekta milioni 1.2 mwaka 2025 lililelekezwa katika Ilani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita imesimamia dhana ya kilimo ni biashara kwa kuimarisha mahusiano ya kimataifa ambayo yamefungua fursa ya masoko na mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi. Jitihada hizo zimewezesha kupatikana kwa fursa za masoko mapya ya mazao nje ya nchi ikiwemo soko la parachichi katika nchi za India na Afrika Kusini, ndizi nchi ya Kenya na mchele nchini ubelgiji, baada ya kukidhi vigezo vya ubora.

Mheshimiwa Spika, aidha, upatikanaji wa masoko umeongeza mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi ikiwemo mchele kutoka tani 184,524 zenye thamani ya shilingi bilioni 176 mwaka 2020 hadi tani 441,909 zenye thamani ya shilingi bilioni 476.8 mwaka 2021. Vilevile, mahindi kutoka tani 92,000 zenye thamani ya shilingi bilioni 58 mwaka 2020 hadi tani 189,277 zenye thamani ya shilingi bilioni 72 mwaka 2021, na parachichi kutoka tani 6,702 zenye thamani ya shilingi bilioni14 mwaka 2020 hadi tani 12,000 zenye thamani ya shilingi bilioni 24.9 mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho, Serikali imeongeza mtaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(TADB)* kutoka Shilingi bilioni 60 hadi Shilingi bilioni 268, sawa na ongezeko la asilimia 346. Kutokana ongezeko hilo *TADB* imeweza kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 116 kwenye miradi 197 ya maendeleo, na kufanya jumla ya mikopo iliyotolewa tangu kuanzishwa kwake kufika shilingi bilioni 482.4. Aidha, benki hiyo imewezesha wakulima milioni 1.5 kupata dhamana ya mikopo ya kiasi cha shilingi bilioni 144.

Mheshimiwa Spika, Serikali imewezesha kupunguza riba za mikopo ya kilimo katika benki za kibiashara kutoka kati ya asilimia 17 na 20 hadi kufikia asilimia tisa. Punguzo hilo limewezesha wakulima kununua pembejeo kwa ajili ya uzalishaji pamona na kuanzisha na kufufua viwanda vidogo ili kuongeza thamani ya mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imetoa ruzuku za pembejeo za kilimo kwa mazao ya korosho, tumbaku na pamba zenye thamani ya Shilingi bilioni 178.8. Kadhalika, katika kipindi hicho Serikali imewezesha uundaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika, ununuzi wa magari 15 kupitia Vyama vya Ushirika, pikipiki 137 na kompyuta 82 kwa ajili ya kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa vyama vya ushirika nchini. Jumla ya Shilingi bilioni 2.44 zimetumika kuunda mfumo na kununua vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine na matokeo ya ziara ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika nchi mbalimbali ni kama ifuatavyo: -

Nchini Ufaransa – Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania imesaini mkataba wa mkopo wa masharti nafuu wenye thamani ya Euro milioni 80,

sawa na Shilingi bilioni 210, wenye lengo la kuimarisha benki hiyo ili kutoa mikopo ya muda mfupi na mrefu kwa sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na uwekezaji mkubwa katika sekta ya mbolea, kwa sasa Kiwanda cha *Itracom Fertilizer Limited* kutoka Burundi kinajenga kiwanda kikubwa cha mbolea katika Jiji la Dodoma chenye thamani ya Dola Milioni 180 na kinatarajiwa kutoa ajira za kudumu kwa wafanyakazi 3,000 na kitakuwa na uwezo wa kuzalisha mbolea tani 600,000 kwa mwaka. Vilevile, upanuzi wa kiwanda cha Minjingu kutoka tani 100,000 kwenda tani 500,000 za mbolea kwa uwekezaji wa Dola milioni 20.

Mheshimiwa Spika, mbali na jitihada hizo, pia jitihada kubwa za kufungua masoko kwaajili ya mazao ya kilimo ambapo hapo awali ilikuwa ni moja ya changamoto kubwa inayotukumba, hivyo tunapenda kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kutokana na juhudi zake za kuimarisha mahusiano na mataifa wanachama wa *EAC* na mataifa mengine. Jambo hili limechochea Uondoaji wa vikwazo 56 vya biashara kati ya 64 vilivyokuwepo kati ya nchi ya Tanzania na Kenya; hii ikiwa ni mafanikio ya utekelezaji wa makubaliano kati ya viongozi wa nchi hizo mbili. Jitihada hizo zimewezesha ukuaji wa biashara kati ya Tanzania na Kenya kufikia Dola milioni 905.

Mheshimiwa Spika, kuna upatikanaji wa soko la China kwa ajili ya mazao maharage ya soya. Jambo hili limetoa fursa ya soko la uhakika kwa wakulima wa mazao hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upatikanaji wa chakula. Mahitaji ya chakula kwa mwaka 2021/2022 yamefikia tani milioni 14.83 ambapo tani 9.4 ni mazao ya nafaka na tani 5.8 ni mazao yasiyo ya nafaka. Mahitaji hayo ukilinganisha na upatikanaji wa tani milioni 18 kwa mwaka Taifa limejitosheleza kwa chakula kwa asilimia 126.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utekelezaji wa malengo ya mpango wa mwaka 2021/2022 katika mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara imetekeleza vipaumbele vifuatavyo: -

Eneo la utafiti wa kilimo, upatikanaji wa pembejeo, kuimarisha kilimo cha umwagiliaji, huduma na mafunzo ya ugani, upatikanaji wa masoko, kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa mitaji, na kuimarisha kilimo anga.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Wizara ilikadiria kukusanya mapato ya Shilingi bilioni 34 kupitia Fungu 43 na Fungu 05. Hadi Aprili, 2022, Wizara imekusanya Shilingi bilioni 4.8 sawa na asilimia 14 ya makadirio. Serikali inaendelea kuboresha na kuimarisha na kutoa elimu ili kuongeza makusanyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 294. Kati ya fedha hizo bilioni 81.9 ni za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 211 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2022, shilingi 54,083,072,288 sawa na asilimia 84.34 ya fedha zilizoidhinishwa za matumizi ya kawaida zimetolewa. Kati ya fedha hizo, shilingi 17,455,234,748 ni za matumizi mengineyo ya Wizara, Taasisi na Bodi na shilingi 36,627,837,540 ni mishahara ya Wizara, Taasisi na Bodi. 334.1.6. matumizi ya bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili, 2022 shilingi 68.66 sawa na asilimia 83 ya fedha za matumizi ya kawaida zimetolewa na kutumika. Aidha, shilingi bilioni 83 ya fedha za maendeleo sawa na asilimia 55 ya lengo la fedha za ndani zimetolewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuongeza upatikanaji wa mbegu bora nchini, *TARI* imezalisha mbegu mama tani 19.9 na mbegu za awali tani 197. Kati ya mbegu za awali zilizozalishwa tani 16 zilipelekwa *ASA* na tani 180 zimepelekwa katika sekta binafsi kwa ajili ya kuzalisha tani 5,933 za mbegu zilizothibitishwa. Vile vile *TARI* imezalisha mbegu za msingi tani 134 ambazo zimewezesha uzalishaji wa tani 26 za mbegu zilizothibitishwa na mazao ya alizeti, maharage, mahindi, ngano, mtama, mpunga, alizeti, ufuta, karanga na pamba.

Mheshimiwa Spika, *TARI* imefanya utafiti kuhusu nafasi mpya ya kupanda pamba ambayo ni sentimita 60 kutoka mstari hadi mstari na sentimita 30 kutoka mche hadi mche badala ya nafasi za awali ambazo zlikuwa ni sentimita 90 kwa 40. Nafasi hiyo mpya itaongeza mavuno kutoka wastani wa kilo 710 hadi kilo kufikia kilo1,422 kwa hekta. Aidha, *TARI* Ukiliguru wamebuni mashine ya kupandia pamba *fabricated* yenye uwezo wa kupanda ekari moja kwa saa moja hadi masaa matatu badala ya masaa 11 kwa jembe la mkono.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii, kwa niaba ya Wizara kuwapongeza watafiti waliogundua mfumo huu ambao ni Dauson Malela, Robert Cheleo Alphonce na Dkt. Paul Saidia ambao ni watafiti wa *TARI* - Ukiriguru kwa ubunifu wao wa kugundua na kutengeneza mashine hiyo rahisi ya kupandia.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili 2022, upatikanaji wa mbegu bora ulifikia tani 49.962 sawa na asilimia 26 za mahitaji ya tani 187,000 kwa mwaka. Kati ya mbegu hizo, tani 35,199 zimezalishwa ndani ya nchi, tani 11,340 zimeingizwa kutoka nje ya nchi na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, Wizara imesambaza kwa wakulima tani 2,000 za mbegu za alizeti zenye thamani ya shilingi bilioni 5.84 kwa utaratibu wa

ruzuku. Mbegu hizo zimesambazwa katika Mikoa ya Dodoma, Singida, Simiyu, Manyara na zinatarajiwa kuzalisha tani 400,000 za alizeti zitakazotuzalishia mafuta ya kula wastani wa tani 100,000. Aidha, *TARI* imezalisha tani 37 za mbegu za ufuta na kusambaza tani 25 kwa wakulima na tani 18 za mbegu za karanga na kusambaza tani 15 kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia *ASA*, *TARI*, Bodi za Chai, Pamba, Mkonge, Korosho, Pareto, Kahawa na vikundi vya wakulima vimezalisha miche bora milioni 32 na mbegu tani 95,000 na kusambaza miche milioni 24 na mbegu tani 95,000 kwa wakulima. Aidha, Bodi ya Pamba Tanzania imesambaza tani 15,548 za mbegu za pamba kwa wakulima zinazotosha kupandwa katika hekta 621,920.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu uzalishaji na uingizwaji wa mbolea nchini, ambapo hadi Aprili, 22 tani 436,452 za mbolea zimepatikana, sawa na asilimia 63 ya mahitaji ya tani 698,260. Kati ya hizo tani 274,000 zimeingizwa kutoka nje ya nchi na tani 43,000 zimezalishwa nchini; na tani 117,900 ni bakaa ya msimu wa 2020/2021. Hadi kufikia Aprili, Bodi ya Tumbaku Tanzania kwa kushirikiana na vyama vya ushirika imesambaza mbolea ya *NPK* tani 20,000 na *CAN* tani 5,066 kwa wakulima ili kuongeza uzalishaji na tija.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2021/2022 upatikanaji wa viuatilifu vya udhibiti wa mlipuko ya usumbufu wa mimea ambapo umefikia lita 106,000 zenye thamani ya shilingi bilioni 3.11. Hadi Aprili, 22 jumla ya lita 34,817 za viuatilifu zimesambazwa kwa kudhibiti nzi wa matunda na viwavijeshi.

Mheshimiwa Spika, pia Wizara imewezesha maabara ya *TPHPA* ama *TAPHA* kupata ithibati kwaajili ya kusaidia mazao ya kilimo yatakayopimwa katika maabara hiyo ili kukidhi viwango vya masoko ya kimataifa. Aidha, Wizara kupitia Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu imeendelea na ujenzi wa Kituo cha Udhibiti wa Visumbufu Kibaiolojia ambao hadi sasa umefikia asilimia 65 na utagharimu jumla ya Shilingi bilioni 3.92 hadi kukamilika kwake.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha matumizi ya zana bora za kilimo, Wizara imeingia mkataba wa kuhudumia vituo jumuishi vya huduma za zana za kilimo *(mechanization hubs)* na kampuni ya *AFTRADE*. Tathmini ya maeneo yanayofaa kuanzisha vituo hivyo imebaini vituo 13 vimekidhi vigezo na taratibu za kuiwezesha kuanza na kazi zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, Wizara imewezesha uanzishwaji wa mashamba darasa 695. Kati ya hayo 378 ni ya alizeti na pamba ni 317. Vilevile, imeanzisha mashamba ya mfano 672. Kati ya hayo alizeti ni 415 na pamba ni 257 katika mikoa ya Dodoma, Singida na Simiyu. Pia, maafisa ugani wa maeneo hayo wamepatiwa tani 10 za mbolea, viuatilifu 1,617 na viuagugu 1,584. Serikali imechukua hatua hii ili kurahisisha utoaji wa mafunzo ya kilimo bora cha alizeti na pamba kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2021/2022 Wizara imeendelea kukarabati miundombinu katika vyuo 12 vya mafunzo ya kilimo nchini ambapo ukarabati wa miundombinu iliyopangwa katika vituo sita umefikia wastani wa asilimia 95 na vyuo sita umefikia asilimia 40. Aidha, mafanikio mengine katika kuimarisha huduma za ugani ni kama nilivyoeleza kwenye mafanikio ya mwaka mmoja wa Serikali ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea na ujenzi wa skimu sita zenye ukubwa wa jumla hekta 9,349 katika Mikoa ya Dodoma, Kilimanjaro, Tabora, Mbeya na Manyara; ambapo shilingi bilioni 12.06 zitatumika hadi kukamilika. Aidha, ukarabati wa skimu nane zenye hekta 3,711 katika mikoa ya Tanga, Dodoma, Iringa, Katavi unaendelea; ambapo jumla ya shilingi milioni 917 zitatumika hadi kukamilika. Aidha, taratibu za manunuzi zinaendelea kwa jumla ya ujenzi wa skimu nane zenye jumla ya hekta 5,930 zilizopo katika Mikoa ya Katavi, Ruvuma, Morogoro, Iringa, Simiyu, Mbeya na Tabora. Jumla ya shilingi bilioni 3.7 zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa skimu hizo hadi kukamilika.

Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika katika skimu nne na unaendelea katika skimu 23 zilizoko Mikoa ya Iringa, Tabora, Kigoma, Rukwa, Mbeya, Dodoma, Mtwara Manyara Singida, Geita na Mwanza. Ujenzi wa skimu hizo utafanyika katika mwaka wa fedha 2022/2023; ambapo jumla ya Shilingi bilioni 1.48 zitatumika kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

Mheshimiwa Spika, katika kufungua masoko mapya ya mazao, Wizara imeshiriki katika Maonesho ya *Expo*, 2020 yaliyofanyika Dubai - Umoja wa Falme za Kiarabu. Mafanikio yaliyopatikana ni kusainiwa kwa hati saba za makubaliano kwa ajili ya kushirikiana katika kuendeleza sekta ya kilimo. Mashirikiano hayo yamejikita katika ujenzi wa vituo vya kuchanganyia mbolea na *pesticide*, upatikanaji na matumizi bora ya zana za kilimo, miundombinu ya umwagiliaji, uhifadhi na usafirishaji wa mazao. Mafanikio mengine ni ushirikiano katika kupoka na kuhodhi masoko ya mazao ya kilimo ambapo tarehe 03 Mei, 2022 shehena ya kontena lenye tani 22 za parachichi aina ya *HASS* lilipokelewa Mumbai India ikiwa ni matokeo ya mkataba uliosaniwa kati ya Tanzania *Horticulture Association* na India.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 tani 6,794 za singa zenye thamani ya shilingi bilioni 21 na bidhaa mbalimbali za mkonge tani 711 zenye thamani ya shilingi bilioni 2.1 zimeuzwa katika soko la ndani. Aidha, tani 20,000 za singa zenye thamani ya dola za Marekani 33.77 na tani 866 za bidhaa mbalimbali za mkonge zimeuzwa kwenye soko la nje. Vile vile, tani 73 za kahawa zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 142.26 zimeuzwa kwenye soko la nje. Kadhalika, tani 53,594 za soya zimeuzwa katika nchi za India, China, Rwanda na Kenya ikilinganishwa na tani 2,647 zilizouzwa

msimu wa 2019/2020. Pia tani 231,000 za korosho ghafi; tani 144,000 za pamba; tani 60,819 za kahawa; na tani 6,875 za kakao zimeuzwa kwenye soko la nje.

Mheshimiwa Spika, Ushiriki wa Sekta Binafsi; Wizara imeendelea kuthamini mchango wa Sekta Binafsi katika kuchochea na ukuaji wa Sekta ya Kilimo, usalama wa chakula, uongezaji wa thamani, kuimarisha upatikanaji wa pembejeo, kuongeza ajira na uhakika wa masoko ya mazao ya kilimo. Taarifa ya utekelezaji wa *ASDP II* kupitia Sekta Binafsi inaonesha kuwa Kampuni 606 za Sekta Binafsi, Asasi za kiraia 47 na Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali 64 yamewekeza katika kilimo. Aidha, Wizara imeratibu majukwaa 52 ya majadiliano na Sekta Binafsi kwa mazao ya asilia ya biashara, nafaka, mikunde, bustani na mbegu, mafuta ya kula kwa ajili ya kutatua changamoto za kikodi na kisera.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha mahusiano ya Kimataifa kupitia wabia wa maendeleo ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kukuza uchumi kutokana na uwekezaji katika Sekta ya Kilimo. Hadi kufikia Juni, 2021 jumla ya Shilingi Bilioni 30.7 zimetumiwa na wabia wa maendeleo katika utekelezaji wa miradi 199 ya sekta ya kilimo. Maeneo yaliyozingatiwa ni pamoja na masuala ya vijana katika kilimo, masoko, mbegu, afya ya mimea, utafiti na uhifadhi wa mazao. Taasisi za Fedha zimeendelea kuwa muhimu katika upatikanaji wa mitaji kwenye sekta ya kilimo. Taarifa ya utekelezaji hadi kufikia Juni, 2021 inaonesha kuwa taasisi za fedha ikiwemo benki ya *CRDB, NMB, TADB* na *TIB* zilitoa mikopo ya Shilingi Trilioni 1.26 katika kuendeleza sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara kwa kushirikiana na Sekta Binafsi iliunda Kamati ya Viongozi kushughulikia mifumo ya ugharamiaji ya Sekta ya Kilimo ikiwemo kupunguza riba kwa wakulima kupata mikopo. Mfano, *TADB* imetoa jumla ya mikopo yenye thamani ya Shilingi Bilioni 116 kwa ajili ya pembejeo za kilimo kwa mazao ya kahawa na kufufua Vinu vya Kuchambua Pamba vya Kahama, Chato, Mbogwe, Bukombe, Manawa, Sola na Kiwanda cha Mafuta cha Chikichi cha *Trolle Meesle* Tanzania *Limited* kilichopo Mkoani Kigoma. Vile vile, *TADB* kupitia Mfuko wake wa Dhamana wa Wakulima Wadogo imetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi Bilioni 144 kwa wakulima 887 pamoja na wadau wengine wa kilimo hususan *AMCOS* na wajasiriamali wadogo.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo inahusika na uzalishaji wa mazao zaidi ya 90 katika kanda saba (7) za kilimo. Mazao hayo yanajumuisha mazao ya asilia ya biashara, mazao ya mafuta, mazao ya chakula na mazao ya bustani. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, uzalishaji wa mazao ya asilia ya biashara ya tumbaku, pamba, kahawa, chai, sukari na mkonge umeongezeka kutoka tani 898,966 hadi tani 938,586 na uzalishaji bado unaendelea kwa mazao ya chai, pareto na mkonge. Aidha, uzalishaji wa mazao ya chakula unaojumuisha mahindi, mazao ya nafaka na yasiyokuwa

nafaka umeongezeka kutoka tani milioni 18 mwaka 2020 hadi milioni 18.66 mwaka 2021, sawa na ongezeko la asilimia 2.0.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mazao ya bustani uzalishaji umefikia wastani wa tani milioni 7.3 ikilinganishwa na tani milioni 7.5 kwa mwaka 2021, sawa na upungufu wa asilimia 3.0. Upungufu huu umesababishwa na athari za ugonjwa wa virusi vya *Corona* uliopelekea usafirishaji wa mazao hayo nje ya nchi kuathirika.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutekeleza malengo ya Serikali ya kuondoa utegemezi wa mazao ya bidhaa za kilimo zenye uhitaji mkubwa ambazo huagizwa nje ya nchi kama vile mafuta ya kula, ngano na sukari. Wizara imesambaza kwa wakulima tani 2,000 za mbegu za alizeti kwa ruzuku ya shilingi bilioni 5.8, mbegu hizo zimesambazwa katika Mikoa ya Dodoma, Simiyu na Manyara. Aidha, mbegu hizo zitatoa mavuno ya mbegu za alizeti 400,000 na kutuingizia tani 100,000 za uzalishaji wa mafuta katika mfumo wetu wa uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, uzalishaji wetu wa ngano ulifikia tani 70,000 ukilinganishwa na mahitaji ya tani milioni moja za ngano kwa mwaka. Uzalishaji mdogo wa ngano unatokana na tija ndogo, uhaba wa mbegu bora zenye uwezo wa kukidhi mahitaji ya soko na mabadiliko ya tabia nchi. Ili kukabiliana na changamoto hizo Wizara imetenga Shilingi Milioni 750 kwa ajili ya utafiti.

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza uwezo wa uhifadhi wa mazao nchini, Wizara imekarabati maghala tisa, yenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 3,000 katika Mkoa wa Ruvuma ambapo ukarabati umefika asilimia 62. Wizara kupitia *CPB* imekamilisha ukarabati wa ghala la Kiteto na vihenge Mkoani Arusha ambapo jumla ya Shilingi Milioni 700 zimetumika kukamilisha ukarabati huo. Kupitia Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Uhifadhi unaotekelezwa na *NFRA,* Wizara imeendelea na ujenzi wa vihenge ambapo umefikia asilimia 90 na ujenzi wa ghala na miundombinu mingine, ambapo umefikia asilimia 66 na Dola za Kimarekani milioni 55 zitatumika katika kukamilisha mradi huo. Ukikamilika uwezo wetu wa kuhifadhi utakuwa tani 250,000.

Mheshimiwa Spika, aidha, ujenzi wa maghala 14 kupitia mradi wa *TANPAC* umefikia wastani wa asilimia 60. Ghala hizo zitahifadhi tani 21,000 na jumla ya shilingi bilioni 14 zimetumika.

Mheshimiwa Spika, uongezaji wa maendeleo ya Ushirika; Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeratibu uuzaji wa tani 597,000 za mazao zenye thamani ya shilingi trilioni 1.5 kupitia Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara kupitia Tume imeratibu uanzishwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika, ambayo itamilikiwa

na Vyama vya Ushirika kwa asilimia 51 na Taasisi za Watu Binafsi kwa asilimia 49. Lengo la kuanzisha Benki hiyo ni kurahisisha upatikanaji wa mitaji kwa wakulima na maelezo ya kina yanapatikana katika ukurasa wa 138. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; Wizara ya Kilimo inawasilisha bajeti mbele yako wakati dunia inaendelea kupitia changamoto kubwa mbili; vita kati ya Ukraine na Urusi pamoja na athari za UVIKO. Changamoto hizo zimeleta mabadiliko ya mifumo ya ugavi duniani na gharama za usafirishaji za bidhaa na huduma Kimataifa katika uchumi wa dunia; na kwa kipekee mifumo ya uzalishaji na usambazaji wa mbolea duniani na ya biashara ya mazao.

Mheshimiwa Spika, kufuatia hali hiyo bei ya mbolea imepanda kwa wastani wa zaidi ya asilimia 100. Mfano, *DAP* imepanda kwa dola za Kimarekani kutoka 396 kwa mwaka 2019 hadi dola 948 kwa mwaka 2022. *UREA* kutoka dola za Kimarekani 249 kwa tani hadi dola za Kimarekani 723 kwa tani. *CAN* imepanda kutoka dola za Kimarekani 210 kwa tani hadi dola 520 kwa tani na *SA* kutoka dola za Kimarekani 128 kwa tani hadi dola za Kimarekani 403 kwa tani.

Mheshimiwa Spika, bei ya mafuta ya kula katika soko la dunia imepanda kutoka dola za Kimarekani 1,631 Machi, 2021 hadi dola za Kimarekani 2,250 Machi, 2022, sawa na ongezeko la asilimia 38. Aidha, bei ya ngano imepanda kutoka dola za Kimarekani 178.24 kwa tani hadi kufika dola 294 sawa na ongezeko la asilimia 65. Hali hiyo imesababisha nchi kukabiliwa na mfumuko wa bei *imported inflation* kutokana na bidhaa zinazoingizwa kutoka nje ya nchi hali inayoathiri ustawi wa wananchi. Aidha, athari za UVIKO na mgogoro unaoendelea kati ya Ukraine na Urusi kutokana na tafiti mbalimbali za Kimataifa, utaathiri mfumo wa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa mbalimbali hadi kufikia mwaka, 2025.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo katika mwaka wa fedha 2022/2023, unalenga kujenga msingi imara wa muda mrefu wa ukuaji wa sekta ya kilimo kwa kiwango cha asilimia 10 ifikapo mwaka, 2030. Pamoja na kujenga msingi wa kukabiliana na athari za majanga ya kiuchumi ikiwemo UVIKO – 19 na vita ya Ukraine na Russia, kulinda sekta na kupunguza matumizi ya fedha za kigeni katika uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi. Wizara inachukua hatua hizo kwa kuzingatia kuwa sekta ya kilimo ni mwajiri mkuu wa nguvu kazi ya Taifa na mchangiaji mkuu wa pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa kiwango cha ukuaji wa sekta ya kilimo kwa asilimia 10 ifikapo mwaka, 2030 kitachangia katika kupunguza umaskini kwa asilimia 50. Azma hiyo itaongozwa na Dira ya Maendeleo ya mwaka 2025, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa mwaka 2025/2026, Sera ya Taifa ya Kilimo ya mwaka 2013, Mwongozo wa Bajeti wa mwaka 2022/2023, Ilani ya Uchaguzi wa Mwaka 2020/2025 na Hotuba ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ya mwaka 2021 aliyoitoa katika Bunge lako Tukufu. Aidha, Mpango

umezingatia maendeleo endelevu *SDG's Goals* za mwaka, 2030. Masuala Mtambuka ya jinsia, mazingira, lishe, mabadiliko ya tabia nchi na athari za VVU na UKIMWI. Ili kufikia ukuaji wa sekta ya kilimo asilimia 10 ifikapo mwaka 2030. Bajeti ya mwaka 2023 ni msingi muhimu kufikia lengo kuu hilo. Aidha, ili kufikia lengo hilo Wizara imejiwekea malengo yafuatayo:-

(i) Kujitosheleza kwa mahitaji ya chakula ndani ya nchi na kuuza nje ya nchi;

(ii) Kufanya mwelekeo wa uzalishaji wa mazao ya chakula kuwa biashara;

(iii) Thamani ya mauzo ya nje kuongezeka kutoka dola milioni 1.2 hadi kufikia Dola bilioni 5.0 ifikapo mwaka 2030;

(iv) Kuongeza idadi ya mashamba makubwa kwa maana ya *Commercial Farms* na *Block Farms* kutoka 110 hadi kufikia mashamba 10,000 ifikapo mwaka 2030;

(v) Kuongeza eneo la umwagiliaji kufika hekta milioni 8.5 sawa na asilimia 50 ya eneo lote linalolimwa ifikapo mwaka 2030, ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo kupitia kilimo cha umwagiliaji kutoka asilimia 10 ya sasa hadi asilimia 50;

(vi) Kutengeneza ajira za vijana na wanawake katika sekta ya kilimo kufikia milioni tatu ifikapo mwaka, 2025;

(vii) Kuhakikisha upatikanaji wa malighafi kwenye viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo za bidhaa kufikia asilimia 100 kutoka asilimia 60 ya sasa;

(viii) Kuongeza upatikanaji wa mikopo kutoka kwenye sekta ya fedha kutoka asilimia tisa ya mwaka, 2022 hadi kufika asilimia 30 ifikapo mwaka, 2030;

(ix) Kupunguza upotevu wa mazao ya kilimo tunayovuna kutoka asilimia 35 ya sasa hadi asilimia 5.0 ifikapo mwaka, 2030;

(x) Kuondoa upungufu wa mafuta ya kula na kulifanya zao la alizeti kuwa moja ya mazao yatakayozalishwa kutosheleza mahitaji ya ndani na mauzo nje ya nchi;

(xi) Kuwekeza katika mashamba makubwa ya chikichi na kuondoa mfumo wa kilimo cha chikichi kwa mashamba madogo ya heka moja ambao tunautumia sasa;

(xii) Kuongeza mauzo ya mazao ya *horticulture* kutoka Dola milioni 750 mwaka, 2020 hadi kufika Dola bilioni 2.0 mwaka, 2030;

(xiii) Kujitosheleza kwa uzalishaji wa mbolea ndani ya nchi na kuvipa vipaumbele viwanda vya ndani vya mbolea na matumizi ya chokaa ili kupunguza gharama za uzalishaji; na

(xiv) Kujitosheleza kwa mahitaji ya mbegu bora na kuuza mbegu nje ya nchi kupitia ushirikishaji wa sekta binafsi.

Matokeo yanayotarajiwa kutokana na utekelezaji wa malengo hayo sio ya muda mfupi, bali yanajenga msingi wa kuwa na matokeo yatakayohakikishia mwendelezo wa ukuaji wa sekta ya kilimo kwa muda mrefu. Ukuaji wa Pato la Taifa, ajira, mapato ya fedha za kigeni, malighafi za viwanda na kujihakikishia usalama wa chakula na kuuza ziada nje. Takwimu zinaonesha kuwa ifikapo mwaka, 2050 idadi ya watu duniani itafika bilioni 9.7 na bilioni 8.5 ifikapo mwaka 2030. Afrika itafikia bilioni 2.4 mwaka 2050 na bilioni 1.6 mwaka 2030. vile vile ifikapo mwaka, 2050 Tanzania itakuwa na idadi ya watu milioni 135 na mwaka 2030 watu milioni 79 ambapo mahitaji ya chakula nchini yatafika tani milioni 18.8, wakati huo huo mahitaji ya chakula duniani yataongezeka kwa wastani wa asilimia 50.

Mheshimiwa Spika, athari za mazingira zitashusha uzalishaji wa mashambani kwa asilimia 4.0 hii ni fursa kwa atakayejiandaa na ni majanga kwa ambaye hatajiandaa na hivyo, matumizi ya teknolojia na uwekezaji kwenye teknolojia ndio muarobaini pekee utakaotatua hatari hii. Aidha, biashara ya chakula katika Soko la Afrika itafikia Dola trilioni 1.0 ifikapo mwaka 2030. Hii itafungua fursa za ajira, kwenye mnyororo wa thamani kutokana na ongezeko hilo la idadi ya watu duniani. Kama Taifa lazima tujiandae sasa ili kufaidika na fursa hiyo ya kibiashara na kujihakikishia usalama wa chakula, ukuaji na uendelevu wa uchumi wetu na kulifanya Taifa letu kuwa huru.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara imepanga vipaumbele mahususi vifuatavyo:-

(i) Kuimarisha utafiti;

(ii) Kutoa ruzuku ya mbegu za alizeti, ngano na miche ya chikichi;

(iii) Kuimarisha upatikanaji wa pembejeo;

(iv) Kuimarisha na kutoa huduma za upimaji wa afya ya udongo ili kuwezesha wakulima kutambua aina ya kiwango cha mbolea kinachohitajika;

(v) Kuendeleza kilimo cha umwagiliaji kwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji;

(vi) Kuimarisha huduma za ugani na kuhamasisha kilimo cha ukanda na ikolojia za kilimo;

(vii) Kuanzisha Tanzania *Agricultural Growth Corridor;*

(viii) Kuimarisha upatikanaji wa mazao ya kilimo;

(ix) Kuimarisha mfumo wa upatikanaji wa mitaji;

(x) Kuimarisha miundombinu ya uhifadhi wa mazao ya kilimo ikiwa pamoja na ujenzi wa maghala katika ngazi ya vijiji, kata na tarafa ili kupunguza upotevu wa mazao;

(xi) Kuhamasisha kilimo cha mashamba makubwa ikiwa ni pamoja na kuanzisha maeneo maalum ya mashamba makubwa;

(xii) Kuanza kutoa ruzuku ya mbolea kwenye mwaka wa fedha 2022/2023; na

(xiii) Kuimarisha kilimo anga na kuimarisha maendeleo ya ushirika.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la kuimarisha utafiti mahitaji yetu kama nchi ya mbegu bora ni tani 652,250 na sasa tunazalisha tani 35,199. Ili kuondoa tatizo hili, Wizara imeongeza bajeti ya utafiti na uzalishaji wa mbegu za msingi kutoka Shilingi Bilioni 11.6 ya mwaka 2021/2022 mpaka kwenda Shilingi Bilioni 40.73 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 sawa na ongezeko la asilimia 250. Hatua hiyo itawezesha upatikanaji wa mbegu za awali na za msingi kutoka tani 226 kwenda tani 1,453 ambazo zitakazokidhi mahitaji ya uzalishaji wa mbegu bora, tani 452,650 zitakazosambazwa kwa wakulima na kufanya kufikia lengo kwa asilimia 69.4 ifikapo mwaka, 2025.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya bajeti ya utafiti ya mwaka 2022/2023 itatumika kuanza safari ya kama Taifa kulinda, kusafisha na kuzalisha mbegu zetu za asili kupitia Taasisi yetu ya *ASA;* na ifikapo mwaka, 2025 mbegu zetu za asili zitapatikana madukani kama ambavyo mbegu zilizoboreshwa zinavyouzwa madukani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara imedhamiria kuhakikisha inajitosheleza kwa mahitaji ya mbegu bora hususani kwa mazao ya mahindi, alizeti, soya, ufuta, ngano, maharage, kunde, mpunga, mtama, choroko na jumla ya Shilingi

Bilioni 43.03 zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha Taasisi yetu ya *ASA* kuzalisha mbegu tani 122,000 za mbegu bora kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto ya athari za kupanda kwa bei ya mbolea duniani ambapo hali hiyo inatazamiwa kuendelea hadi kufika mwaka 2023/2024; na katika kulinda uzalishaji wetu na kuwalinda wakulima wa Tanzania Wizara inatarajia kutumia Shilingi Bilioni 150 kutoa ruzuku ya mbolea kwa mazao yote kwa utaratibu utakaoelezwa wakati wa kuwasilishwa bajeti kuu ya Serikali. Ruzuku hiyo haitakuwa ya kudumu bali itatolewa katika kipindi maalum kulingana na mahitaji ya nyakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, utaratibu wa ruzuku kwa wakulima kupitia mfumo wa mazao kujigharamia *(Crop Financing)* utaendelea kutekelezwa. Ni heri Wizara ya Kilimo isifanye jambo lolote kwa mwaka wa fedha 2022/2023 bali wakulima Watanzania wapate ruzuku ya mbolea itakayofanya wazalishe, wailinde nchi yetu, walinde ukuaji wa uchumi, walinde mapato ya nje na kulilinda pato letu la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, naagiza Kampuni na Viwanda vyote vya mbolea nchini kusajiliwa na wakala wa *TFRA* ifikapo tarehe 31 Mei, 2022 ili kurahisisha utoaji na usimamizi wa ruzuku. Katika kuimarisha usimamizi wa utoaji wa ruzuku mifuko ya mbolea itawekwa *Barcodes* na *label* ya ruzuku ili kutofautisha na mbolea zitakazoendelea kuuzwa sokoni bila ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kampuni yoyote ambayo haitatekeleza agizo hili na kukubali kutumia mfumo utakaowekwa na *TFRA* wa kusimamia na kusajili kampuni, mawakala na kuweka mfumo wa *Point of Sale (POS)* kwenye maduka na ghala zao za Mikoani na Wilayani, Serikali haitosita kumfutia leseni yake ya biashara. Mpango huu wa ruzuku ya mbolea utawapa kipaumbele wazalishaji wa mbolea ndani ya nchi ili kulinda viwanda vyetu, ajira na usalama wa chakula.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kuwalinda na kuwawezesha wawekezaji katika viwanda vya ndani vya kuzalisha mbolea ikiwemo kiwanda cha *ITRACOM* chenye uwezo wa kuzalisha tani 600,000 za mbolea. Vilevile kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi nyingine na Serikali itawezesha upatikanaji wa vivutio vya uwekezaji kwa kiwanda cha mbolea Minjingu, ili kuweza kuongeza uwezo wake wa kuzalisha kutoka tani 100,000 za sasa.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea na mazungumzo na Wizara ya Nishati kuhusu kufufua mradi wa kuzalisha mbolea ya *urea* kwa kutumia gesi asilia. Vilevile Wizara itaiwezesha kampuni ya *TFC* ya Serikali Shilingi Bilioni Sita kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake kama mtaji ili kuweza kujiendesha kibiashara na kutumika kama chombo cha Serikali cha kuimarisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo, hususan mbolea na viuatilifu.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kuwahakikishia wazalishaji wadogo wa mbolea hai *(organic)* na chokaa kuwa, itaendelea kuwalea, kuwalinda na kuwahakikishia masoko ili kupunguza gharama za kuagiza mbolea za aina hiyo kutoka nje ya nchi. Kupitia Bunge lako Tukufu tunawahamasisha vijana wabunifu ambao wanaweza kuzalisha mbolea za kilimo hai *(organic)* waje Wizara ya Kilimo ili waweze kusaidiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara itakamilisha utaratibu wa kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo, mfuko huo utatumika kutoa ruzuku za pembejeo, kuwezesha uhimilivu wa bei za mazao*(stabilization fund)* kutokana na athari za majanga, mdororo wa uchumi na gharama za uwekezaji katika miundombinu ya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, Uongezaji wa Thamani na Uhifadhi wa Mazao ya Kilimo. Katika eneo la umwagiliaji katika mwaka wa fedha wa fedha wa 2022/2023 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imepanga kujenga mabwawa 14 yenye uwezo wa mita za ujazo Milioni 131.5 na kujenga skimu mpya 25 zenye jumla ya hekta elfu 53.234 katika Mikoa 14. Vilevile Tume itaboresha, itakarabati na kukamilisha skimu 30 zenye jumla ya hekta 41,771 katika Mikoa 10. Katika kutekeleza mpango huo jumla ya Shilingi Bilioni 256.2 zitatumika. Mpango huu utaongeza eneo la umwagiliaji kwa hekta 95,000 kutoka hekta 727,280 za mwaka 2021 hadi kufikia hekta 822,285 sawa na asilimia 68 ya lengo la Ilani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, ongezeko hilo litaongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo kama mpunga kwa tani 403,000 zenye thamani ya Bilioni 345 na vitunguu tani 374,000 zenye thamani ya Shilingi Bilioni 2.9 na hivyo kuongeza Pato la Taifa. Uwekezaji huu unakadiriwa kutoa ajira za moja kwa moja zipatazo 475,000.

Mheshimiwa Spika, Tume pia itafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika skimu 44 zenye ukubwa wa hekta 91,000 katika Mikoa ya Katavi, Iringa, Mbeya, Rukwa, Songwe, Dodoma, Kagera, Mwanza, pwani, Kigoma, Tabora, Geita, Singida, Arusha, Morogoro, Manyara, Njombe na Mtwara zitakazojengwa katika mwaka wa fedha wa 2023/2024. Vilevile itafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa mabonde ya kimkakati 13, jumla ya hekta 272,617 ambazo ni Bonde la Mto Kilombero hekta 53,00, Ifakara hekta 4,000, Ruvuma hekta 26,000, Ruhuhu hekta 3,700, Rufiji hekta 64,000, Ziwa Viktoria hekta 20,000, Mto Suguti hekta 4,800, Makondeko hekta 9,000, Mto Lukuledi hekta 4,680, Malagarasi hekta 7,000, Kasinde hekta 15,000, Songwe hekta 3,000 na skimu nane za kimkakati zenye jumla ya hekta 30,000 za Bugwema - Musoma, Mtambo - Hai, skimu za Mto Umba - Lushoto, skimu za Mkomazi - Korogwe, skimu ya Bonde la Kiru - Babati, skimu za Ngomai - Kibaigwa, Skimu ya Gereza la Kalankulukulu - Tanganyika na Lutambandosya - Mbinga. Ujenzi wa skimu na mabonde ya kimkakati utafanyika katika mwaka wa fedha 2022/2023 na 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, pia Tume itanunua mitamba mitambo 12 kwa ajili ya ujenzi wa skimu. Itanunua vifaa vya upimaji *land survey,* itanunua magari 38 kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa miradi kupitia ofisi za umwagiliaji za Mikoa na itajenga ofisi 17 za umwagiliaji za Mikoa. Jumla ya Shilingi Bilioni 59.6 zitatumika katika kutekeleza mpango huo.

Mheshimiwa Spika, Wizara itafungua ofisi 146 za Tume ya Umwagiliaji kwenye Wilaya ambazo zitakuwa na Wahandisi wa umwagiliaji, Mafundi Sanifu Ujenzi na Maafisa Kilimo. Watumishi hao kwa kushirikiana na watumishi waliopo Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, watasimamia miradi ya umwagiliaji katika Wilaya zao na kusimamia ukusanyaji wa ada za huduma za umwagiliaji. Aidha, watumishi hao watakuwa chini ya Ofisi za Tume ya Umwagiliaji na kuwajibika moja kwa moja Wizara ya Kilimo. Mfumo huo wa usimamizi wa miradi ya umwagiliaji utawezesha kuokoa upotevu wa Shilingi 100,000,000,000 kwa mwaka kutoka katika skimu za umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo hilo la umwagiliaji Wizara imeongeza bajeti kutoka Shilingi Bilioni 46.5 za mwaka wa fedha 2021 hadi Bilioni 361.5 ambalo ni ongezeko la asilimia 677. Uwekezaji huu matarajio yake ni kuongeza mtandao wa umwagiliaji kwa hekta 95,000 kuwa na ofisi za umwagiliaji kwenye Wilaya 146 na magari 38 kwa ajili ya ofisi za umwagiliaji za Mikoa pamoja na kutengeneza ajira 475,000.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kuimarisha huduma za ugani ili kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao nchini. Itawezesha upatikanaji wa huduma za upimaji wa afya ya udongo kwa wakulima kwa huduma ya msingi na ya lazima. Huduma hiyo itaenda sambamba na kusajili wakulima na kuwaweka kwenye Kanzi Data maalum. Aidha, kila mkulima atapewa cheti kitakachoonesha afya ya udongo wake katika shamba lake ili kumwezesha kuzalisha mazao kulingana na afya ya udongo wa shamba lake.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia azma hiyo Wizara itanunua na kusambaza vifaa vya kupimia afya ya udongo kwa Maafisa Ugani wa Halmashauri 142, vishikwambi 6,377 na *Extension Kits* 400 katika Halmashauri 46. Wizara itakamilisha ufungaji wa mfumo wa *GPS* kwa pikipiki zote na kuweka mfumo wa usimamizi wa huduma za ugani na kuwezesha kila Afisa Ugani apate sare ambazo atavaa akiwa kazini. Aidha, itawezesha uanzishwaji wa mashamba darasa 400 na mashamba darasa 400 kwa mazao ya kimkakati nay a kipaumbele katika Mikoa ya Singida, Simiyu, Morogoro, Njombe, Ruvuma, Kilimanjaro, Manyara, Tabora, Mara, Iringa, Mbeya.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaanzisha mfumo utakaowawezesha maafisa ugani kuwatambua wakulima bora watakaotumika kutoa huduma za ugani kwa wakulima wengine. Katika kuondokana na tatizo la upungufu wa maafisa ugani, wanafunzi wanaosoma katika vyuo vya kilimo katika ngazi zote kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Wizara

itaanza mfumo wa kuwapeleka katika mafunzo ya vitendo kwa mwaka mmoja kabla ya kuhitimu masomo yao na eneo hilo Serikali itashirikiana na Wadau wa Maendeleo. Ili kulinda ardhi ya kilimo, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, itawezesha upimaji wa ardhi ya kilimo na kuitangaza katika Gazeti la Serikali na kuilinda.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaanzisha kituo cha huduma za mawasiliano ya kilimo *(call centre)* kwa ajili ya kurahisisha huduma. Wizara itaandaa mwongozo wa huduma za ugani na kuusambaza katika Mikoa yote 26.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Sekta Binafsi itaanza kukarabati vituo 200 vya Rasilimali Kilimo vya Kata ambavyo vitatumika kwa ajili ya shughuli za kilimo, jumla ya Milioni 400 zimetengwa. Kupitia Bunge lako Tukufu naomba kuagiza Halmashauri zote ambazo vituo vya rasilimali za kilimo zilijengwa wakabadilisha matumizi yake kuanzia tarehe Mosi Julai, Wizara itaanza kukarabati na kutumia vituo vyake kwa ajili ya mashamba ya mfano na vituo vya kutoa huduma na zana za kilimo.

Mheshimiwa Spika, mahitaji yetu ya mafuta ya kula nchini ni tani 650,000 kwa mwaka ukilinganisha na uzalishaji wa tani 300,000 na tani 350,000 huagizwa nje ya nchi. Kati ya kiasi hicho kinachozalishwa nchini tani 270,000 sawa na asilimia 90 kinatokana na zao la alizeti na kiasi kinachobaki kinachangiwa na mazao mengine ikiwemo chikichi, karanga, nazi, pamba na ufuta.

Mheshimiwa Spika, ili kuziba nakisi ya tani 400,000 za mafuta ya kula tunahitaji kuzalisha tani Milioni 1.4 za alizeti. Kwa sasa tunazalisha wastani usiozidi tani laki Saba ambazo zinatupatia mafuta wastani wa tani 270,000. Ili kuzalisha tani Milioni 1.4 za alizeti zitakazopelekwa kiwandani kukamuliwa kuziba nakisi ya tani 400,000 za mafuta ya kula tunahitaji tani 9,454 za mbegu bora. Kwa maana hiyo, mahitaji yetu ya alizeti ili kukidhi mahitaji ya ndani ni tani Milioni 2.3.

Mheshimiwa Spika, Wizara imejiwekea lengo la kuzalisha tani Milioni Tatu za alizeti ifikapo mwaka 2025 ili kama nchi tuwe na mafuta ya alizeti tani Milioni Moja tunahitaji kulima eneo lenye ukubwa wa hekta Milioni 2.4. Aidha, eneo hili la kilimo linahitaji tani 12,000 za mbegu kwa ajili ya uzalishaji wa tani 1,000,000 mafuta ya kula.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia lengo hilo, Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023 inachukua hatua tatu za kimkakati, pamoja na majukumu ya uhamasishaji Wiaara itazalisha na kugawa tani 5,000 za mbegu bora kwa ruzuku. Jumla ya Bilioni 11 zitatumika kuzalisha mbegu hizo katika mwaka wa fedha 2023/2024. Wizara itagawa tani 10,000 na mwaka 2024/2025 itagawa tani 15,000. Shughuli hiyo ya uzalishaji wa mbegu itafanywa na *ASA* na

kuingia mikataba na Kampuni binafsi kwa ajili ya kuzalisha mbegu na Wizara kuzigawa kwa wakulima kwa ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua ya pili, Wizara inajadiliana na Wizara ya Fedha na Mipango ili kuweka motisha ya kikodi kwa viwanda vinavyozalisha mafuta ya alizeti kwa kuwaondolea kodi ya ongezeko la thamani. Utafiti uliofanywa na Wizara ya Kilimo unaonesha kuwa Serikali itapoteza mapato ya kodi Shilingi Bilioni 53 katika kipindi cha miaka mitatu. Upotevu huo utapungua kila mwaka katika kipindi cha miaka mitatu kwa kuwa viwanda vitaongeza uzalishaji kwani kwa sasa viwanda hivyo vinafanya kazi chini ya asilimia 30 ya uwezo wake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kipindi cha miaka mitatu, uzalishaji katika viwanda hivyo utafikia asilimia 100 na Serikali itakusanya mapato ya ziada kupitia *PAYE* kutokana na ongezeko la ajira linalokadiriwa kufika watu 171,000 kwa mwaka wa kwanza na kufika mpaka watu 717,000 ifikapo mwaka 2026/2027. Mapato mengine yataongezeka ni pamoja na kodi ya mapato na ushuru wa mazao. Makusanyo hayo yataongeza mapato ya Serikali hivyo upotevu ulioelezwa hapo awali ni kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo itafanya viwanda vyetu vinavyochuja mafuta *double refinery*, kuwa shindani na kupunguza ugumu wa maisha kwa watanzania na kuwafanya kuwa na kipato cha ziada na kutumia fedha hizo katika matumizi mengine ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, hatua ya tatu, Wizara imeanza kuvitaka viwanda vinavyochuja mafuta mara mbili kununua mafuta ghafi yanayozalishwa na wazalishaji wadogo *(backyard processors)* ambao wengi wao ni wanawake na vijana ambao wanalima alizeti kwa kutumia mashine ndogondogo za *SIDO*. Mkulima anayelima ekari moja na kukamua mafuta yake na kuuza mafuta kwa bei ya leo anapata faida ya Milioni 1.3. Mkulima anayelima ekari moja na kuuza alizeti aliyovuna kama mbegu anapata faida ya 420,000 tu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kengele ya pili imegonga. Nakuongezea dakika 10, omba fedha.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwa kutambua ukweli kuwa kilimo ni msingi na ustawi wa maisha ya mwanadamu na kwa utashi wa kisiasa wa Serikali ya Awamu ya Sita katika kuendeleza kilimo, Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ina lengo la kukuza uchumi wa nchi kwa kuwekeza fedha katika maeneo ya kipaumbele. Uzalishaji wa mbegu kufika bilioni 43, Utafiti kufika bilioni 40.7, Umwagiliaji kutoka bilioni 46 mpaka bilioni 361, Ujenzi wa maghala bilioni 25. Vilevile, bajeti hii imelenga kutoa ruzuku ya mbolea kwa mazao yote, kuendeleza mashamba makubwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 Wizara inatarajia kukusanya shilingi bilioni 126 na milioni 117 kutokana na vyanzo mbalimbali. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 17.732 zitakusanywa kupitia Fungu 43 na bilioni 126 zitakusanywa kupitia Fungu Na. 05.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha Bajeti ya Wizara ya Kilimo imeongezeka kwa Mafungu yote Matatu kutoka bilioni 294 hadi shilingi 751,123,280,000 sawa na ongezeko la asilimia 153. Sehemu kubwa ya fedha hizo zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji, miundombinu ya uhifadhi, kuimarisha upatikanaji wa mazao, kuimarisha utafiti, uzalishaji wa mbegu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Kilimo inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 751,123,280,000 kupitia Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Fungu 43 kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 368,561,661,000 kupitia Fungu 43 kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 268 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya Maendeleo ambapo shilingi 185,978,709,000 ni fedha za ndani na shilingi 82,927,405,000 ni fedha za nje. Aidha, shilingi 99,655,547,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Shilingi 49,403,470,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 50 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Fungu 05; jumla ya shilingi 366,768,000,000 zinaombwa. Kati ya fedha hizo, shilingi 361,500,000,000 ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ambapo shilingi 350,000,000,000 ni fedha za Ndani na shilingi bilioni 11.5 ni fedha za nje. Aidha, kati ya fedha hizo zinazoombwa, shilingi 5,268,352,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo shilingi 3,630,168,000 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. shilingi 1,638,184,000 ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Fungu 24; jumla shilingi 15,793,267,000 zinaombwa. shilingi bilioni 1.1 ni kwa ajili kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja imetolewa Iamuliwe)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana.

Sasa tunaendelea kwa utaratibu wetu hapa anakuja Mwenyekiti, lakini kabla Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji hajaja kusoma atakuja hapa Mwenyekiti wa Bunge kuja kuendelea, kabla hajaja nina matangazo mawili:-

Tangazo la kwanza, Kamati ya Uongozi mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge Saa Saba tutakutana katika Ukumbi wa Spika jengo la Utawala.

Tangazo linguine, Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kwamba siku ya leo na kesho wakati wa hotuba hii ya wiaala ya Kilimo hapa, Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(TADB)* imeandaa banda la maonesho nyuma ya Ukumbi wa Msekwa. Maonesho hayo ni maalum kwa Waheshimiwa Wabunge kufahamu fursa na huduma za benki hiyo, ikiwemo mikopo kwa wakulima, wafugaji na wavuvi na kutoa elimu kuhusiana na shughuli za benki hiyo kwa ujumla. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnakaribishwa kutembelea banda hilo katika siku hizi mbili.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo Mwenyekiti anakuja kuendelea na ratiba.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. David M. Kihenzile)Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge. Namwita Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ili aweze kuwasilisha. Anayewasilisha ni Mheshimiwa Benaya Kapinga kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba taarifa hii iingizwe yote kwenye Kumbukumbu za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza inahusu taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na maoni ya kuhusu Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa bajeti wa Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, pamoja na maoni ya Kamati ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii imegawanyika katika sehemu nne kama zinavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati. Msingi wa Kamati kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara ya Kilimo ni Masharti ya Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 6 (7) (a) kikisomwa kwa pamoja na kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo. Kanuni ya 117(4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yaliyotokana na Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Wizara hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Hivyo naomba Bunge lipokee na kujadili taarifa hii kwa lengo la kuboresha na kuridhia hoja ya Waziri wa Kilimo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ninayoiwasilisha inajumuisha mafungu matatu ambayo ni Wizara ya Kilimo Fungu 43, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Fungu 45 na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Fungu 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya pili inahusu uchambuzi na Tathmini iliyofanywa na Kamati kuhusiana na hoja ya Waziri wa Kilimo kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Masuala yanayochambuliwa ni Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti wa Wizara ya Kilimo baada ya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Mambo yaliyochambuliwa ni pamoja na ukusanyaji wa maduhuli, upatikanaji wa fedha za matumizi ya kugharamia miradi ya maendeleo na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa makusanyo na maduhuli unaonesha kwamba:

(a) Jumla ya makusanyo ya maduhuli si ya kuridhisha, kwani hadi kufikia mwezi Februari, 2022 Wizara na Taasisi zake zilifikia wastani wa 11.29% ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 3.89 kati ya shilingi bilioni 34.4 zilizokusudiwa ikiwa ni ndani ya kipindi cha robo ya tatu ya utekelezaji ya majukumu ya Wizara.

(b) Mwenendo wa makusanyo ya maduhuli ya Wizara hadi kufikia mwezi Februari ulifikia 78.28% ya lengo la kukusanya jumla ya shilingi bilioni 3.5 kati ya shilingi bilioni 4.4.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imefikia asilimia 1.3 ya lengo kwa kukusanya jumla ya shilingi milioni 311,975 kati ya shilingi bilioni 30.01.

(d) Kwa kipindi kilichobaki cha utekelezaji ni vigumu kufikia lengo lililokusudiwa hasa ikizingatiwa kuwa kipindi kilichokwisha katika utekelezaji ni takribani 75%.

(e) Kwa upande wa Wizara ya Kilimo imefanya vizuri kwa kukusanya 78.28% ya lengo kwa kipindi cha robo ya tatu ya utekelezaji wa bajeti. Hivyo uwezekano wa kufikia malengo ni mkubwa.

(f) Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa kipindi cha utekelezaji wa bajeti kwa 75% imekusanya chini ya 2% ambapo kiasi kikubwa cha makusanyo kinategemewa kupatikana kutokana na ada za huduma ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenendo wa makusanyo wa maduhuli ya Wizara unatoa mwelekeo wa kufikia lengo. Changamoto kubwa iko Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ambayo inatarajia ada za huduma ya umwagiliaji zikikusanywa kwa ukamilifu wake zitatumika kukarabati na kujenga skimu za umwagiliaji ili kufanikisha wakulima wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ya Kilimo inatekeleza jumla ya miradi tisa chini ya Fungu 43; miradi mitano Fungu 5; na miradi minne inatekelezwa nje ya bajeti ya Serikali *off budget projects*. Jumla ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya kugharamia miradi hiyo ni Shilingi bilioni 211.2 sawa na 72.20% ya bajeti ya Wizara ya Kilimo na bajeti ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa madhumuni ya kuzingatia masharti ya kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea miradi minne ifuatayo:-

(a) Mradi wa ujenzi wa Makao Makuu ya Ofisi ya Wizara unaoendelea unaotekelezwa katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma eneo la Mtumba ambapo utekelezaji wake unalenga kufanikisha azma ya Serikali kuhamia Dodoma.

(b) Mradi wa ukarabati wa Ofisi ya Bodi ya Mkonge unaotekelezwa katika Manispaa ya Tanga kupitia program ya kuendeleza Sekta ya Kilimo ya Awamu ya Pili *ASDP II.* Lengo la kutekeleza mradi huu ni kuiwezesha Bodi ya Mkonge kuwa na ofisi ya kudumu kwa ajili ya kusimamia na kuongeza uzalishaji wa zao la mkonge.

(c) Mradi wa ujenzi wa kituo cha udhibiti wa visumbufu kibaologia na usanifu wa maabara kuu ya kilimo na kituo mahiri cha usimamizi wa mazao baada ya kuvuna, unatekelezwa katika Halmashauri ya Mji

wa Kibaha kwa kutumia fedha za ndani kutoka bajeti ya Serikali na fedha za nje kutoka kwa wadau wa maendeleo.

(d) Mradi wa ukarabati au ujenzi wa skimu ya umwagiliaji wa shamba la zabibu Chinangali II ambapo unatekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino kwa ushirikiano kati ya Wizara ya Kilimo, Ofisi ya TAMISEMI na Chama cha Ushirika, CHABUMA kwa lengo la kuibua uzalishaji wa zao la zabibu katika Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara hiyo, Kamati ilibaini na kujifunza kuwa:-

(a) Ofisi ya Rais TAMISEMI inaweza kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za kilimo kupitia Halmashauri zake kwa kuwasaidia wakulima kujiunga kwenye vyama vya ushirika na kudhamini upatikanaji wa mikopo kupitia benki za kibiashara nchini.

(b) Bado kuna haja ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika kutekeleza jukumu lake la msingi la Usimamizi na Uendeshaji wa Vyama vya Ushirika kwa ajili ya manufaa ya wanaushirika.

(c) Serikali ihakikishe makosa yaliyoua Bodi za Mazao mbalimbali hayajirudii katika maboresho yanayofanywa ili kuhakikisha mazao yanayosimamiwa na Bodi za Mazao yanazalisha kwa tija na yanachangia pato la Taifa na kutoa ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo haukuwa kama ulivyotarajiwa. Hali hii, siyo dalili nzuri katika utekelezaji bora wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika waliidhinishiwa jumla ya Shilingi bilioni 81.8 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia mwezi Februari 2022, kiasi cha fedha zilizopokelewa ilikuwa Shilingi bilioni 48.9 sawa na asilimia 59.69 ya kiasi kilichoidhinishwa. Mchanganuo wa upokeaji wa fedha unaonekana katika Jedwali Na. 01 katika ukurasa wa tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi unaonesha kwamba:

(a) Mwenendo wa jumla wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida siyo mbaya, kwani uchambuzi umeonesha hadi kufikia mwezi Februari, 2022 mafungu yote yalikuwa yamepokea kiasi cha zaidi ya 61%.

(b) Juhudi za makusudi za kuimarisha kilimo cha umwagiliaji zimeendelea kuchukuliwa na Serikali ambapo Tume ya Taifa ya

Umwagiliaji hadi kufikia mwezi Februari, 2022 ilikuwa imepokea zaidi ya asilimia 80 ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Taasisi zilizo chini yake, Kamati ilishauri kuhusu mambo mbalimbali. Naomba kulijulisha Bunge kuwa, Taarifa ya Waziri wa Kilimo ilionesha kwamba, Serikali imezingatia sehemu kubwa ya ushauri. Mfano wa ushauri wa Kamati uliozingatiwa ni kuhusu kuimarisha huduma za ugani kwa kuongeza bajeti kwa ajili ya kuwapatia wagani vitendea kazi muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Utekelezaji ilionesha Serikali imeongeza bajeti ya huduma za ugani kutoka Shilingi milioni 603 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 hadi Shilingi bilioni 11.5 kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Kwa kuthibitisha hilo, Kamati ilishuhudia hafla ya Uzinduzi wa Ugawaji wa Vitendea Kazi kwa Maafisa Ugani ulioongozwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan tarehe 4 Aprili, 2022 ambapo pikipiki 7,000, vifaa vya kupima afya ya udongo 143 pamoja na simu janja 384 viligawiwa kwa Maafisa Ugani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mazingatio mazuri ya ushauri, upo ushauri uliotolewa na Kamati ambao unahitaji kufanyiwa kazi na Serikali. Kwa mfano, suala la kuhakikisha maelekezo ya kuzitaka Halmashauri kurudisha 20% ya mapato yatokanayo na ushuru wa mazao kurejeshwa kwa ajili ya kuendeleza Sekta ya Kilimo kutungiwa sheria ili kulipa nguvu katika utekelezaji wake, bado ushauri huu haujatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa pamoja zimekadiriwa kukusanya maduhuli na kutengewa bajeti ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kulinganisha na bajeti inayomalizika. Uchambuzi wa maduhuli na makadirio ya matumizi hayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Kilimo alieleza Kamati kuwa, jumla ya Shilingi bilioni 116.1 zinakadiriwa kukusanywa na Wizara ya Kilimo na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kiasi hicho ni ongezeko la asilimia 298.27 ikilinganishwa na lengo la maduhuli kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Mchanganuo wa makadirio hayo unaoneshwa katika Jedwali Na. 2 katika ukurasa wa 12 wa taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa:

(a) Kwa ujumla Makadirio ya Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yameongezeka kwa asilimia 298.27 ikilinganishwa na

lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo kuna ongezeko la zaidi ya asilimia 286.80

(b) Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeongezewa ukusanyaji wa madhuhuli kwa zaidi ya asilimia 286.80 wakati mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kwa kipindi cha robo tatu ya utekelezaji wa bajeti ulifikia asilimia 1.3 tu. Kwa maelezo hayo, haitakuwa rahisi kufikia lengo la makusanyo lililowekwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ikizingatiwa uzoefu uliopatikana kwa mwaka wa fedha unaomalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kwamba, uwekaji wa lengo la makusanyo utakuwa na tija iwapo utazingatia uhalisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika wanakadiriwa kutumia shilingi bilioni 90.9 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kiasi hicho ni ongezeko la matumizi ya kawaida kwa asilimia 27.89 ikilinganishwa na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Hali hiyo ikilinganishwa na uzoefu wa upatikanaji wa fedha kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ili kuona uwezekano katika hali halisi, Kamati imejiridhisha kuwa ukadiriaji huu wa matumzi ya kawaida unaonyesha uhalisia wakati wa utekelezaji wa bajeti inayoombwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi umeonesha kuwa katika bajeti ya Wizara ya Kilimo kuna ongezeko la bajeti la asilimia 73.61 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022. Mchanganuo wa Makadirio hayo unaonekana katika Jedwali Na. 03 ukurasa 14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu hizi zinadhihirisha kuwa uendeshaji wa shughuli za Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika zimeongezewa msukumo katika bajeti. Kamati imejiridhisha kuwa makadirio ya bajeti ya matumizi ya kawaida yanaendana na utekelezaji wa bajeti ya miradi maendeleo. Jambo la kuzingatia ni Serikali kuiwezesha Wizara kupata fedha kwa kadri ya mahitaji ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilichambua makadirio ya jumla ya shilingi bilioni 731.1 kwa ajili ya kugharimia miradi ya Maendeleo inayopangwa kutekelezwa na Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Makadirio hayo ni ongezeko la asilimia 153 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 04 katika ukurasa wa 16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa jumla unaonesha kwamba:-

(a) Bajeti ya Maendeleo kwa Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeongezeka kwa asilimia 280. Tafsiri ya ongezeko hili ni kwamba idadi, thamani, na ukubwa wa miradi inayotekelezwa itaongezeka ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2021/2022 na hivyo kuongeza uzalishaji na tija kwa kilimo.

(b) Pamoja na bajeti ya Kilimo kuongezeka bado ongezeko hilo halikidhi mahitaji ya Wizara ambayo ni angalau Shilingi trilioni mbili kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie. Pamoja na ongezeko hili bado ongezeko hili halikidhi mahitaji ya Wizara ambayo ni angalau Shilingi trilioni mbili kwa mwaka. *(Makofi)*

(c) Kiasi cha Shilingi bilioni 751.1 zilizotengwa kutekeleza Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ni sawa na asilimia 1.83 ya Bajeti ya Taifa ambapo shilingi trilioni 41.06 haijakidhi matakwa ya utekelezaji wa Azimio la Maputo la Mwaka 2003 na Malabo la Mwaka 2014 ambapo linataka nchi wanachama kutenga asilimia 10 ya Bajeti ya Taifa kwa ajili ya kuendeleza sekta ya kilimo. *(Makofi)*

(d) Kwa mara ya kwanza mwaka huu Tume ya Maendeleo ya Ushirika imekasimiwa Bajeti ya Maendeleo ambayo itasaidia kuimarisha uwezo wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchambuzi huo, ni wazi kwamba Wizara na Taasisi zilizo chini yake zitaongezewa uwezo wa utekelezaji wa miradi ikilinganishwa na utekelezaji wa mwaka wa fedha 2021/2022. Ni maoni ya Kamati kuwa, utekelezaji wa miradi ya maendeleo nchini unaweza kuwa na mafanikio endapo Wizara itapewa fedha zilizoombwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu maoni na ushauri. Kutokana na uchambuzi wake, Kamati inatoa ushauri kuhusu maombi ya fedha kwa Wizara ya Kilimo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo: -

(i) Kwa kuwa bajeti iliyoongezwa kwa kiasi kikubwa ni mkopo kutoka Shirika la Fedha Duniani *(IMF)* ili mkopo huu uweze kulipika ni lazima bajeti iliyoidhinishwa na Bunge itolewe kwa wakati ili kuwezesha utekelezaji wa malengo na mikakati iliyokusudiwa na urejeshwaji wa mkopo huo kwa wakati. *(Makofi)*

(ii) Ili bajeti iliyoongezeka ilete tija inayokusudiwa rasilimali watu ni nyenzo muhimu katika kufikia malengo yaliyobainishwa. Kamati inashauri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma iwezeshe upatikanaji wa watumishi wanaohitajika mapema iwezekanavyo na kulingana na mahitaji. Aidha Wizara ya Kilimo ishirikishwe kuainisha kada ya watumishi kulingana na mahitaji na mipango iliyojiwekea.

(iii) Kiasi cha Nyongeza bajeti iliyotolewa kwa mkopo kwenye masharti nafuu kitatumika kujenga uzio wa mashamba ya kuzalisha mbegu yaliyovamiwa na wananchi ili kuzuia uvamizi wa mashamba hayo. Kamati inashauri, ili kuongeza ufanisi wa fedha za mkopo fedha zilizopangwa kujengea uzio zitumike kwenye kuongeza uzalishaji. Aidha juhudi za ulinzi wa mashamba hayo zifanyike kwa kuwamilikisha ardhi za mashamba hayo kisheria kwa kupata hati, kupanda miti kuzunguka mashamba husika, ikiwa pia ni njia ya kuhifadhi mazingira na kujenga mahusiano mazuri na wananchi wanaozunguka mashamba hayo.

(iv) Wizara ya Kilimo iendelee na mikakati ya kujenga uelewa wa pamoja kwa viongozi wa kitaifa Ofisi ya TAMISEMI, Wizara ya Fedha, Benki Kuu, Wizara ya Viwanda na Biashara, taasisi za kifedha na sekta binafsi ili taasisi iwe na uelewa wa pamoja kuhusu dhana ya kilimo ni uchumi, kilimo ni ajira na kilimo ni malighafi ya viwanda. Uelewa wa pamoja utasaidia kutoa kipaumbele kwenye upatikanaji, upangaji wa bajeti kwa sekta ya kilimo.

(v) Kutokana na kuendelea kupanda kwa bei ya mbolea siku hadi siku imekuwa ni vigumu kwa wakulima kumudu gharama za mbolea. Kamati inashauri Serikali iandae mpango mkakati wa utoaji ruzuku kwenye mbolea ili kumpunguzia mkulima gharama za uzalishaji pamoja na kunusuru mfumuko wa bei za vyakula.

(vi) Wizara ya Kilimo itumie changamoto inayoikabili dunia ya uhaba wa bidhaa za ngano na mafuta ya kula kama fursa ya kuongeza uzalishaji, uchakataji na biashara ya mazao hayo. Kwa kufanya hivyo nchi yetu itaongeza fursa ya ajira, uhakika wa soko la Afrika Mashariki lakini pamoja na kuipunguzia Serikali gharama kubwa ya kutumia fedha za kigeni kwaajili ya kuagiza bidhaa hizo kutoka nje.

(vii) Wizara ya Kilimo ishirikiane na Ofisi ya Rais TAMISEMI na kuandaa mpangokazi utakaowezesha mikopo ya halmashauri inayotolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kutumika kwenye Kilimo.

(viii) Utekelezaji wa ujenzi na uboreshaji wa barabara za vijijini ushirikishe Wizara ya Kilimo. Kwa kufanya hivyo kutawezesha ujenzi wa barabara

hizo kwa kutoa kipaumbele kwenye maeneo yenye uzalishaji mkubwa.

(ix) Fedha za mpango zitakazotumika kuimarisha miundombinu ya uzalishaji mbegu pamoja na kuzalisha mbegu bora na miche ya kisasa izingatie mahitaji ya mbegu za asili kwa kutafiti, kuzalisha na kuzifufua ili kulinda utamaduni wetu pamoja na umuhimu wa virutubisho vilivyopo kwenye mbegu za asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Kamati ina ushauri ufuatao: -

(i) Serikali iimarishe ushirika kwa kutenga bajeti ya kutosheleza, maafisa ushirika kupata vitendea kazi kwaajili ya kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi; ikiwa pamoja na kuvisimamia kikamilifu vyama vya ushirika vinavyokiuka taratibu za kuongoza vyama hivyo.

(ii) Wizara iharakishe mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Namba Sita ya Mwaka 2013 na Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya Mwaka 2002. Mapungufu ya kisheria na kisera yamepelekea baadhi ya viongozi wa vyama vya ushirika kutumia mwanya huo kukiuka taratibu za kiuongozi katika vyama vya ushirika.

(iii) Kuendelea kuchukua hatua stahiki za kuimarisha mfumo wa ushirika ili kuwezesha mazao yote ya kilimo kuwekewa utaratibu wa kuwa na ushirika kwa ajili ya kupata pembejeo, ikiwemo mbolea mbegu bora na viuatilifu kwa wakati na bei nafuu ili kuongeza tija na upatikanaji wa masoko wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, Ushauri wa Kamati katika utekelezaji wa Mipango ya Tume hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, ni kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kutumia fedha za mkopo wenye masharti nafuu kutoka Shirika la Fedha Duniani, Wizara imepanga kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika skimu mpya 25 zenye jumla ya hekta 53,234. Kamati inashauri kabla ya kuanza ujenzi wa skimu mpya, fedha hizo zitumike kufanya matengenezo ya skimu mbalimbali za umwagiliaji ambazo kwa muda mrefu zimekuwa hazifanyi vizuri kutokana na ukosefu wa bajeti ya kuboresha skimu hizo.

(ii) Kuweka mikakati thabiti ya ukusanyaji wa ada za umwagiliaji kwa lengo la kuwezesha ujenzi wa skimu nyingi zaidi kwa maeneo mbalimbali nchini. Aidha, ukusanyaji wa ada hizo usimamiwe kikamilifu.

(iii) Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji utekelezwe na wakandarasi kutoka sekta binafsi ili iwe rahisi kuwawajibisha endapo kutatokea

hitilafu ya aina yoyote. Kwa msingi huo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itabaki kuwa msimamizi na mkaguzi wa ujenzi wa miundombinu na miradi inayotekelezwa.

(iv) Ujenzi wa skimu mpya za umwagiliaji uzingatie maeneo yanoyafaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Aidha, ili miradi hiyo iwe endelevu ni vyema ikashirikisha Halmashauri husika na Wabunge wa maeneo miradi inapotekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne ni hitimisho. Kama inavyofahamika, Maendeleo katika sekta ya kilimo ni muhimu, hasa katika kukuza uchumi wa taifa na kuleta msukumo kwenye ukuaji wa sekta ya viwanda. Ukuaji wa sekta hii una umuhimu mkubwa katika kuzalisha chakula cha kutosha ili kuhakikisha uwepo wa usalama wa chakula na lishe kwa wananchi wakati wote. Sekta ya kilimo inachangia takribani asilimia 29.1 ya Pato la Taifa, asilimia 65.5 ya ajira, asilimia 65 ya malighafi inayotumika katika sekta ya viwanda na asilimia 30 ya pato la bidhaa zinazouzwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, Wizara ya Kilimo ni mwezeshaji na mratibu muhimu wa kufanikisha utekelezaji wa mipango mbalimbali ikiwemo Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Wwamu ya Pili na utekelezaji wa Malengo Endelevu ya Milenia *(SGDs);* hususani lengo namba moja linalohusu kupunguza umaskini uliokithiti na lengo namba mbili linalohusu kutokomeza tatizo la utapiamlo kwa kuimarisha lishe bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani. Naomba kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya Wizara ya Kilimo. Kutokana na umuhimu wao natamani kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa kuwataja majina yao. Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda naomba majina yao yazingatiwe kwenye Kumbukumbu ya Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuona umuhimu wa sekta ya kilimo. Kwa kipindi kifupi cha uongozi wake tumeshuhudia kasi kubwa ya ongezeko la bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa lengo la kuongeza tija kwenye kilimo. Vile vile napenda kumshukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na wenyeviti kwa kusimamia na kuliongoza vema Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumshukuru Waziri Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe (Mb) kwa ushirikiano mkubwa anaoutoa kwa Kamati, ambapo umechangia kwa sehemu kubwa kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake. Utendaji wake na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Anthony Mavunde (Mb) umedhihirisha jinsi vijana walivyo hazina kubwa kwa ustawi na maendeleo ya taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru pia watendaji wote wa Wizara ya Kilimo na Taasisi zilizo chini ya Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Andrew Massawe, akisaidiana na Naibu Katibu Mkuu, Profesa Siza Tumbo kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati. Aidha, nampogeza Ndugu Gerald Mweli kwa kuhamishiwa Wizara ya Kilimo kama Naibu Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Bunge Ndugu Dickson Bisile, Makatibu wa Kamati Ndugu Rachel Nyega na Eunice Shirima, wakisaidiwa na Ndugu Waziri Kizingiti, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 NA MAONI YA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 MAELEZO YA JUMLA

### 1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/ 2023.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu **NNE** zifuatazo: -

(a) Sehemu ya **Kwanza** inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;
(b) Sehemu ya **Pili** inaripoti matokeo ya Uchambuzi na Tathmini kwa kuchanganua Utekelezaji wa Malengo ya Mpango wa Wizara hii, Ukusanyaji wa Maduhuli, Upatikanaji wa fedha na uzingatiaji wa ushauri wa Kamati;
(c) Sehemu ya **Tatu** inaripoti Maoni na Ushauri wa Kamati kutokana na uchambuzi; na
(d) Sehemu ya **Nne** inahitimisha na kulishauri Bunge kuhusu hoja ya Waziri wa Kilimo.

**1.2 Msingi wa Uchambuzi wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa Kamati kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara ya Maji ni Masharti ya Kanuni za Bunge. Kifungu cha 6 (7) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo.

Kanuni ya 117(4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yaliyotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Wizara hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Hivyo, naomba Bunge lipokee na kujadili taarifa hii kwa lengo la kuboresha na kuridhia Hoja ya Waziri wa Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**1.3 Mawanda ya Uchambuzi**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo inajumuisha mafungu matatu yaani: -Wizara ya Kilimo (Fungu 43), Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (Fungu 05) na Tume ya Maendeleo ya Ushirika (Fungu 24).

**SEHEMU YA PILI**

**2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI**

**2.1 Ufafanuzi wa Jumla**

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inakusudia kujenga msingi wa ushauri wa Kamati kuhusiana na Hoja ya Waziri wa Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Masuala yanayochambuliwa ni Taarifa za Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**2.2 Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo baada ya ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo.

Mambo yaliyochambuliwa ni pamoja na Ukusanyaji wa Maduhuli, Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya kugharimia Miradi ya Maendeleo na Upatikanaji wa Fedha kwa ajili ya kugharamia Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa makusanyo ya maduhuli unaonesha kwamba:

(a) Jumla ya makusanyo ya maduhuli si yakuridhisha kwani hadi kufikia mwezi Februari, 2022, Wizara na Taasisi zake zilifikisha wastani wa **asilimia 11.29** ya lengo kwa kukusanya jumla ya **shilingi 3,896,038,539.46** kati ya **shilingi 34,495,500,000.00** zilizokusudiwa ikiwa ni ndani ya robo tatu za utekelezaji wa majukumu;

(b) Mwenendo wa makusanyo ya maduhuli ya Wizara hadi kufikia mwezi Februari ulifikia **asilimia 78.28** ya lengo na kwa kukusanya jumla ya **shilingi 3,507,026,664.46** kati ya **shilingi 4,480,000.00** zilizokusudiwa;

(c) Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imefika **asilimia 1.3** ya lengo kwa kukusanya jumla ya shilingi **389,011,875.00** kati ya **shilingi 30,015,000,000. 00** zilizokusudiwa;

(d) Kwa kipindi kilichobaki cha utekelezaji, ni vigumu kufikia lengo kwa kuwa kipindi kilichokwisha katika utekelezaji ni takribani **asilimia 75**;

(e) Wizara ya Kilimo wamefanya vizuri kwa kukusanya **asilimia 78.28** ya lengo ndani ya kipindi cha robo tatu ya utekelezaji wa bajeti, hivyo uwezekanao wa kufikia malengo ni mkubwa; na

(f) Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa kipindi cha utekelezaji wa bajeti kwa **asilimia 75,** imekusanya chini ya **asilimia 2** ambapo kiasi kikubwa cha makusanyo kinategemewa kupatikana kutokana na ada za huduma ya umwagiliaji.

**Mheshimiwa Spika**, mwenendo wa makusanyo ya madhuhuli ya Wizara unatoa mwelekeo wa kufikia lengo, changamoto kubwa iko kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ambayo inatarajiwa ada za huduma ya umwagiliaji zikikusanywa kwa ukamilifu wake zitatumika kukarabati na kujenga skimu za umwagiliaji ili kuwanufaisha wakulima wengi zaidi.

### 2.3 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara ya Kilimo inatekeleza jumla ya miradi 9 chini ya Fungu 43, miradi 5 Fungu 05 na miradi 4 inatekelezwa nje ya Bajeti ya Serikali (*Off Budget Projects*). Jumla ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya kugharimia miradi hiyo ni shilingi **211,248,000,000.00** sawa na **asilimia 72.20** ya bajeti ya Wizara ya Kilimo na bajeti ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa madhumuni ya kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilitembelea miradi 4 ifuatayo: -

(a) Mradi wa Ujenzi wa Makao Makuu ya Ofisi za Wizara unaotekelezwa katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma eneo la Mtumba. Mradi huu ni utekelezaji wa azma ya Serikali ya kuhamia Dodoma;

(b) Mradi wa Ukarabati wa Ofisi ya Bodi ya Mkonge unaotekelezwa katika Manispaa ya Tanga kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II); Mradi huu unalenga kuiwezesha Bodi ya Mkonge kuwa na Ofisi ya Kudumu kwa ajili ya kuhakikisha uzalishaji wa zao la Mkonge unaongezeka;

(c) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha udhibiti wa visumbufu kibailojia na Usanifu wa Maabara Kuu ya Kilimo na kituo mahiri cha usimamizi wa mazao baada ya kuvuna. Mradi huu unatekelezwa katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha kwa

kutumia fedha za ndani kutoka bajeti ya Serikali na fedha za nje kutoka kwa wadau wa maendeleo; na

(d) Mradi wa ukarabati/ujenzi wa skimu ya umwagiliaji wa shamba la zabibu Chinangali II, ambao unatekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino kwa ushirikiano kati ya Wizara ya Kilimo, Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Chama cha Ushirika CHABUMA kwa lengo la kuinua uzalishaji wa zao la zabibu katika mkoa wa Dodoma.

**Mheshimiwa Spika,** katika ziara hiyo Kamati ilibaini na kujifunza kuwa:

(a) Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) inaweza kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za kilimo kupitia Halmashauri zake kwa kuwasaidia wakulima kujiunga kwenye Vyama vya Ushirika na kudhamini upatikanaji wa mikopo kupitia benki za biashara nchini.

(b) Bado kuna haja ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika kutekeleza jukumu lake la msingi la Usimamizi na Uendeshaji wa Vyama vya Ushirika kwa kutoa elimu na kuajiri Watendaji wa Vyama vya Ushirika wenye weledi na utaalamu wa kuendesha Vyama vya Ushirika kwa ajili ya manufaa ya wanaushirika.

(c) Serikali ihakikishe makosa yaliyoua Bodi za Mazao mbalimbali hayajirudii katika maboresho yanayofanywa ili kuhakikisha mazao yanayosimamiwa na Bodi za Mazao yanazalisha kwa tija, yanachangia Pato la Taifa na kutoa ajira kwa Watanzania.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo haukuwa kama ulivyotarajiwa. Hali hiyo, si dalili nzuri kwa utekelezaji bora wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa. Ni maoni ya Kamati kuwa ubora wa miradi iwapo utekelezaji wake utakwenda kama ilivyopangwa kwa kuipatia Wizara sawasawa na mahitaji yake.

### 2.4 Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika waliidhinishiwa jumla ya **shilingi 81,894,780,509.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia mwezi Februari 2022, kiasi cha fedha zilizopokelewa ni **shilingi 48,995,773,678.90** sawa na **asilimia 59.69** ya kiasi kilichoidhinishwa. Mchanganuo wa upokeaji wa fedha unaonekana katika **Jedwali Na. 01**.

**Jedwali Na. 1: Hali ya Upatikanaji wa Fedha kwa Matumizi ya Kawaida**

| Na. | WIZARA/TAASISI | MAKADIRIO KWA MWAKA 2021/2022 | KIASI KILICHOPATIKANA HADI MWEZI FEBRUARI, 2022 | ASILIMIA YA MAKADIRIO |
|---|---|---|---|---|
| | WIZARA YA KILIMO | 64,123,243,000.00 | 37,894,780,594.00 | 58.94 |
| | TUME YA UMWAGILIAJI | 4,987,450,000.00 | 3,318,087,466.64 | 82.03 |
| | TUME YA USHIRIKA | 12,803,378,000.00 | 7,782,905,618.26 | 61 |
| **JUMLA** | | **81,894,780,509.00** | **48,995,773,678.90** | **59.69** |

**Chanzo**: ***Randama ya Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24***

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi unaonesha kwamba:

(c) Mwenendo wa jumla wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida si mbaya, kwani uchambuzi umeonyesha hadi kufikia mwezi Februari, 2022 Mafungu yote yalikuwa yamepokea kiasi ambacho ni zaidi ya **asilimia 61** ya bajeti zake ikiwa ni robo tatu ya kipindi cha utekelezaji.

(d) Juhudi za makusudi za kuimarisha kilimo cha umwagiliaji zimeendelea kuchukuliwa na Serikali ambapo Tume ya Taifa ya Umwagiliaji hadi kufikia mwezi Februari, 2022 ilikuwa imepokea zaidi ya **asilimia 80** ya bajeti yake.

**2.5 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Taasisi zilizo chini yake, Kamati ilishauri kuhusu mambo mbalimbali. Naomba kulijulisha Bunge hili kuwa, Taarifa ya Mtoa hoja ilionesha kwamba, Serikali imezingatia sehemu kubwa ya Ushauri. Mfano wa Ushauri wa Kamati uliozingatiwa ni kuhusu kuimarisha huduma za ugani kwa kuongeza bajeti kwa ajili ya kuwapatia wagani vitendea kazi muhimu.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa za utekelezaji zilionesha Serikali imeongeza bajeti ya huduma za ugani kutoka **shilingi milioni 603** Mwaka 2020/2021 hadi **shilingi bilioni 11.5** Mwaka 2021/2022. Kwa kuthibitisha hilo, Kamati ilishuhudia hafla ya Uzinduzi wa Ugawaji wa Vitendea Kazi kwa Maafisa Ugani uliongozwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan tarehe 4 Aprili, 2022 ambapo pikipiki 6,000, vifaa vya kupima afya ya udongo 143 pamoja na simu janja 384 vimegawiwa kwa Maafisa Ugani.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na uzingatiaji mzuri wa ushauri, upo ushauri uliotolewa na Kamati ambao unahitaji kufanyiwa kazi na Serikali. Kwa mfano, suala la kuhakikisha maelekezo ya kuzitaka Halmashauri kurudisha **asilimia 20** ya mapato ya Halmashauri yatokanayo na ushuru wa mazao yanatakiwa kurejeshwa kwa ajili ya kuendeleza Sekta za Kilimo kulifanya kuwa na nguvu ya kisheria katika utekelezaji wake.

Kamati ilipendekeza suala hili liboreshwe zaidi kwa kuifanyia marekebisho Sheria ya Fedha ya Halmashauri za Wilaya ya mwaka 1982 (*Local Government Finance Act,* 1982) ili kuingiza kipengele kitakachoruhusu kutenga **asilimia 20** ya fedha ya mapato ya ndani ya Halmashauri zitokanazo na ushuru wa mazao kwa ajili ya maendeleo ya kilimo ikiwa ni sehemu ya kuimarisha ugharamiaji wa Sekta ya Kilimo.

**2.6 Makadirio ya Maduhuli na Matumizi**

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa pamoja zimekadiriwa kukusanya maduhuli na kutengewa bajeti ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu

kuwa, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kulinganisha na bajeti inayomalizika. Uchanganuzi wa Maduhuli na Makadirio ya Matumizi hayo ni kama ifuatavyo:

### 2.6.1 Makadirio ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** mtoa hoja alieleza kuwa, Jumla ya shilingi **116,117,732,000.00** zinakadiriwa kukusanywa na Wizara ya Kilimo na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Kiasi hicho ni ongezeko la **asilimia 298.27** ikilinganishwa na lengo la maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Mchanganuo wa makadirio hayo unaoneshwa katika **Jedwali Na. 2.**

**Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka 2022/23 ikilinganishwa na Mwaka 2021/22**

| Na | Wizara/ Taasisi /Mikoa | Makadirio ya Maduhuli kwa mwaka 2021/2022 | % jumla kwa wizara | Makadirio kwa mwaka 2022/2023 | Ongezeko | Ongezeko kwa Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | WIZARA YA KILIMO | 4,480,000.00 | 5.71 | 17,732,000.00 | 13,252,000.00 | 74.73 |
| | TUME YA UMWAGILIAJI | 30,015,000,000.00 | 1.3 | 116,100,000,000.00 | 86,085,000,000 | 286.80 |
| | TUME YA USHIRIKA | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| **JUMLA** | | **30,019,480,000.00** | | **116,117,732,000.00** | **86,098,252,000** | **298.27** |

***Chanzo:*** *Randama za Fungu 43 na Fungu 05*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi umeonesha kwamba:

(c) Kwa ujumla makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 yameongezeka kwa **asilima 298.27** ikilinganishwa na lengo la makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Ambapo ongezeko la zaidi ya **asilimia 286.80** limeongezeka kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.

(d) Kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeongezewa ukusanyaji wa madhuhuli kwa zaidi ya **asilimia 286.80** wakati mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kwa kipindi cha Robo tatu za utekelezaji wa bajeti ulifikia **asilimia 1.3** tu. Haitakuwa rahisi kufikia lengo la makusanyo linalowekwa kwa Mwaka wa

Fedha 2022/2023 ikizingatiwa uzoefu uliopatikana kwa Mwaka wa Fedha uliotangulia.

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kwamba, uwekaji wa lengo la makusanyo utakuwa na tija iwapo utazingatia uhalisia. Kwa mfano; kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilifikia lengo la makusanyo chini ya **asilimia 2** katika kipindi cha robo tatu ya muda wa utekelezaji, lakini lengo linalowekwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 limeongezeka kwa **asilima 286.27**. Ni dhahiri kuwa kama hakuna maelezo ya kutosha kwa lengo la makusanyo linalowekwa, Wizara ya Kilimo itakuwa na lengo la maduhuli ambalo halitekelezeki.

### 2.6.2 Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika wanakadiria kutumia **shilingi 90,995,875,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kiasi hicho ni ongezeko la matumizi ya kawaida kwa **asilimia 27.89** ikilinganishwa na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Hali hiyo ililinganishwa na uzoefu wa upatikanaji wa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ili kuona uwezekano katika hali halisi. Kamati imejiridhisha kuwa ukadiriaji huu wa matumzi ya kawaida unaonyesha uhalisia wakati wa utekelezaji wa bajeti inayoombwa.
**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi umeonesha kuwa katika bajeti ya Wizara ya Kilimo kuna ongezeko la bajeti kwa **asilimia 27.89** ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/2022. Mchanganuo wa Makadirio hayo unaonekana katika **Jedwali Na. 03.**

**Jedwali Na. 3: Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2021/2022**

| Na. | TAASISI | MAKADIRIO KWA MWAKA 2021/2022 | MAKADIRIO KWA MWAKA 2022/2023 | ASILIMIA KATIKA ONGEZEKO |
|---|---|---|---|---|
| | WIZARA YA KILIMO | 64,123,243,000.00 | 99,655,547,000.00 | 55.42 |
| | TUME YA UMWAGILIAJI | 4,987,450,000.00 | 5,268,352,000.00 | 5.33 |
| | TUME YA USHIRIKA | 12,803,378,000.00 | 14,693,267,000.00 | 12.86 |
| **JUMLA** | | **81,914,O71,000.00** | **119,617,166,000.00** | **73.61** |

***Chanzo: Randama za Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24***

**Mheshimiwa Spika,** takwimu hizi zinadhihirisha kuwa uendeshaji wa shughuli za Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika zimeongezewa msukumo katika bajeti. Hata hivyo, kiasi cha bajeti kilichoongezwa ni kidogo kulingana na uzito wa majukumu makubwa waliyonayo katika kuhakikisha tija inaongezeka kwenye kilimo kwa kuboresha miundombinu ya umwagiliaji, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya hifadhi ya mazao, kuimarisha vituo vya utafiti, upatikanaji wa pembejeo, kuimarisha huduma za ugani pamoja na kuimarisha Usimamizi na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika.

Kamati imejiridhisha kuwa makadirio ya bajeti ya matumizi ya kawaida yanaendana na utekelezaji wa bajeti ya miradi maendeleo, jambo la kuzingatia ni Serikali kuiwezesha Wizara kupata fedha kwa kadri ya mahitaji ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

### 2.6.3 Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua makadirio ya jumla ya **shilingi 731,161,661,000.00** kwa ajili ya kugharimia miradi ya Maendeleo inayopangwa kutekelezwa na Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendelo ya Ushirika kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Makadirio hayo ni ongezeko la **asilimia 840.36** ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kama inavyooenekana katika **Jedwali Na. 04**.

**Jedwali Na. 4: Makadirio ya Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2021/2022**

| Na | TAASISI | MAKADIRIO KWA MWAKA 2021/2022 | MAKADIRIO KWA MWAKA 2022/2023 | ASILIMIA KATIKA ONGEZEKO |
|---|---|---|---|---|
| | WIZARA YA KILIMO | 164,748,000,000.00 | 104,158,114,000 | 63.22 |
| | TUME YA UMWAGILIAJI | 46,500,000,000.00 | 361,500,000,000.00 | 677.14 |
| | TUME YA USHIRIKA | 0.00 | 1,100,000,000.00 | 100.00 |
| **JUMLA** | | **211,248,000,000.00** | **731,161,661,000.00** | **840.36** |

***Chanzo:*** *Randama za Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa jumla unaonesha kwamba:

a) Bajeti ya Maendeleo kwa Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, Tume ya Maendeo ya Ushirika imeongezeka kwa **asilimia 840.36** tafsiri ya ongezeko hili ni kwamba idadi, thamani, na ukubwa wa miradi inayotekelezwa itaongezeka ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2021/2022 na hivyo kuongeza uzalishaji na tija kwenye kilimo.

b) Pamoja na bajeti ya Wizara ya Kilimo kuongezeka kwa **asilimia 840.36**, hata hivyo ongezeko hili halijakidhi mahitaji ya Wizara ambayo ni shilingi **Trilioni 2** kwa mwaka.

c) Kiasi cha **shilingi 751,123,280,000.00** zilizotengwa kutekeleza Bajeti ya Wizara ya kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ni sawa na **asilimia 1.83** ya bajeti ya Taifa ambao ni **shilingi 41,063,915,287,000. 00** haijakidhi matakwa ya utekelezaji wa Azimio la Maputo (2003) na Malabo (2014) ambalo linazitaka

nchi wanachama kutenga **asilimia 10** ya bajeti ya Taifa kwa ajili ya sekta ya kilimo.

d) Kwa mara ya kwanza Tume ya Maendeleo ya Ushirika imekasimiwa Bajeti ya Maendeleo ambayo itasaidia kuimarisha uwezo wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo ni wazi kuwa Wizara na Taasisi zilizo chini yake zitaongeza uwezo wa utekelezaji wa miradi ikilinganishwa na utekelezaji ulivyokuwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Ni maoni ya Kamati kuwa, utekelezaji wa miradi ya maendeleo nchini unaweza kuwa na mafanikio endapo Wizara itapewa fedha zilizoombwa kwa wakati.

**SEHEMU YA TATU**

**3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi wa Kamati, Ushauri kuhusu maombi ya fedha kwa Wizara ya Kilimo ni kama ifuatavyo:

**3.1 Wizara ya Kilimo**

(1) Kwa kuwa bajeti iliyoongezeka kwa kiasi kikubwa ni mkopo kutoka Shirika la fedha duniani (IMF), ili mkopo huo uweze kulipika, ni lazima bajeti inayoidhinishwa na Bunge itolewe kwa wakati ili kuwezesha utekelezaji wa malengo na mikakati iliyokusudiwa na urejeshwaji wa mkopo huo kwa wakati.

(2) Ili bajeti iliyoongezeka ilete tija inayokusudiwa, Rasilimali watu ni nyenzo muhimu katika kufikia malengo yaliyobainishwa, Kamati inashauri Ofisi ya Rais Managementi ya Utumishi wa Umma iwezeshe upatikanaji wa Watumishi wanaohitajika mapema iwezekanavyo na kulingana na mahitaji. Aidha, Wizara ya Kilimo ishirikishwe kuainisha kada ya Watumishi kulingana na mahitaji na mipango iliyojiwekea.

(3) Kiasi cha nyongeza ya bajeti iliyotolewa kwa mkopo wanye masharti nafuu kitatumika kujenga uzio wa mashamba ya kuzalisha mbegu ili kuzuia uvamizi wa mashamba hayo. Kamati inashauri ili kuongeza ufanisi wa fedha hizo, pesa hizo zitumike kwenye kuongeza uzalishaji. Aidha, ulinzi wa mashamba hayo ufanyike kwa kumilikisha ardhi za mashamba hayo kisheria kwa kupata hati, kupanda miti kuzunguka mashamba husika ikiwa pia ni njia ya kuhifadhi mazingira na kujenga mahusiano mazuri na wananchi wanaozunguka mashamba hayo.

(4) Wizara ya Kilimo iendelee na mikakati ya kujenga uelewa wa pamoja kwa Viongozi wa Kitaifa, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Wizara ya Fedha - Benki Kuu, Wizara ya Viwanda na Biashara, Taasisi za Kifedha na Sekta Binafsi ili Taifa liwe na uelewa wa pamoja kuhusu dhana ya kilimo ni uchumi, kilimo ni ajira

na kilimo ni maligafi ya viwanda. Ulewa wa pamoja utasaidia kutoa kipaumbele kwenye upangaji wa bajeti kwa sekta ya kilimo.

(5) Kutokana na kuendelea kupanda kwa bei ya mbolea siku hadi siku, imekuwa ni vigumu kwa wakulima kumudu gharama za mbolea, Kamati inashauri Serikali iandae Mpango Mkakati wa utoaji ruzuku kwenye mbolea ili kumpunguzia mkulima gharama za uzalishaji lakini pia kunusuru mfumuko wa bei za vyakula.

(6) Wizara ya Kilimo itumie changamoto inayoikabili dunia ya uhaba wa bidhaa za ngano na mafuta ya kula kama fursa ya kuongeza uzalishaji, uchakataji na biashara ya mazao hayo. Kwa kufanya hivyo nchi yetu itaongeza fursa ya ajira, uhakika wa soko la Afrika Mashariki lakini pia kuipungunzia Serikali gharama kubwa ya kutumia fedha za kigeni kuagiza bidhaa hizo nje ya nchi.

(7) Wizara ya Kilimo ishirikiane na Ofisi ya Rais – TAMISEMI na kuandaa Mpango kazi utakaowezesha mikopo ya Halmashauri inayotolewa kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kutumika kwenye kilimo. Mpango utakaoandaliwa uhusishe kutenga maeneo yanayofaa kwa kilimo, kuwekeza kwenye miundombinu ya umwagiliaji, kuwapatia mbegu bora na zana bora za kilimo. Hatua hizo zitasaidia kutafanikisha azma Serikali ya kuvutia wananchi wengi zaidi kujishughulisha na kilimo.

(8) Utekelezaji wa ujenzi na uboreshaji wa barabara za vijijini ushirikishe Wizara ya Kilimo, kwa kufanya hivyo kutawezesha ujenzi wa barabara hizo kutoa kipaumbele kwenye maeneo yenye uzalishaji mkubwa.

(9) Fedha na mipango itakayotumika kuimarisha miundombinu ya uzalishaji mbegu pamoja na kuzalisha mbegu bora na miche ya kisasa izingatie mahitaji ya mbegu za asili kwa kutafiti, kuzalisha na kuzifufua ili kulinda utamaduni wetu pamoja na umuhimu wa virutubisho vilivyomo kwenye mbegu za asili.

### 3.2 Tume ya Maendeleo ya Ushirika

(1) Serikali iimarishe Ushirika kwa kutenga bajeti ya kutosheleza Maafisa Ushirika kupata vitendea kazi kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, ikiwa ni pamoja na kuvisimamia kikamilifu Vyama vya Ushirika vinavyokiuka taratibu za kuongoza Vyama hivyo.

(2) Wizara iharakishe mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013, na Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya Mwaka 2002. Mapungufu ya kisheria na kisera yamepelekea baadhi ya viongozi wa Vyama vya Ushirika kutumia mwanya huo kukiuka taratibu za kuongoza Vyama vya Ushirika.

(3) Kuendelea kuchukua hatua stahiki za kuimarisha Mfumo wa Ushirika ili kuwezesha mazao yote ya kilimo kuwekewa utaratibu wa kuwa na ushirika kwa ajili ya kupata pembejeo ikiwemo mbolea, mbegu bora na viuatilifu kwa

wakati na kwa bei nafuu ili kuongeza tija na upatikanaji wa masoko ya uhakika.

### 3.3 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu Utekelezaji wa Mipango ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kamati inashauri yafuatayo: -

(v) Kwa kutumia fedha za mkopo wenye masharti nafuu kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF), Wizara imepanga Kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika skimu mpya 25 zenye jumla ya hekta 53,234. Kamati inashauri kabla ya kuanza ujenzi wa skimu mpya, fedha hizo zitumike kufanya matengenezo ya skimu mbalimbali za umwagiliaji ambazo kwa muda mrefu zimekuwa hazifanyi vizuri kutokana na ukosefu wa bajeti ya kuboresha skimu hizo.

(vi) Kuweka mikakati thabiti ya ukusanyaji wa ada za umwagiliaji kwa lengo la kuwezesha ujenzi wa skimu nyingi zaidi kwenye maeneo mbalimbali nchini. Aidha, ukusanyaji wa ada hizo usimamiwe kikamilifu.

(vii) Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji utekelezwe na wakandarasi kutoka sekta binafsi ili iwe rahisi kuwawajibisha endapo kutatokea itirafu ya aina yoyote. Kwa msingi huo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itabaki kuwa msimamizi na mkaguzi wa ujenzi wa miundombinu na miradi inayotekelezwa.
(viii) Ujenzi wa skimu mpya za umwagiliaji uzingatie maeneo yanoyafaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Aidha, ili miradi hiyo iwe endelevu ni vyema ikashirikisha Halmashauri husika na Wabunge wa maeneo miradi inapotekelewa.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Maelezo ya Kuhitimisha

**Mheshimiwa Spika,** kama inavyofahamika, Maendeleo katika Sekta ya Kilimo ni muhimu hasa katika kukuza uchumi wa Taifa na kuleta msukumo kwenye ukuaji wa sekta ya viwanda. Ukuaji wa sekta hii una umuhimu mkubwa katika kuzalisha chakula cha kutosha ili kuhakikisha uwepo wa usalama wa chakula na lishe kwa wananchi wakati wote. Sekta ya kilimo inachangia takribani asilimia 29.1 ya pato la Taifa, asilimia 65.5 ya ajira, asilimia 65 ya malighafi inayotumika katika sekta ya viwanda na asilimia 30 ya pato la bidhaa zinazouzwa nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa msingi huo, Wizara ya Kilimo ni mwezeshaji na mratibu muhimu wa kufanikisha utekelezaji wa Mipango mbalimbali ikiwemo Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo awamu ya Pili na utekelezaji wa Malengo Endelevu ya Milenia (SGDs) hususani lengo namba 1 linalohusu kupunguza umaskini uliokithiti na lengo namba 2 linalohusu kutokomeza tatizo la utapiamlo kwa kuimarisha lishe bora.

**4.2 Shukurani**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya Wizara ya Kilimo. Kutokana na umuhimu wao natamani kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa kuwataja majina yao. Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*). Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Dkt. Christine G. Ishengoma, Mb | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Athuman A. Maige, Mb | - | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Yustino Job Ndugai, Mb | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Dkt. Balozi Bashiru Ally Kakurwa, Mb | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Prof. Sospeter M. Muhongo, Mb | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Deo Kasenyenda Sanga, Mb | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Christopher Ole Sendeka, Mb | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Prof. Partrick A. Ndakidemi, Mb | - | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Charles John Mwijage, Mb | - | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Munde Tambwe Abdallah, Mb | - | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Livingstone Joseph Lusinde, Mb | - | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Dkt. Rita Enespher Kabati, Mb | - | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb | - | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb | - | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb | - | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Janejelly James Ntate, Mb | - | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Mrisho Mashaka Gambo, Mb | - | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Tumaini Bryceson Magessa, Mb | - | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Jackson Gidion Kiswaga, Mb | - | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Benaya Liuka Kapinga, Mb | - | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Furaha Ntego Matondo, Mb | - | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Yahya Ali Khamis, Mb | - | Mjumbe |
| 23. | Mhe. Mohamed Suleiman Omar, Mb | - | Mjumbe |
| 24. | Mhe. Michael Mwita Kembaki, Mb | - | Mjumbe |
| 25. | Mhe. Yustina Arcadius Rahhi, Mb | - | Mjumbe |
| 26. | Mhe. Prof. Shukrani Elias Manya | - | Mjumbe |
| 27. | Mhe. Emmanuel Peter Cherehani, Mb | - | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuona umuhimu wa sekta ya kilimo. Kwa kipindi kifupi cha uongozi wake tumeshuhudia kasi kubwa ya uongezaji bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa lengo la kuongeza tija kwenye kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kumshukuru Waziri Kilimo, Mhe. Hussein Bashe (Mb) kwa ushirikiano mkubwa kwa Kamati ambao umechangia kwa sehemu kubwa kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake. Utendaji wake

na Naibu Waziri wake, Mhe. Anthony Mavunde (Mb) umedhihirisha jinsi vijana walivyo hazina kubwa kwa ustawi na maendeleo ya Taifa letu.
Nawashukuru pia watendaji wote wa Wizara ya Kilimo na Taasisi zilizo chini ya Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu. Andrew Masawe, akisaidiana na Naibu Katibu Mkuu, Prof. Siza Tumbo kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati. Aidha, nampogeza Ndg. Gerald Mweli kwa kuhamishiwa Wizara ya Kilimo kama Naibu Katibu Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Bunge Ndg. Dickson Bisile, Makatibu wa Kamati Ndg. Rachel Nyega na Ndg. Eunice Shirima, wakisaidiwa na Ndg. Waziri Kizingiti, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa Taarifa hii.
Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Christine Gabriel Ishengoma (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI**

17 MEI, 2022

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kapinga Benaya kwa taarifa ya Kamati/ Naona unakunywa na maji kidogo, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tunaanza uchangiaji, mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, akifuatiwa na Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga mchangiaji wa tatu atakuwa ni Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda. *(Makofi)*

**MHE. ANNE K. MALECELA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kukushukuru kwa kunifanya kuwa mchangiaji wa kwanza. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa uhai, namshukuru Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali ya Chama Cha Mapinduzi Awamu ya Sita, nampongeza Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan, anakwenda vizuri sana na wananchi wa Jimbo la Same Mashariki wameleta salamu kwamba azipokee, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe na Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze kuchangia, na leo ninaomba kuchangia kwa unyenyekevu mkubwa sana. Mheshimiwa Charles Kimei aliniuliza kwanini unachangia tangawizi kila siku, ninachangia tangawizi kila siku kwasababu kubwa moja, wananchi wangu wa Jimbo la Same Mashariki takribani asilimia 80 mpaka 85 wanalima zao la Tangawizi. Watanishangaa

nikija nikaanza kuchangia kahawa, cocoa na miwa kwasababu wao wanalima zao la tangawizi, hivyo ni lazima nilizungumzie na kuisihi Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tulianza kulima Tangawizi mwaka 1988. Zao hili lililetwa na mzee mmoja anaitwa Mzee Kilango Chikila. Hatujui alilitoa wapi, lakini alilileta mwaka 1988. Tukaanza kulilima zao la tangawizi kwenye miinuko mikubwa ya mita 800 hadi 1500. Tangawizi iliyo bora ni ile inayolimwa kwenye miinuko mikubwa, na Jimbo la Same Mashariki ni jimbo la milima na milima hii ya tarafa mbili yote inalima tangawizi kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumelima tangawizi kwa miaka 34 sasa. Ninaongea kwa masikitiko kidogo lakini kwa unyenyekevu. Tumelima kwa miaka 34 sisi wenyewe bila kupata msaada kutoka Serikali Kuu; na kwa wakulima kama mnalima wenyewe bila ya kuboreshewa miundombinu ya kilimo ni lazima mtapata mazao hafifu. Tangu mwaka 2000 mimi nipo hapa Bungeni ninaongelea hili zao, lakini kwa uzito niliongea kuanzia mwaka 2005 nilipochaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninaiomba Serikali; na niongee kwa lugha ya unyenyekevu, lakini baadaye kama itapanda mnisamehe sana. Wananchi hawa wanalima hili zao wenyewe; nikiwa nina maana kwamba zao la tangawizi linatumia maji mengi sana, kwa hiyo tuna mirefeji lakini ile mifereji tumeitumia kwa miaka 34. Narudia tena, Serikali hatujapata msaada kutoka kwenu. Ni lazima Serikali mjue kwamba ninyi mnapaswa kuangalia miundombinu ya kilimo kwaajili ya wakulima. Hili ni hitaji la kikatiba la wananchi. Serikali ni lazima muwasaidie wakulima kwenye miundombinu ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka 34 hadi sasa ninapoongea tunategemea kulima tani 25,000 tu, lakini ujue tunavuna tani 25,000 tukiwa hatuna msaada wa Serikali. Iwapo Serikali mtafanya kazi yetu ya kikatiba ya kuboresha miundombinu ya kilimo ya Jimbo la Same Mashariki tunategemea tutavuna takribani tani 50,000. Juzi nilikwenda jimboni kufanya ziara nikaona nimletee Mheshimiwa Waziri picha hizi. Nikimaliza kuzungumza nitaomba hawa vijana waje wachukue wampelekee. Nimepiga picha miundombinu ya kilimo ya jimbo langu ambayo wananchi wanafanya wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa hii sio haki. Wananchi wanatengeneza miundombinu ya kilimo wenyewe ni kitu kigumu sana kwenye miinuko mikubwa ile ambayo Mheshimiwa Waziri wewe ulikuja, ulikuja kwenye ile miinuko. Na ninakuomba radhi, nitasema, pole sana kwa kuwa ulitapika sana kwenye ile miinuko. Ni kweli, yupo mwenyewe ameketi pale. Ile miinuko ni migumu lakini wananchi wale wanalima tangawizi kule, hawapati msaada wa Serikali, miundombinu ya kilimo yote hii wanatengeneza wenyewe. Mheshimiwa nitaomba upewe baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumeanza kuchakata tangawizi sisi. Tumepata kiwanda ambacho sisi wananchi wa kule tulikijenga wenyewe. Hata hivyo ninaomba niipongeze sana *PSSSF* kwasababu ilikuja kuwa mbia, na sasa tumejenga kiwanda cha tangawizi ambacho ni cha kwanza katika Afrika Mashariki. Tangawizi tunayovuna ni hii hapa, tangawizi tunayochakata ni hii hapa, tangawizi ya unga tunayotengeneza ni hii hapa.

*(Hapa Mhe. Anne K. Malecela alionesha aina ya tangawizi zinazolimwa, zilivyochakatwa na zao la tangawizi katika mfumo wa unga)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Kwa sababu kile ni kiwanda hatuwezi kuchakata tangawizi bila *TBS* kuja. *TBS* wameangalia ubora wa tangawizi ya Same Mashariki. Mtaniwia radhi, mkiangalia vizuri mtaona ni tofauti na tangawizi nyingine zozote hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumze kitu kimoja, kwa siku moja ya masaa 24 kiwanda kile kinachakata tani 10, sijui mmenielewa! Tani 10. Sasa sisi wenyewe kwa mwaka tunalima tani 25,000, siyo tangawizi ya kutosha kwenye kile kiwanda. Sijui Serikali mmenielewa hapa? Kwa siku moja tunachakata tani 10, kwa mwaka mmoja tunavuna tani 25,000 ina maana kile kiwanda hakitapata tangawizi ya kutosha. Serikali ninaomba kwa unyenyekevu mkubwa nendeni mkaangalie miundombinu ya killimo na muiboreshe ili wananchi wale wavuna tangawizi kwa wingi, wawe na mazao ambayo yatakifanya kile kiwanda kipate malighafi ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu angalieni Nigeri kwanini…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela. Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MHE. ANNE K. MALECELA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, niwie radhi utakuwa. Angalieni Nigeria, Nigeria ina zao la tangawizi na ni zao la pili kuchangia kwenye *GDP* ya nchi asilimia 23. Kwa hiyo hili zao kama Serikali mtafanya kile mnachohitajika kufanya kwamba mkaboreshe miundombinu ya kilimo wananchi hawa watalima tangawizi kwa wingi. Mimi ninaomba hilo mliangalie vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema naongea kwa unyenyekevu lakini Mheshimiwa Bashe hapana niongee kwa ukali sasa hivi. Kwanini mnawafanyia wale wananchi hivi? Mnategemea wananchi walime wenyewe, wavune kidogo waishi vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Bashe sitaunga mkono hoja yako hata kidogo; na ninatangaza kuondoa shilingi mpaka utoe jibu ambalo litanifurahisha, ama sivyo leo hotuba yako ya kilimo itakuwa ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme ukweli; kwanini Nigeria wao wanavuna tangaziwi nyingi kiasi kile? Ni kwasababu Serikali ya Nigeria imesimama imara kwenda kushika wananchi wake wanaolima tangawizi, na ndiyo maana Tangawizi inakuwa mchangiaji wa pili wa *GDP* ya nchi ile kwa asilimia 23. Mimi naomba, nafikiri sina mengi ya kuzungumza, hoja yangu kubwa wewe kama Serikali uje Same Mashariki ukaisimamie miundombinu ya kilimo cha tangawizi. Bila ya hivyo mimi na wewe hatutaelewena, sitaunga mkono hoja nitangoja mwisho. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimwita Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, wakati huo Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, anajiandaa. *(Makofi)*

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kusimama hapa. Lingine kwa kweli leo ni siku ambayo nina amani sana na furaha kubwa, kwa sababu naichangia Wizara ambayo inaonesha kwamba watu wapo *serious. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sisi ambao ni Wabunge Mawaziri wote hawa tunawaona, tunajua kila mtu utendaji wake ulivyo. Vipo vitu ambavyo kuna Waziri anaongea, hata maswali wananchi wanatutuma, tunakuja hapa tunauliza, Waziri akidanganya tunajua, Waziri akifanya siasa tunajua na Mawaziri ambao wapo *serious* pia tunajua. Wizara hii ya Kilimo ni Wizara ambayo ipo na watu *serious* kupita mfano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina Wizara zangu chache; Wizara ya Kilimo, Wizara ya Madini, nyingine siwezi kuzisema leo lakini hizo naamini kwamba zipo na watu *serious* na lazima niwapongeze watu hawa kwa sababu kazi kubwa na hali halisi ya maisha ya wananchi wetu inajulikana. Wananchi wetu wana shida sana kule, vipo vitu vingine tukikaa kupongezana na kusifiana sana mambo kule yatakuwa hayaendi. Mwaka 2025 itafika wakati sasa tunakaa tunaanza kutafutana, tunabembeleza, tunapiga magoti tunaonekana kwenye magazeti haipendezi. Kwa hiyo, kwa Mawaziri ambao wanafanya kazi vya kutosha na kwa kiwango cha juu, ni lazima tuwapongeze. *(Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy Mayenga, kuna taarifa kutoka Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nakubaliana na dada yangu Lucy Mayenga kwamba ni kweli mawaziri hawa vijana wanafanya kazi, lakini jukumu letu kama Bunge ni kuhakikisha Wizara ya Fedha tunaibana ili wawapelekee hawa Mawaziri fedha wakabadilishe maisha ya watanzania ambao asilimia 80 ni wakulima. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mayenga unapokea taarifa?

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Taarifa hiyo si mbaya, naipongeza kwa sababu pesa ndiyo kila kitu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Rais wetu, kwa kweli huyu mama anafanya kazi kubwa sana, nasema hivi kwa sababu hata kwenye Wizara hii tumeona kiwango cha pesa bajeti ya Wizara hii kwa mara ya kwanza imefika shilingi bilioni 751 haijapata kutokea. Kwanza ameonesha kuwathamini sana wakulima, lakini amewaheshimisha…*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mayenga imefika bilioni 700, bilioni weka takwimu vizuri.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema bilioni 751.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sawa. Imetoka bilioni 200 mpaka bilioni 751, lakini Mheshimiwa Rais pamoja na Wizara hii wameweza kupandisha, yapo maeneo ambayo tunajua kabisa kwamba ukiyagusa, kama tunavyojua kwamba kilimo kinamgusa mwananchi kwa asilimia 100. Maeneo ya utafiti, maeneo ya hawa ndugu zetu Maafisa Ugani, maeneo ya maendeleo yote katika Sekta ya Elimu yamepandishwa kwa kiwango kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitolea mfano kwenye utafiti; kutoka bilioni 7.0 mpaka bilioni 11.6; kwenye huduma za ugani bajeti imepanda kutoka milioni 603 mpaka bilioni 11.5; kwenye umwagiliaji kutoka bilioni 17 mpaka bilioni 51; ni mabadiliko makubwa sana na kwa kweli kwenye hili tunampongeza sana Mheshimiwa Rais, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii Naibu na Watendaji wote. Kama ingekuwa kuna uwezo Waziri mmoja na watendaji wake na hii timu ya Wizara ya Kilimo kuhudumia Wizara mbili, kuna Wizara ningependekeza kama iende huko pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimpongeze mama yangu Mwenyekiti wa Kamati hii. Ni mama ambaye amekuwa anafanya ziara kwa vitendo na kwa kweli Kamati hii imekuwa ikifanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo matamko mengi sana ya historia ya kilimo katika nchi yetu, imeanza kwa mambo mengi sana. Awamu ya Kwanza naya Nne wao walijikita kwenye masuala mazima ya uzalishaji; Awamu ya Pili na Tatu wao walijikita kwenye Muundo wa Taasisi pamoja na mifumo mizima ya kilimo; Awamu ya Tano iliyopita ilijikita kwenye kuboresha masuala mazima ya kuongeza thamani ya mazao, uzalishaji lakini na pia

vilevile kuweka miundombinu bora kwa ajili ya kusaidia kilimo chetu katika mazao ambayo yanapatikana yaweze kusafirishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo ambayo nataka niyazungumzie, tunazungumza kwamba kwenye sekta hii, zipo pesa nyingi sana. Wizara hii Mheshimiwa Waziri kaka yangu Bashe amepewa fedha nyingi sana na fedha hizi naomba awe mkali sana. Nasema hivi kwa sababu moja kati ya tatizo kubwa sana ambalo limekuwa likitokea hapa nchini kwetu, ni kwamba bado baadhi ya watu ni kama wanataka ku-*test test* mitambo hivi, bado hawaamini kwamba kula fedha ya Serikali ni kosa na unaweza kuchukuliwa hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali au Wizara hii ijitahidi sana kusimamia pesa hizi kwa sababu kule kwa wananchi kilimo ni kinachukua asilimia 70 ya Watanzania. Kwa hiyo, bila fedha hizi kusimamiwa ipasavyo maendeleo na yale matokeo ambayo tunahitaji hatutayapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kuzungumzia, kuna Miradi ya Umwagiliaji katika Wilaya yangu ya Kishapu, ipo Miradi ya Umwagiliaji katika Kata za Mwadui, Lohumbo Itilima na Talaga, kuna skimu za umwagiliaji. Naomba Mheshimiwa Waziri kwa unyenyekevu mkubwa, ikiwezekana tuweze kupata fedha pale. Katika skimu ya Umwagiliaji ya *NIDA* ambayo ilikuja mwaka 2020, namshukuru sana Wazii alikuja pale Shinyanga Vijijini baada ya kelele nyingi sana za kaka yangu Mheshimiwa Ahmed, Mbunge wa Jimbo, alikuja akasikiliza shida zetu na akatuelewa na nimpongeze na nimshukuru kwamba ametupatia fedha kwa ajili ya *skimu* hiyo ya umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia atusaidie skimu ya umwagiliaji ya kwenye Kata Uhendele ambayo ipo kwenye Manispaa ya Kahama Mjini. Kuna Mheshimiwa Diwani wetu pale anaitwa Justin Sita amekuwa akipiga kelele kila mara kwenye kila kikao kwamba mradi huu uweze kupata fedha, naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie. Miradi hii endapo kama itafanikiwa, itasaidia akinamama. Watu wanategemea miradi hii ikifanikiwa maji yale yaweze kulisha mifugo pamoja na akinamama waweze kupata maji kwa ajili ya matumizi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho; naomba kusema hivi, naomba tumpe Mheshimiwa Rais wetu muda. Mheshimiwa Rais wetu ameingia katika kipindi ambacho kina changamoto nyingi sana, endapo sisi wanasiasa tutakuwa tunakaa katika kila kitu kwa kuangalia dosari, kuangalia hapa amefanya hivi, kwa kuangalia kukosoa, hatuwezi kumpa moyo Mheshimiwa Rais wetu. Tumpe muda tukae, kama ambavyo tulikuwa tumeanza mwezi Januari, Februari, Machi mpaka Aprili maneno yalikuwa mengi mengi, lakini juzi amekuja amefanya jambo la maana, maneno yamekuwa mengi ndivyo Watanzania walivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kumpa moyo Mheshimiwa Rais, afanye kazi, ameingia kipindi kigumu, kipindi ambacho kina matatizo mengi, matatizo ya vita ya Urusi, UVIKO na mengine mengi, lakini naomba nimpe moyo, tupo pamoja naye hata kama kuna wanasiasa ambao tunawasikia wanaongeaongea vitu ambavyo havieleweki, sisi tupo pamoja naye na naomba wanasiasa hao washindwe na walegee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga.

Nilimwita Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, wakati huo wafuatao wanajiandaa: Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, Mheshimiwa Charles John Paul Mwijage na Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii. Kama walivyosema wenzangu waliotangulia bado nampongeza Mheshimiwa Waziri Bashe, kwa kuwa amekuwa mwepesi, tunapompelekea matatizo yetu kutusaidia hususani sisi watu wa Nyanda za Juu Kusini ambapo ndiyo tunalima sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imezungumza habari ya pembejeo na hasa tukienda kwenye eneo la mbolea; kwa muda mrefu imekuwa bei pamoja na kwamba wameizungumzia, wananchi wamepata shida sana, sana katika ulimaji msimu huu wa kilimo. Tunafahamu kabisa na Mheshimiwa Waziri amesema kwamba dunia imepandisha bei, lakini mwisho wa siku Watanzania wana Serikali yao ambayo wanaitegemea na tunajua kwamba kilimo ndiyo uti wa mgongo kama ambavyo tulikuwa tukisema miaka mingi, watanzania hao wanahitaji chakula. Sasa Serikali kuchelewa kutoa maamuzi ya kuwasaidia wakulima na hasa kuweka ruzuku kwenye mbolea, nafikiri wamefanya kosa kubwa sana la kutufanya tusiwe na chakula kipindi kinachokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia mbolea kupanda bei, *DAP* ilikuwa shilingi 66,000; *Urea* ilikuwa Sh.53,000, mbolea hizi zilifika mpaka bei ya shilingi 150,000 kwa mfuko wa kilo 50. Sasa kuna haja ya Mheshimiwa Waziri kuona matatizo yanapotokea kuwa na *first truck* ya kuamua kuweza kusaidia Watanzania. Kwa kukaa kimya mpaka leo bajeti imekuja na Waziri anatamka na hatujui utekelezaji wake utachukua muda gani, kwa kweli hatujawatendea haki wakulima wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amezungumza kwenye hotuba na naweza kumwamini kwa sababu naamini anaweza kufanya kazi …

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa kutoka wapi?

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo hapa.

**MWENYEKITI:** Sawa, taarifa.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kumpa mzungumzaji taarifa kwamba, pamoja na kwamba mbolea ilikuwa bei ya juu, lakini bado upatikanaji wake ulikuwa ni changamoto kwa wakulima wetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakagenda unaipokea taarifa?

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea. Tunaamini kwa uchapa kazi wa Mheshimiwa Bashe, bajeti hii ameipata moja kwa moja akiwa Waziri, kwa hiyo, alichokisema hapo kwamba anaenda kuhakikisha mbolea inashuka bei, lakini si tu, hivyo inapatikana kwa wakati ili wakulima wasiingie kwenye matatizo. Tunaomba Mheshimiwa Waziri alitekeleze hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la chai. Zao la chai ni zao kubwa sana katika nchi yetu ya Tanzania. Mikoa inayolima chai au sehemu zinazolima chai, Lushoto, ukienda Muheza, Njombe na Rungwe kwetu tunalima sana chai. Nimekuwa nikisema mara nyingi hapa Bungeni na nikiongea na Mheshimiwa Bashe juu ya zao hili. Zao hili kwa ripoti ya Bodi ya Chai yenyewe, inasema uzalishaji wa chai umepungua kwa asilimia nne katika mwaka uliopita. Kwa nini zao hili linapungua kwa wakulima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao hii linapungua kwa sababu bei yake haipandi na bahati mbaya sana Bodi ya Chai kama wapo hapa wananisikiliza wanapendelea maeneo kwa maeneo. Nchi ni moja lakini chai inauzwa bei tofauti tofauti. Ukienda Rungwe chai haizidi Sh.230, lakini ukienda Njombe unakuta chai kilo moja ni Sh.500. Nchi moja, wakulima hao hao, Rais wao mmoja, lakini bado tumewagawa kwenye bei. Sijaelewa ni vigezo gani Bodi ya Chai inatumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, Bodi ya Chai haisimamii haki ya wakulima, kuna makampuni yanayonunua chai mbichi, lakini wakulima kwa muda mrefu hawalipwi madeni yao bila sababu yoyote. Sisi tunaamini Bodi ya Chai ndiyo msimamizi wa wakulima wasiokuwa na sauti, lakini bodi hii imeungana na wanunuzi, imeungana na makampuni na kuwaacha wakulima wakihangaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la pembejeo kwa wakulima wa chai. Makampuni haya yanatoa mikopo ya mbolea kwa bei ambayo si

nzuri. Mtu anapewa mfuko wa mbolea kwa bei iliyo juu, akija kuuza chai anakuja kukatwa, mwisho wa siku mkulima anabaki na fedha ndogo sana. Naomba Mheshimiwa Waziri alisimamie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii chai nimeizungumzia muda mrefu na naomba sana, sana kwa maelezo ya *CAG,* ukaguzi uliofanyika mwaka huu Machi, 2022, makampuni sitaki kuyataja hapa, yamekopa wakulima toka 2018 mpaka leo hii hawajawalipa madeni yao. Naamini Mheshimiwa Bashe anayamudu makampuni haya, naomba ayasimamie ili wawalipe wakulima stahiki zao, kwa sababu wamefanya kazi kwa jasho na sasa wanahitaji kutumia fedha zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie Benki ya Kilimo; benki hii ipo kwa ajili ya wakulima, lakini kwa mfano, kwa wakulima wadogo wadogo, kuna mfuko ambao ulitolewa pesa zaidi ya bilioni 7.0 kwa ajili ya kuwakopesha wakulima wadogo wadogo, lakini pesa hii kwa mujibu wa *CAG* kwenye ripoti ya Machi, 2022, walichukua pesa hiyo wakabadilisha matumizi badala ya kuwakopesha wakulima wadogo wadogo. Pesa hiyo ikaenda kufanya kazi nyingine bila kuwasaidia hao wanaohitaji msaada wa kukopa. Naomba hilo pia Mheshimiwa Waziri akija kuhitimisha anipe maelezo tuweze kuelewa ilikuwaje, kwa sababu mwisho wa siku wakulima wakubwa wanafaidika na walio wengi ambao ni wadogo hawapati chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwamba Benki ya Kilimo lengo lake ni kusaidia Watanzania, tunaomba isimamie lile kusudio ambalo imepewa na Serikali. Pia kuna Mfuko wa Pembejeo, Mfuko huu unaenda kufilisika kwa sababu zaidi ya bilioni 27 ambazo zilitolewa, bilioni 20 zimekopwa na hazijarudi. Sasa tunawezaje kusaidia Watanzania kama kuna fedha zinatolewa halafu hazirudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Mheshimiwa Waziri ametoa kwenye hotuba yake akisema, anataka watu wanaouza pembejeo mbolea waungane. Naamini katika mipango mizuri aliyonayo Mheshimiwa Waziri au iliyonayo Serikali yake, lakini mwisho wa siku utekelezaji haupo. Kupanga ni kitu kingine na kutekeleza ni kitu kingine. Kwa hiyo, Mfuko huu zaidi ya asilimia 72 pesa bado ziko mikononi mwa watu, hazijarudi wakati sisi tunategemea pesa hizi ziweze kusaidia wale wengine ambao bado hawajakopa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalima parachichi kama alivyosema Mheshimiwa Waziri na watu wamejitokeza kulima parachichi kweli kweli, lakini kwenye *export* ya parachichi tunashindwa kujenga kiwanda cha kutengeneza *box* la kuhifadhia parachichi mpaka twende Kenya tukanunue. Nafikiri hatujitendei haki kama Watanzania kwa sababu kujenga kiwanda cha kutengeneza *box* hapa, tutatoa ajira kwa vijana na tutapunguza gharama ya k*u-export* parachichi, badala ya kwenda kuagiza Kenya, *order*

inachukua mpaka siku nne mpaka siku saba, mtu aipate kutoka Kenya, ije Rungwe iende Makete, tunakuwa hatuwatendei haki Wtanzania. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa nilikuongeza dakika moja. Tunakushukuru sana nafikiri Mheshimiwa Waziri pia suala la parachichi amelisikia na hata wananchi wa Mufindi nao wanafuatilia kwa karibu sana kuhusu jambo hilo.

Nilimwita Mheshimiwa Boniventure Destery Kiswaga, wakati huo Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Butondo pamoja na Mheshimiwa Kunti wanajiandaa.

**MHE. BONIVENTURE D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu kwa namna ya pekee ambavyo wamelichukulia suala la Wizara ya Kilimo kwa mtazamo si msimamo. Nchi zote duniani viongozi ili tupate mabadiliko lazima tuwe na mitazamo kuliko kuwa na misimamo. Kwa hiyo, hili Mheshimiwa Waziri ameliweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo mazao matano ya kimkakati ambayo Waziri Mkuu aliyasimamia ili kuondokana na adha mbalimbali ambazo wananchi wetu wanazipata. Leo ukienda kule mitaani mfumuko wa bei wanalalamikia mafuta ya kula, mfumuko wa bei wanalalamikia sabuni. Sasa sisi tunayo mazao ambayo yanaweza kumaliza tatizo hili. Zao la kwanza; zao la michikikichi hili linatoa mafuta pamoja na sabuni. Kama tutalisimamia na kuliimarisha tutaondokana na tatizo hili kubwa ambalo wananchi wetu wanaendelea kuwa nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la pamba pamoja na zao la alizeti, hizi zote ni mbegu ambazo zinatoa mafuta ambayo wakulima wetu na wananchi wanaweza kupata mahitaji muhimu zaidi. Zao hili la pamba na alizeti ni mazao ambayo yanalimwa kila mwaka, ni mazao ambayo yanahitaji mvua ya kutosha. Nipo kule Magu nimeona mazao ya pamba pamoja na alizeti ambavyo yanakabiliwa na ukame wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewahi kutoa hapa mchango kwamba tunayo mabonde, tunayo maziwa, tunayo mito, tutumie kwa ajili ya umwagiliaji, hapa ndipo ambapo wawekezaji ambao wanatafutwa na Wizara mbalimbali kuja kuwekeza hapa Tanzania, waje wawekeze miundombinu ya umwagaliaji ili wananchi wetu waweze kulima, waweze hata kuchangia kulipa hiyo miundombinu. Tukifanya hivyo, tutaondokana na adha na tutazalisha mazao ya kutosha kuhakikisha kwamba tunapata mafuta na sabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba hivi sayansi imegota kutengeneza mbegu ya zao la pamba ambayo inaweza kuwa ni mti? Ukilimwa leo unapaliliwa miaka mitano ili wananchi wasiwe wanalima kila mwaka ili tuwe na uhakika wa kuvuna miaka yote. Kwa sababu wananchi wetu wanahangaika sana kila mwaka kulima zao hili. Hivi sayansi imegota ndugu zangu? Tuone utafiti ambao unaoweza kusaidia ili tuweze kuwasaidia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninampongeza sana Mkurugenzi wa Bodi ya Pamba na Wataalam wake kwa kusimamia zao hili muhimu. Ninaomba, wananachi wamenituma mbegu za pamba ziwe zinakwenda mwezi wa Septemba. Maana wanapolima mwezi wa Oktoba na wa Novemba haya ni mazao ambayo sasa yanaonekana hata wadudu hawapati shida kwenye kupulizia. Kwa hiyo, ninaomba sana mbegu za pamba ziweze kwenda mwezi wa Septemba. *(Makofi)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa. Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Tabasam.

**T A A R I F A**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mchangiaji kwamba suala la kugawa mbegu za pamba liendane na dawa za pamba na mbolea wakati huo huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiswaga unapokea taarifa?

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea naunga mkono. Kwa sababu ardhi yetu kule Kanda ya Ziwa imechoka. Nampongeza Waziri hapa amesema hatafanya kazi nyingine bora mbolea iende kwa wakulima. Tatizo kubwa tulilonalo sisi kule, mvua yetu ni ya wastani na wananchi wetu wanapata taabu kutumia mbolea hii. Wanataka mbolea ya samadi au mbolea ambayo inaweza kuendana na hali ya hewa kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa ndipo utafiti sasa unatakiwa utumike kwa hali ya juu sana. Hili nakwenda na kwenye mbegu, nimesikia hapa Mheshimiwa Waziri amesema kwamba mbegu za asili, mbegu za mahindi, mbegu za alizeti, mbegu za pamba za asili zitaanza kutumika. Nchi ikikosa mbegu za asili ni hatari. Kwa hiyo, nakupongeza sana kwa sababu vituo vyetu vya utafiti vimeanza kuizalisha mbegu hii na kuwa nyingi. Mbegu hii ndiyo ambayo inavumilia magonjwa mbalimbali ambayo yanakuja kutuathiri Watanzania na kutuondolea kabisa tija ya mazao. Kwa sababu tatizo tunalohangaika nalo hapa ni tija. Mazao tunazalisha kidogo kwa sababu ya wadudu kuwa wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho tusijifungie, dunia imekwisha kubadilika. Kule duniani nchi za wenzetu zilizoendelea wana kilimo cha aina mbalimbali ambacho kinasaidia. Kwa mfano, kuna mbegu za mahindi ambazo zinaweza kutoa mafuta ya kula na mafuta mengine. Hebu tutafiti, tuone namna ambavyo tunaweza kulifanya Taifa likawa na mazao mbadala mchanganyiko ambayo yanaweza kusaidia. Hata maua pia, kuna maua yanatoa mafuta halafu hayo hayo majani yanakwenda kulisha mifugo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri umeleta mfumo mpya, watu wako leo wanavaa sare za kilimo, tuone sasa kwamba wanamfikia mkulima na kwa sababu umeamua jambo hili na sisi tunakuunga mkono. Wewe bado ni kijana, wewe bado una nia njema, wewe bado una mtazamo, tunauhakika kilimo chetu kinakwenda kubadilika. Tuombe wataalam wako wakusaidie, kama hawatakusaidia walete mbele ya Bunge tuweze kukusaidia hao ambao hawawezi kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga. Nilimwita Mheshimiwa Charles John Paul Mwijage aweze kuchangia.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi ni Mjumbe wa Kamati lakini ni muumini wa sekta za kiuzalishaji. Naogopa nisije nikasahau, naomba kuunga mkono taarifa ya Kamati pia ninaunga mkono yote taarifa ya mtumishi, mimi naiita bajeti ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitazungumza mambo matatu kwa sababu tumezungumza sana suala hili mwaka jana na tumelichakata kwenye Kamati. Moja nitazungumza kuhusu umuhimu wa kilimo. Suala la pili nitazungumza mtazamo wa Serikali ya Awamu ya Sita kwenye sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilipokuwa mdogo, nilipoacha ziwa la Mama nilikwenda kulelewa na Bibi yangu aliitwa Zuhura Teshasha. Mama yangu alinipenda sana na watu wengine walikuwa wananiletea zawadi. Pamoja na udogo wangu nilikuwa na uwezo wa kutambua zawadi ya Mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zawadi ya Mama ingekuja ningesema hiyo zawadi ya mama. Napenda niwaambie, kitendo cha kutoa bajeti shilingi bilioni 294 kwenda kwenye shilingi bilioni 751 hiyo ni zawadi ya Mama. Nimemsikia mtumishi na wewe mtumishi hii siyo ya kwako umetumwa. Hii ni zawadi ya Mama, anasema atawatafuta vijana, atawapa heka tano au heka 10 hiyo siyo ya kwako, wewe ni mtumishi hiyo ni zawadi ya Mama. Wale ambao siyo watumishi wa Mama anachukua watu 10 anawapa heka mbili, huyo siyo mtumishi wa Mama. Mtumishi wa Mama ni kama wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumza kitu kingine. Hii ni bajeti ya Taifa, ile ya TAMISEMI ilikuwa ni bajeti ya wananchi, hii ni bajeti ya Taifa. Nizungumze suala jingine nikipata muda nitawaambia *change of mind, working by targets.* Nimemsikia mtumishi kwamba sisi tubadilishe malengo, sikiliza bajeti yake na ninyi Watanzania mnasikiliza, anaweka malengo kwamba ifikapo mwaka fulani sisi tuuze kiasi fulani. Kiburi cha Ukraine anauza nje Dola Bilioni 64, ndiyo kiburi cha Ukraine na angalia anauza nini Ukraine, anauza mazao ambayo na sisi tunaweza kulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine nitakalozungumzia ni suala la uchumi jumuishi. Ziko *block farming* 110 anasema mtumishi na hii umetumwa na mama nina taarifa. Anasema yeye mtumishi, *block farming* 110 atatengeneza *block farming* 10,000 kufikia 2025. Angalizo, hakikisha na Mkuu wa Mkoa wa Kagera unamwambia akutengee hekta 50,000 na vijana wa Kagera waweze kupata ardhi na mimi nitapambana na uongozi wa Kagera kuanzia Kijiji, iwe Wilaya lazima watoe ardhi vijana walime. Siwezi kukubali, siwezi kukubali wananchi wangu kutengewa heka mbili, lazima watengewe heka tano, heka 10, heka 20. Naanza kuchangia. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma gazeti la *Business Insider, Business Insider* wanasema sababu tano, nazungumza umuhimu wa kilimo. Wanasema umasikini wa Afrika unatokana na sababu tano na sababu mbili ziko kilimo, lakini sababu mbili za kilimo zinaweza kuondoa umasikini kwa asilimia 70 tukizi-*address*. Mheshimiwa Waziri amezungumza anaweza kuondoa umaskini kwa asilimia 50 kama Mama atampa zawadi na sina wasiwasi. Sina wasiwasi zawadi itakuja, Shilingi Trilioni Mbili zitakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya sababu inayotajwa ni *tariff berrier* na *non-tariff berrier.* Wale wenye ukwasi mkubwa, mazao yetu tunayolima wanayawekea kodi kubwa na wanayawekea masharti yasiyokuwa ya kikodi. Lakini watu wale wenye ukwasi mkubwa, kitu ambacho wanacho kingine wana ruzuku sana mazao yao yanayoshindana na kwetu hapo ndipo naungana na mtumishi anasema litoke jua inyeshe mvua atatoa ruzuku kwa mbolea. Naomba mumuunge mkono ili kusudi aweze kutoa ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala jingine *Business Insider* wanasema *inadequate infrastructure and inadequate expertise.* Kwamba hatuna miundombinu na hatuna utaalam. Nimewaona jeshi la kilimo limeshajengwa *uniform,* usiwavike *uniform,* usiwaruhusu kurudi nyumbani wapige wiki kama mbili hapa uwapige shule na mimi uje uniite mtumishi mwenzako niwape maneno. Kwa hiyo, *inadequate expertise is very important*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala jingine ni miundombinu. Nitumie fursa hii kuiunga mkono Serikali, mwaka 1970 Muadhama Raulian Rugambwa na Baba Askofu Kibila na Sheikh Mkuu wa Mkoa wa Kagera waliamua kuanzisha

mradi wa Mto Ngono tangia siku hiyo tulijua kwamba tunakwenda kwenye neema, baadae Mzee Byabato wakaanzisha Kagera *Basin Organization*. Nimesoma kwenye bajeti kwamba Serikali inakwenda kufanya *assessment* ya *irrigation* Mkoa mzima wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie kama kuna kitu kilisahaulika na sasa hivi wakati wa Mama hakikufufuka, hakitafufuka tena. Wananchi wa Kagera, Kagera *Basin* inakwenda kurudi halafu niwaambie Ngono *Project* inakwenda kurudi halafu *basin* yote ya *Victoria* inakwenda kulimwa, tunakwenda kuzalisha chakula. Maana yake ni nini? Tunakwenda kuwa *exporter* wa mazao. Kiburi cha Ukraine ni uwezo wa kuuza nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewaambia *target* lazima mambo yote Wabunge tuyalenge kwenye malengo, unauza nini? Natofautiana na Mtumishi. Hatuwezi kusubiri mpaka 2030 kuweza kuuza nje mazao yenye thamani ya Dola Bilioni Sita *no!* Lazima kabla ya 2025 tutumie pesa hizi na Mama atakuongeza nyingine ili kusudi uweze kuzalisha zaidi. Kuzalisha zaidi ndiyo kutatuwezesha sisi kuwezakuwa na kiburi. Hatutampiga jirani yetu lakini tutakuwa na kiburi ili hata wale vijana wenye jambo lao kwa sababu tutakuwa na kipato kikubwa tunaweza kubadilisha ile jezi Namba 23 ikawa Namba 46, ni kiasi cha kubadilisha tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja niwaambie. Kiasi cha mafuta tunachotumia nchini lita Bilioni Saba ndiyo mafuta ya alizeti ambayo Ukraine anazalisha. Lakini *arable land* ya Ukraine ni ndogo tunamzidi mara tatu kwa *arable land* ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani sana, nina imani lakini kuna mazao yenye mashaka, mojawapo ya mazao yenye mashaka ni haya yanayojitokeza. Kwetu sisi tunalima vanila, Serikali itusaidie ku-*address* suala la vanilla, lakini kwetu sisi tunalima chai, chai ya Kagera irudi kwenye nafasi yake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Mwijage.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Ninakuongeza dakika moja uhitimishe hoja yako Mheshimiwa. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. Lakini jambo la Mama, zawadi ya Mama ukiiangalia utaiona na watumishi wa Mama wanakuja na heka tano kwa mtu siyo heka mbili kwa watu 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Charles John Paul Mwijage kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo wakati huo Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala ajiandae.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu kabisa Wizara ya Kilimo ambayo hotuba yake kimsingi ni hotuba nzuri na unaweza ukaona bajeti hii ni kubwa, ni takribani mara tatu zaidi ya bajeti katika kipindi kilichopita ambayo ina jumla Shilingi Bilioni 751. Kwa kweli naomba nitumie fursa hii kukupongeza sana Mheshimiwa Waziri Bashe, Naibu Waziri Mavunde, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu, Mrajisi wa Vyama vya Ushirika na Ndugu zetu Watendaji Wakuu, Bodi ya Pamba, Bodi ya Korosho, Wakurugenzi ambao kwa kweli mmekuwa mkitekeleza wajibu wenu pakubwa sana pamoja na watumishi wote wa Wizara hii ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kwa kweli kumshukuru sana na kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano, Mama yetu mpendwa Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anaipa kipaumbele sana Wizara hii ya Kilimo ili mradi kuona kwamba Watanzania sasa wanapata ukombozi kupitia shughuli kubwa kwa sababu Watanzania zaidi ya asilimia 70 ni wakulima, tuna matumaini watanzania Mama atatufikisha pale ambapo sote tunatarajia tutakwenda kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo kimsingi nataka nianzie katika eneo zima la Wizara ambayo imefanya kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba wanatoa vitendea kazi hususan pikipiki kwa maana pia vifaa kwa ajili ya kupima udongo na vifaa vingine ambavyo kwa kweli vitasaidia sana kusukuma jitihada za mafanikio katika sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili Mheshimiwa Bashe pamoja na Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote Wizara hii, ninawapongeza sana kwa ubunifu mkubwa na mawazo chanya ambayo nchi yetu ya Tanzania tunao uhakika kwa Watendaji kama hawa na Viongozi kama hawa tutafika mbali sana. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala jingine muhimu sana ni kuhusiana na suala la pembejeo. Tumeshuhudia na hasa katika eneo ambalo ni la ukanda wa Ziwa Viktoria na hasa Mkoa wa Shinyanga na sisi tunalima zao la pamba. Tumepata pembejeo kwa maana ya viuatilifu pamoja na mbegu kwa wakati. Hili ni jambo kubwa sana kwa sababu kwa miaka mingi tumekuwa tukipiga kelele kuhusiana na suala zima la kuchelewesha mbegu na kuchelewesha dawa. Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mama Samia Suluhu Hassan na chini ya Mheshimiwa Hussein Bashe ukweli umeupiga mwingi na tumepata dawa kwa wakati na mbegu kwa wakati na wakulima wamelima kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa iliyopo ni suala la mvua. Wenzangu wamezungumza hapa, tuna mvua za wastani na kwa kipindi hiki hasa cha mwaka wa kilimo msimu huu, kwa kweli tunatarajia mapato yetu ya uzalishaji kupungua kutoka asilimia tuliyokuwa tunatarajia hadi asilimia 50. Kwa hiyo, tunaona kwamba kuna uwezekano wa zao la pamba kutokupatikana katika matarajio tuliyokuwa tumejiwekea kwa sababu ya hali halisi ya hewa na kutokana na suala la mvua kutokuwepo ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba jitihada hizi ziendelee katika msimu unaokuja ili changamoto hii isije ikajirudia kwa mara nyingine kabisa kuhusu suala la pembejeo na mbegu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka nizungumzie jambo jingine ni suala zima la Kitengo cha Ushirika. Kuna changamoto kubwa katika eneo hili. Kwanza ni upungufu wa watumishi katika eneo hili. Kama tunavyofahamu Maafisa Ushirika hawa ndiyo Wakaguzi wa Ndani *(Internal Auditor)* katika Vyama vya Msingi katika maeneo yetu yote. Tatizo hili ni kubwa, unaweza ukaangalia katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu tuna Maafisa Ushirika Wanne, lakini Kishapu ina vijiji zaidi ya 128. Hili ni tatizo kubwa, Tarafa Tatu ukubwa zaidi ya kilomita za mraba karibu 4,300, ni eneo kubwa sana. Sasa Maafisa Ushirika Wanne, Vyama vya Msingi zaidi ya 98 watafanyaje kazi? Kwa hiyo, eneo hili tunaomba sana Mheshimiwa Waziri lifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ni suala zima la ku-*over stay* kwa watumishi. Maafisa Ushirika wapo ambao wanao umri wa miaka 15 mpaka zaidi ya miaka 15. Serikali na Wizara ifanye kazi ya ziada kuhakikisha kwamba watumishi hawa wawe wanahamishwa ili tuweze kuleta watumishi ambao wanaweza wakaleta chachu na mafanikio ya haraka katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala jingine ni suala la sekta ya umwagiliaji. Tunashukuru kwamba Serikali katika mwaka huu wa fedha wametenga fedha za kutosha. Naomba skimu ya kwangu ya Itilima, skimu ya kwangu ya Nyenze, Idukilo hizi zipewe kipaumbele na hasa ile ya Itilima ina zaidi ya hekari 2,000. Eneo hilo ni kubwa na ni zuri. Serikali ya Awamu ya Nne iliwahi kuleta Shilingi Milioni 200 na baadhi ya miundombinu iko sawasawa. Naomba Mheshimiwa Waziri utakapokuwa una-*wind up* eneo hili uzungumzie ni kwa namna gani utaenda kutusaidia ili hizi skimu ziweze kukaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ni Vyama vya Ushirika. Tuna Chama Kikuu cha Ushirika – *SHIRECU*. *SHIRECU* hii ndiyo imezaa Chama Kikuu cha Mkoa wa Simiyu, lakini Bukombe na Ushirombo pia *KACU*. Chama hiki ni kama tumekitupa. Zaidi ya awamu tatu au miaka mitatu ama minne tumekuwa tukiomba ukomo wa bajeti kwa ajili ya kuhakikisha tunafufua viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *ginery* ya Munze, wewe mwenyewe umefika Mheshimiwa Waziri Bashe na unaifahamu vizuri. *Ginery* ile ni nzima inahitaji matengenezo ya kawaida. *Ginery* ya Uzogole lakini tunayo *Oil Milling* Manispaa ya Shinyanga. Hizi *asset* tunazitupa, naomba Mheshimiwa Waziri, wameomba Shilingi Bilioni Sita. Shilingi Bilioni 4.4 ni kwa ajili ya ununuzi wa pamba pamoja na marekebisho ya magari, Shilingi Bilioni 1.3 kwa ajili ya kulipa madeni na vitu vingine, kwa nini katika Shilingi zaidi ya Bilioni Mia Saba hii tusije tukawafikiria *SHIRECU*? kwa sababu wakati mwingine tunakatisha tamaa Viongozi wa Ushirika na watu wa Ushirika. Naomba wakati una-*wind up* uzungumze kuhusu *ginery* ya Munze, *ginery* ya Uzogole na suala zima la ukomo wa madeni hizi Shilingi Bilioni Sita tuweze kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nina imani na wewe kwa sababu utakwenda kusaidia, lakini nikupongeze kwa sababu baadhi ya Vyama vya Ushirika ambavyo vimesajiliwa….

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Butondo kengele yako ya pili imeshalia tayari.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naunga mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea nilimuita Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala wakati huo Mheshimiwa Jackson Kiswaga anajiandaa.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kutoa mchango wangu kwenye sekta hii muhimu ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya na uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Mheshimiwa Waziri, nina uzoefu wa miaka sita, sasa tunakwenda saba; kwenye Wizara hii ya Kilimo kila Waziri anayekuja amekuwa na maneno matamu sana ya kutupa matumaini makubwa wakulima wa nchi hii. Sijawahi kuwa na shida na matumaini ya maneno matamu ya kumtoa nyoka pangoni. Shida yangu kubwa Mheshimiwa Bashe ambalo mpaka sasa kwa hotuba yako tamu uliyoitoa leo kulihutubia Taifa hili: Je, haya uliyotunenea mbele ya Bunge hili, Mheshimiwa Mwijage amesema umelihutubia Taifa; ndiyo na kweli umelihutubia Taifa, yatakwenda kutekelezeka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya unayoyasema, yasemwa miaka nenda, miaka rudi, lakini hatujawaji kuona utekelezaji wake. Suala la bajeti tulisema sana, lakini mkawa mnaongezewa, mnaongezewa, mnaongezewa. Shida siyo kuongezewa bajeti kwenye vitabu, shida ni utolewaji wa fedha kwenda kwenye utekelezaji wa miradi. Wakati mwingine nikikuangalia nakuonea

huruma kama vile unaanza kuzeeka kabla ya umri wako, lakini ndiyo hivyo tena tumekupa majukumu, kubali kuzeeka. Utalitendea haki Taifa hili kama haya uliyoyanena leo kulihutubia Taifa hili, utakwenda kuyasimamia kwa dhati ya moyo wako wakulima wa nchi hii wakaona uwepo wako kwenye hii Wizara. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba maneno yake ni mazuri na tunaona njia na nuru ya bajeti yake, lakini Mheshimiwa Waziri huwezi ukawa na miujiza yoyote yakutekeleza haya kama hutakuwa na wasaidizi wa kutosha kwenye Wizara yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitolee tu mfano upungufu wa watumishi kwenye Chuo Kikuu cha Sokoine. Chuo hiki ndicho kinachotuzalishia wataalam; na watalaam hao ndio tunawategemea watoke chuoni waende *field* kwa wananchi wetu kule kusaidia kilimo bora, kilimo chenye tija kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhitaji wa watumishi Chuo Kikuu ni 2,076; tulionao ni 1,253. Tuna upungufu wa zaidi ya watumishi 800. Bila ya hawa kuwepo, haya yote aliyoyaeleza Mheshimiwa Waziri itakuwa ni kazi bure. Kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Bashe, tunakuomba usimame kwenye ajira zinazokuja hizo zilizotangazwa na naiomba Serikali, kipaumbele iwe ni sekta ya kilimo tupate watumishi wa kutosha waende wakatusaidie kwenye suala zima la kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la pili ambalo natamani kulisema leo, ni suala zima la ushirika. Wote tunaamini kwenye suala zima la ushirika, lakini nina changamoto moja. Moja ameisema kaka yangu Mheshimiwa wa Jimbo la Kishapu kuhusu upungufu wa watumishi, lakini pamoja na upungufu wa watumishi wa Ushirika, halikadhalika watumishi waliopo baadhi yao sio waadilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna madhaifu makubwa sana ya watumishi wa Kitengo cha Ushirika kutokuwa waadilifu, lakini kwenye ushirika huko huko watumishi wetu, Maafisa Ushirika, wao ndio wanajifanya wamiliki wa ule ushirika ilhali wamiliki wa ushirika ni wananchi wenyewe walioamua kujiunga kwenye ushirika, lakini wao ndio wamekuwa ma-*top* wa ule ushirika kiasi kwamba kupelekea watu na Watanzania kuuchukia ushirika kwa sababu ya watumishi wasiokuwa waadilifu kwenye sekta ya ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kifanyike? Namwomba Mheshimiwa Waziri, watumishi wote wa sekta yako ya ushirika ambao sio waadilifu, suluhisho lisiwe kumtoa Chemba kumpeka Hombolo, suluhisho ni apaki gari lake pembeni hili atupishe tuweze kufanya kazi ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nilitembelea Mikoa ya Kusini kwa ajili ya kwenda kuona namna gani ushirika unafanya kazi. Tumekuta watu kule

wako vizuri na mfumo wao uko vizuri; na leo kwa mara ya kwanza nakuwa muumini wa Stakabadhi Ghalani ambayo niliipinga kikao kilichopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipofika kule nikakuta watu hawa kwenye ushirika wao wanafanya mazao yao vizuri, wanauza mazao yao vizuri, na kiasi kwamba inapelekea kwenda kuwa na vitega uchumi ambavyo vina fedha nyingi sana. Ila changamoto iliyopo, watu hawa unakuta wanamiliki mradi wa Shilingi bilioni 1.5 lakini watu hawa wanakwenda kukopa fedha kwa ajili ya kumpeleka mtoto wake shule, analipa riba ya asilimia 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri, naomba ushirika uende ukawafundishe wananchi wetu ambao wako tayari kujiunga na ushirika namna ya kujiwekea akiba kwenye vyama vyao badala ya kwenda kukopa benki, waepukane na kodi ya asilimia 24 waweze kuchukuwa fedha yao ile iliyoko pale waweze kukidhi mahitaji yao wakiwa wamevuna mazao yao na wanasubiri msimu wao wa bei kupanda ili waweze kuvuna mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naomba pia nizungumzie suala zima la kodi kwenye zana za kilimo. Tuna changamoto kubwa sana kwenye zana zetu za kilimo na hili limesemwa hapa. Tuna mfuko wa pembejeo ambao sasa unaenda kuzama baharini. Sasa hebu fikiria, leo mwananchi wa kawaida, wa Itololo kule ambaye ana eka zake tano au kumi, anatamani kutoka kwenye kilimo cha jembe la mkono angalau akanunue *power tiller* ama hata trekta, lakini ukienda kuuliza bei ya *power tiller* ni shilingi milioni kumi na kitu, shilingi milioni saba, na kadhalika; ukigusa trekta, shilingi milioni 45, shilingi milioni 60, shilingi milioni 30. Ni mwananchi gani wa nchi hii jamani anayeweza kumiliki trekta kwa bei hizo?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kuondokana na kilimo kisichokuwa na tija na tuwasadie wakulima wetu, tunaiomba na Serikali kwa ujumla, zana za kilimo

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** … wananchi waweze kumiliki matrekta na kuleta tija kwa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimwita Mheshimiwa Jackson Kiswaga na mchangiaji wetu wa mwisho kwa *session* hii atakuwa Mheshimiwa Neema Lugangira.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nipate kuchangia katika bajeti hii muhimu ya kilimo. Kwanza nianze kwa kumnukuu mnenaji mmoja maarufu duniani anaitwa John C. Maxwell anasema, "*everything rises and falls depending on the leadership.*" Kila kitu kinaweza kupanda au kushuka kinategemeana na uongozi. Nchi inaweza kuzama, kampuni inaweza kuzama, Wizara inaweza kuzama kutegemeana na uongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza Waziri akitoa hotuba zake kuanzia tarehe 4 siku ile wakati anagawa zile pikipiki, alitoa hotuba moja jiwe sana ambayo ilikuwa kwa kweli ni mwongozo. Kama akiweza kuisimamia, ile ni *operating model* yake ambayo akiitekeleza nchi hii itakwenda kubadilika. sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namshukuru sana Rais, kwa kweli nimekuwa nikiwasikia hawa wenzetu wanaitwa wachache wanasema kwamba *political will;* maana wakizungua mambo yao wanasema, "*political will*" kwamba tumemwona Rais ana *political will* kwenye upande wa kilimo. Hivyo nina uhakika kwamba nchi hii kwenye kilimo itakwenda kubadilika kwanza kugawa zile pikipiki karibu 7,000 na sasa kupandisha bajeti kutoka Shilingi bilioni 294 kwenda Shilingi bilioni 754. Hiyo ni *political will.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wenzangu ambao walikuwa wanazungumza kwamba ni maneno; haya sasa siyo maneno tena, kwa sababu tayari jambo limeshakuwa kwenye bajeti na bajeti zimeshatoka. Kwa hiyo, tunashukuru. Pia mwaka jana nilichangia kwa habari ya ruzuku na ninamshukuru sana Rais, pamoja na Waziri kwa sababu ya ruzuku ambayo wanakwenda kuweka sasa kwenye mbolea pamoja na mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii inaonesha namna gani tutakwenda ku-*transform* kilimo cha nchi hii. Kwa hiyo, kwa kweli niseme Mungu awabariki sana na sisi kama watumishi wenu na wafuasi wenu tutaendelea kuhakikisha kwamba tunafanya kazi ili tuwatie moyo katika kutekeleza majukumu yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumezungumzia habari ya umwagiliaji, nakushukuru Mheshimiwa Waziri kwamba sasa tunakwenda kubadilisha kilimo chetu kwenye umwagiliaji. Bilioni hizo ambazo zimewekwa kwenye kilimo, sasa naomba hata Jimbo la Kalenga lipate kufaidika pamoja na umwagiliaji huu. Kwenye Jimbo la Kalenga tuna *scheme* zipatazo 19 ndogo ndogo na za kati. Sasa changamoto nyingi tulizonazo kwenye hizi skimu, nyingi ni za kizamani na kienyeji. Kwa hiyo, unakuta kwamba zinahitaji kutengeneza mabanio tu kidogo ambayo ni bajeti ndogo ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kueleza skimu zote hapa. Kwa mfano, kuna Skimu ya Weru iliyoko Kata ya Ulanda, wanasema hii ina ukosefu wa banio, kwani iliyopo ni ya kienyeji fedha za kutengeneza banio na kugawa

mifereji; kitu kama hicho, ziko kama 19. Kwa hiyo, utatusaidia na sisi tupate bajeti, siyo kubwa, angalau tutengeneze hizi banio ndogo ndogo hata kwenye huu umwagiliaji mdogo mdogo tuweze ku-*maximize* tuweze kupata mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna skimu nyingine nilikuwa ianze, tulishafanya usanifu katika Kijiji cha Magubike Kata ya Nzi. Shilingi milioni 40 zilishatumika kufanya usanifu, lakini hatukuendelea. Hili tutaliangalia, nafikiri *document* ninayo hapa, nitakuja tuzungumze kirefu na Mkurugenzi wa Tume ya Umwagiliaji hapo ili tuone tunakwendaje juu ya hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye vyama vya ushirika, ushirika ni nguzo muhimu sana kwenye ukuaji wa uchumi unaokua kwa wakulima. Hata Mwalimu Nyerere wakati fulani alisema, katika mambo ambayo alishawahi kusikitika sana, alisema alisikitika kuuacha ushirika. Tumeona hata wawekezaji wakubwa ambao ninao kule kwenye Jimbo la Kalenga, ambao walikuja katika kulima tumbaku miaka hiyo, walitokea katika ushirika. Kwa hiyo, ushirika ni nguzo muhimu na inaweza kusaidia nchi hii ikaweza kukua kwa sababu watu wakilima katika ushirika ni rahisi sana kuweza kuratibu hata shughuli zao za kilimo lakini shughuli za kimasoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye ushirika kumekuwa na changamoto kubwa. Moja ya changamoto ambazo naziona pia kwenye ushirika ni ukosefu wa vifaa. Kwa mfano, hawana magari. Ni ngumu sana kuweza kufanya uratibu *(coordination)* wa shughuli za kilimo kama hawana vifaa. Kwa hiyo, Serikali ione namna gani itafanya kuimarisha ushirika kuhakikisha kwamba inawapa vitendea kazi, hasa magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Afisa Ushirika wengi wako chini ya Halmashauri. Sasa napendekeza hawa Maafisa Ushirika wahame kwenye Halmashauri, wawe chini ya Wizara ya Kilimo ili sasa Waziri wa Kilimo awe na nguvu ya kuweza kuwaamuru. Tuliona kwenye ardhi, Waziri wa Ardhi wa wakati huo alihamisha Maafisa Ardhi wakaenda kwenye Wizara ya Kilimo na tumeona ufanisi. Kwa hiyo, na kwenye ushirika tufanye hivyo hivyo, vinginevyo *line of reporting* zinakuwa nyingi. Kwa hiyo, hakuna mtu mwenye nguvu wa kuweza kuwasimamia. Hili tuliangalie sana ili kama tunataka tukuze kilimo chetu kiweze kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanzisha Kituo cha Afya ya Mimea pale Arusha. Tunaishukuru Serikali, sasa tunaweza kutoa ithibati; tumepata ithibati ambayo inaturuhusu sisi tuuze mazao yetu kwenye nchi zinazotuzunguka. Sasa changamoto ambayo naiona pale ni kwamba tuna mashine ambazo tulipewa za msaada, mashine moja moja; sasa Serikali ione umuhimu wa kuhakikisha kwamba tunanunua mashine nyingine ili sasa kama hii inaharibika, basi tunakuwa na mashine nyingine za kuweza kuendelea kukagua mazao yetu na kuendelea kuyapa ubora unaotakiwa ili tuweze kuuza nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ambalo nimeliona, hatuna wataalam. Mara nyingi mitambo ikiharibika tunaleta wataalam kutoka nje na gharama za kuwalipa hawa ni kubwa sana. Kwa hiyo, Serikali ione umuhimu wa kupeleka vijana wetu wakajifundishe huko nje ili waje wahudumie hizi mashine zetu, tusiingize hizi gharama za kuleta wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye suala lingine ni kwenye maghala. Nilishalizungumza suala la maghala kwenye viwanda, lakini huku nitalizungumza katika mtizamo mwingine. Maghala yatatusaidia sana. Kwanza tumekuwa na tatizo la sumukuvu kubwa sana katika nchi hii na ukiangalia mazao yanavyohifadhiwa katika maeneo yetu mara nyingi wanamwaga chini ardhini, lakini tutakapokuwa na maghala mpaka kwenye vijiji kama Waziri alivyozungumza, yatasaidia sana kwanza kutunza ubora, na pia kudhibiti upotevu wa mazao. Tuna asilimia karibu 30 mpaka 40 ya mazao yetu yanayopotea. Kwa hiyo, tukiwa na haya maghala itasaidia sana kuratibu na pia kuwa na mazao yenye ubora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kwenye hili atafute pesa, aidha anakopa; hapo ni mahali pazuri pa kuanzia. Hapo utatengeneza alama, utawasaidia Watanzania kupata masoko na utaweza kuratibu mazao yanayozalishwa katika nchi hii na kuwatafutia masoko.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naona kengele imeshagongwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimwa Jackson Kiswaga kwa mchango wako. Mchangiaji wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Neema Lugangira.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii. Napenda kuanza kwa kumshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri na Wizara ya Kilimo kwa kutambua umuhimu wa lishe. Kwa mara ya kwanza kwenye hotuba ya bajeti ya Wizara ya Kilimo jambo la lishe limetambuliwa na limetajwa kwa kina. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo, hivi karibuni Wizara ya Kilimo imezindua Kampeni ya Kitaifa ya Lishe na huo ni mwendelezo wa kutekeleza ahadi ya Ilani ya Chama vha Mapinduzi ambapo jukumu la kutokomeza masuala ya udumavu na aina zote za utapiamlo yamewekwa chini ya Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana pia Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuweka uzito mkubwa katika suala zima la tafiti na uzalishaji wa mbegu ili kuongeza tija ya kilimo. Nami mchango wangu kwa siku ya leo utajikita katika eneo la mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri wa Kilimo amesema, "hivi sasa tunazalisha mbegu kwa asilimia 26 tu ya mahitaji yetu." Kwa maana hiyo, bado uzalishaji wa mbegu uko chini na hatujitoshelezi. Kwa hiyo, lazima tuweke jitihada za makusudi kabisa ili kuongeza uzalishaji wa mbegu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ameelezea mipango ya kina ya Serikali katika kufanya tafiti na pia kuimarisha mbegu za msingi pamoja na mbegu za awali. Naomba nitumie fursa hii kuikumbusha Wizara Kilimo, hatuwezi kuongeza tija ya mbegu zetu kama hatukuwa tunajumuisha mbegu za asili. Kwa mantiki hiyo, namshukuru pia Mheshimiwa Waziri ametoa ahadi hapa kwamba ifikapo 2025 mbegu za asili zitakuwa zinauzwa madukani kama ilivyo mbegu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tufikie hapo, yapo mambo ya msingi lazima yaanze kufanyika hivi sasa. Kwa hiyo, napenda kupendekeza mambo manne yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, tukija kwenye suala la kiusalama, tumeona vita ya Ukraine na Urusi, jinsi ambavyo nchi inaweza ikaamua kutokuuzia kile ambacho inazalisha. Kwa hiyo, nasi tukiendelea kutegemea mbegu za nje kwa zaidi ya asilimia 70, ipo siku tutakuwa hatarini kutopata mbegu yoyote, hivyo kujikuta tuna njaa. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri ahakikishe ya kwamba suala la uzalishaji wa mbegu ndani ya nchi analitia uzito mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa pili, Sheria ya Mbegu ya Mwaka 2003 haitambui mbegu za asili. Sasa tutafikaje 2025 kuzizalisha ziuzwe madukani ikiwa Sheria ya Mbegu ya Mwaka 2003 haitambui mbegu za asili? Kwa hiyo, naomba sheria hii ya mbegu ya mwaka 2003 ifanyiwe mapitio ili sheria hii izitambue na iweze kuzilinda mbegu zetu za asili kama ambavyo wanafanya nchi za wenzetu India, Ufilipino, Malaysia, Ethiopia na Zimbambwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa tatu, ni lazima sasa Wizara ichukue jitihada za makusudi kabisa za kuboresha Kituo cha Tafiti cha Kutumia Vinasaba vya Mbegu ili kwanza kuimarisha uzalishaji wa mbegu zetu na pia sisi kama Taifa tunaweza tukaingia kwenye soko la vinasaba vya mbegu duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa mwisho, ni lazima tuanzishe benki ya mbegu za asili ambazo zitasimamiwa na jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naungana na wenzangu kuwapongeza sana Waziri Mheshimiwa Bashe pamoja na Mheshimiwa Anthony Mavunde. Mheshimiwa Bashe ni kaka yangu, ni kati ya *mentors* wangu, lakini atakapohitimisha, asiponipa maelezo ya uhakika ya kujitosheleza kwamba Wizara hii inakwenda kufanya nini ili kuzitambua na kuzilinda mbegu za asili, basi nitaondoka na Shilingi yake na ataifuata Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kikao chetu cha asubuhi *session* ya kwanza leo. Hapa kuna wageni wachache naomba kuwatambulisha.

Wako wageni wa Mheshimiwa Hussein Bashe, Waziri wa Kilimo kutoka Simiyu, ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa Mkoa wa Simiyu, wakiongozwa na Ndugu Shemsa M. Seif ambaye ni Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Simiyu, akiambatana na Katibu wa CCM wa Mkoa Bwana Innocent Nanzaba. Karibu sana kiongozi wetu wa chama. *(Makofi)*

Pili, kuna mgeni wa Mheshimiwa Hussein Bashe pia ambaye ni Nevile Meena, Mwandishi wa Habari. Sijui kama yuko hapa. Ah, nilifikiri huyu hapa.

Tatu, mgeni mwingine wa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ni Ndugu Nduimana Azaile ambaye ndiye Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha Mbolea cha *ITRACOM* kinachojengwa hapa. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tutakaporejea watakaoanza kuchangia ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mheshimiwa Yahya Ally Mhata pamoja na Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga na Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna. Kwa hiyo, wajiandae.

Nahitimisha shughuli hizi za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nilimtaja Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga na Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna. Naomba tuanze na Mheshimiwa Miraji Mtaturu.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyoko mezani ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kutoa pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya kwa ajili ya Taifa letu na katika kila hatua anayoendanayo katika muda wa uongozi wake amekuwa akiwaletea matumaini makubwa Watanzania. Ushahidi mkubwa ni huu wa juzi tu pale alipoamua kusikiliza cha wafanyakazi na kuweza kupandisha mishahara kwa asilimia 23. 3, ambayo ni kubwa sana nchi, zote za Afrika hazijafanya hivyo, ni Tanzania peke yake. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri. Tumepokea hotuba yake, tumepokea mipango ya Wizara yake. Kwa hakika Mheshimiwa Bashe unatuheshimisha sana kama Taifa, unafanya kazi nzuri sana. Kama kijana wa Kitanzania unaonekana wazi wazi wewe ni mzalendo wa kweli, na kwa hakika Mheshimiwa Rais hakukukosea na kukuweka kwenye Wizara hii. Hongera sana, tunaomba tukuhakikishie kwamba Wabunge tutaendelea kukuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa ndugu yangu Mheshimiwa Antony Mavunde, Naibu Waziri, nawe unafanya vizuri, unamsaidia sana Mheshimiwa Waziri na timu yenu ni timu ambayo inaonekana wazi kwamba inaenda kufunga magoli ambayo ni magoli ya kukiboresha kilimo cha Tanzania. Nimpongeze sana Katibu Mkuu kaka yangu Massawe Pamoja na Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa namna mlivyojipanga vizuri katika kukileta kilimo kiwe ni kilimo cha manufaa kwa ajili ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo nimefurahi kuona kwamba hata bajeti, kama ambavyo nimepongeza Mheshimiwa Rais, ni utashi wa hali ya juu sana kwamba kutoka bajeti ya bilioni 234 kwenda

mpaka bilioni 751 si jambo dogo. Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, lakini hii ni mipango ambayo Wizara ikiongozwa na Waziri wameweza kumpelekea maoni na mapendekezo yao. Nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri, huu mwendo mzuri. Wabunge tumekuwa tukilalamika hapa kwamba bajeti ni ndogo, lakini kwa bajeti hii, ingawa ni ndogo lakini inaweza kuwa nafasi nzuri ya kuanzia katika kuboresha kilimo chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nitakuwa na maeneo machache kuchangia leo. Nitachangia leo, nitachangia kuhusiana na kilimo cha umwagiliaji, suala la mbegu na nitamalizia ushirika kama muda utanitosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa eneo la umwagiliaji. Nimefurahi sana kwamba katika bajeti hii tunayoenda kuiangalia hapa tumeona ambavyo tumevuka vizuri. Bilioni 51 zitaenda kuleta mapinduzi makubwa kwenye kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu nilikuwa naomba, kama ambavyo ulishasema huko nyuma, kwamba tutajitahidi kuhakikisha kwamba Tume ya Umwagiliaji inakwenda kwenye halmashauri zetu. Kule ndiko kwenye mahitaji, na nivizuri wakiwa Jirani kwa sababu wataweza kusimamia kwa karibu sana. Ni kweli kwamba tumekuwa na maafisa kilimo lakini yeye ana-*deal* na mambo ya ugani na mambo mengine, lakini suala la umwagiliaji ni *component* inayoonekana kama Wizara ya maji hivi. Lakini kwa sababu Tume ya Umwagiliaji iko mezani kwako ukiweza kuweka wawakilishi ambao watakuwepo muda wote, wanaamka na kulala pale pale, watasaidia sana kuhuisha kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi niseme tu, kwa bajeti ambayo tumeiona hapa tukijipanga vizuri tunaweza tukaibadilisha sana kilimo chetu kwa sababu kilimo cha kutegemea mvua kwa kweli tumeona kimekuwa hakina tija tena. Ninyi wenyewe ni mashahidi, mwaka huu tulijitahidi kupeleka mbegu, na nipongeze sana kwenye eneo hili; mmepeleka mbegu za kutosha mfano za alizeti kule Singida Mkoa wa Dodoma pamoja na Mkoa wa Simiyu, lakini mvua zimekuwa chache; maana yake jitihada zetu zimekwenda kugonga mwamba. Lakini tungekuwa na maji ya kutosha, tungekuwa na skimu za umwagiliaji wa kutosha leo hii ile mbegu ambayo tumeipanda kule isingepotea, maana kuna baadhi ya maeneo hakuna tena matumaini ya kuvuna alizeti ambayo tumeipanda kwa bei nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kipekee kabisa kwangu mimi kwenye eneo la kwangu pale Jimbo la Singida Mashariki niliongelea Habari ya skimu ya umwagiliaji wa Mang'onyi. Nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwamba mmekubali kunipelekea milioni 700 ambayo itaenda kuisaidia sana skimu ile ili ianze kufanya kazi. Wananchi wa Mang'onyi wanatusubiri kwa hamu. Lakini kama haitoshi kwenye ule mgodi wa madini ambao unaenda kufunguliwa hivi karibuni wako tayari kununua mboga mboga kutoka kwenye mashamba

ya wakulima wale. Maana yake ni kwamba, soko litakuwepo na hiyo skimu italipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama haitoshi niombe sana tuongeze suala mabwawa katika maeneo mbalimbali katika jimbo langu, tukiweza kuweka mabwawa yatawasaidia wakulima kuendelea kufanya kilimo cha umwagiliaji. Naomba, kama Kata za Mkiwa, Kikio, Isuna, Mang'onyi, Misuwaha paoja na Ndung'unyi tukipata mabwawa yatatusaidia sana kuboresha kilimo chetu ambacho ni kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mbegu ni roho ya kilimo. Tukiwa na mbegu nzuri zitasaidia kuleta mazao mengi, uzalishaji wa mazao ukiwa mwingi maana yake hata mnyororo wa thamani utakuwa umepatikana. Kwa kwa hiyo niombe sana; kuna suala ambalo tumelizungumza hapo nyuma, tuwe na mbegu zetu za asili na tuzilinde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anajua namna ambavyo GMO tumekuwa tukitumia sasa hivi; lakini kuna mahali ambapo tukitegemea tutakuwa ni watumwa wa mbegu za nje siku moja tutajikuta hatuna mbegu zetu, na hivyo hatutakuwa salama. Hata hivyo tunao wenzetu wa *ASA* ambao ndiyo wakala wa mbegu nchini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa; hitimisha hoja yako basi, naona muda wako umekwisha.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** …Mheshimiwa Mwenyekiti, basi ninaomba sana mbegu zipewe kipaumbele ili ziwasaidie wakulima kupata tija na ninaamini kabisa uzalishaji utaongezeka na lengo la wizara itatimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa muda kidogo utakuwa umepunguzwa kwa sababu wachangiaji wapo wengi. Kwa hiyo, ni vizuri tukaenda kwa utaratibu mzuri. Nilimuita Mheshimiwa Yahya Ally Mhata.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ameniwezesha mchana huu kusimama ndani ya Bunge lako hili Tukufu ili kujadilia bajeti hii ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitatoa shukrani kwa hawa wafuatao. Naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya wizara hii, Naibu wake, Katibu Mkuu, Mrajisi wa Vyama vya Ushirika na watumishi wote wa Wizara ya Kilimo ambao kwa njia moja au nyingine wameshiriki katika maandalizi ya bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka Jimbo la Nanyumbu, jimbo ambalo ndilo ambalo linazalisha sana korosho, tunazalisha sana ufuta na tumeanza kujikita katika kilimo cha alizeti. Sasa kwa leo naomba nijielekeze kilimo cha korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitamshukuru sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Samia Suluhu Hassan ambaye kwa miaka miwili mfululizo ameweza kutupatia pembejeo bure. Hili jambo kwakweli nila kushukuru sana, kwa sababu moja ya changamoto ya wakulima ni upatikanaji wa pembejeo; lakini si pembejeo bure kwa mara ya kwanza pembejeo zimefika kwa wakati ndani ya wilaya yetu. Hili ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tarehe 17 mwezi wa tano, Mkuu wetu wa Mkoa, ndugu yangu Kaguti amekuwa akishikiri katika kuhakikisha pembejeo zinasambazwa kwenda katika wilaya zetu. Kwa hiyo, mimi natoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Waziri na uongozi mzima wa mkoa kwa jitihada wanazofanya katika kuhakikisha kwamba kilimo chetu cha korosho kinakwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewahi kuzungumza ndani ya Bunge lako kwamba pembejeo peke yake haitoshi, wananchi wetu wanahitaji fedha kwaajili ya palizi, kupulizia mikorosho, kuokota korosho na hatimaye kukusanya hizo korosho na kuzirudisha nyumbani. Lakini, wananchi hawana fedha. Kwa hiyo, tunatarajia benki zetu zi-*support* nguvu za wananchi, na nguvu za mama yetu. Hata hivyo, benki zetu zinatuangusha. Tarehe 28 mwezi wa nne *MAMCU* walifanya Mkutano Mkuu pale Masasi na Benki zote zilikuja pale, Mkuu wa Mkoa aliwaita akawahimiza kutoa mikopo kwa vyama vya msingi. Mimi nina vyama 37, lakini mpaka nianvyozungumza hakuna hata chama kimoja kimepata mkopo kwaajili ya zao la korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunakata kuinua zao la korosho, tutainuaje zao la korosho kama hatuwapatii mikopo wakulima wetu? Juzi hapa nimemsikia Mheshimiwa Waziri, ndugu yangu Mkenda, anasema Benki ya *NMB* imetoa bilioni mbili kwaajili ya mikopo kwa vijana wetu. Sasa, sasa hizi benki zinashindwaje kutoa mikopo kwa wakulima ili waweze kuinua zao letu la korosho? Kwa hiyo, ninakuomba sana kesho Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa anieleze na anishawishi; ni jitihada gani amezichukua kuzishawishi hizi benki ili ziweze kuwakopesha wakulima wetu; vinginevyo tunatwanga maji kwenye kinu. Hatuwezi kuinua zao la korosho kwa kutumia nguvu ya mwananchi kupata msaada kutoka kwenye benki zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu uadilifu kwa wataalamu wetu, hasa wafanyakazi wa ushirika. Tunawafanyakazi ambao si waadilifu, Ndani ya Jimbo langu msimu huu uliopita zaidi ya shilingi milioni 60 hazikuweza kulipwa kwa wakulima na chanzo kikubwa ni watumishi wa Idara ile ya Ushirika. Jambo hili Mheshimiwa Waziri analifahamu sana, kwamba tunao

watumishi pale si ambao si waadilifu lakini wanaachiwa. Tunakuja kuwaeleza jamani huyu mtumishi si mwadilifu lakini wanasema huyu ndiye anafanya kazi. Sasa, kama anafanya kazi basi mumchukue nyinyi kwa sababu kule kwa wananchi amesababisha matatizo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hakuna kitu ambacho kinaudhi kama mkulima amelima korosho, amepeleka *godown* halafu asipate fedha. Halafu mfanyakazi wa ushirika ambaye ndiye *Internal Auditor* katika *AMCOS* anasema kwamba *AMCOS* zote hazina matatizo, lakini kumbe kuna matatizo kibao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ninamuomba sana Mheshimiwa Waziri, hawa watumishi ambao tunakuja kukuletea malalamiko uchukue hatua *immediately.* Haiwezekani wakulima wanapata tabu, na tukienda sisi Wabunge tunalalamikiwa kama vile sisi ndio tumesababisha matatizo hayo kumbe ni watumishi wenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ninayoiona kwa hawa wafanyakazi wa ushirika wanawatu wawili wanaowajibika kwao kuna Mkurugenzi wa Halmashauri halafu kuna Mrajisi wa Vyama. Sasa naomba sana Serikali iamue hawa watumishi wapelekwe eneo moja. Na mimi ningeomba hawa watumishi wa ushirika wote waende kwa Mrajisi ili waweze kuwajibika moja kwa moja; vinginevyo wale watumishi kule wanakuwa kama miungu watu. Wao badala ya kuvisimamia hizi *AMCOS* wao ndiyo wanakuwa wenye *AMCOS.* Wananchi ambao ndio wenye *AMCOS* wanaweka pembeni wao ndio wanakuwa miungu watu. Sasa hili jambo kweli halikubaliki, hatukubali kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kesho Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa aeleze ni jitihada gani amezifanya kwa hawa watumishi ambao wamesababisha hasara kubwa ndani ya wilaya yangu, wamesababisha kadhia kubwa ndani ya wilaya yangu na bado wapo ndani ya wilaya yangu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache naomba kuunga mkono hoja, nategemea majibu mazuri sana kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kesho. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako Mheshimiwa Yahya Ally Mhata. Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kukushukuru kwa kunipa nafasi. Nimshukuru Mheshimiwa Rais na kumshukuru

Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu na Makatibu Wakuu, pamoja na waratibu wa taasisi zote zinazoshiriki kwenye mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kutoa pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri kwa muda mchache ameleta matumaini makubwa ndani ya Sekta ya Kilimo. Na hii nikwasababu Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake wamekuwa vijana wakizunguka nchi hii kusikiliza kero za wananchi, kero za wakulima na kuhakikisha yakuwa wanakuja kuzifanyia kazi niwapongeze sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninayo machache. Kwanza la kwanza Mheshimwa Waziri tukupongeze sana kwa hatu ya kwanza ambayo umefanya kutoa pembejeo bure kwa wakulima hususani kwenye zao la pamba. Mimi nisipoizungumzia pamba sitapata usingizi kwasababu ndio mkoa mkubwa unaozalisha pamba ya Tanzania hii. Na ndiyo inayowapatia wananchi wangu kipato kikubwa ambacho tunakitegemea na mwaka huu wa fedha ulioisha tulipata tena zao la alizeti. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunakupongeza kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa iliyopo ni suala zima la viuatilifu vinavyopatikana. Kwamba vinakuja ndani ya muda, lakini kulingana na elimu ya watumiaji wetu ile dawa haiui wale wadudu. Sasa, kwa kutokuua kule kunasababisha madhara makubwa sana. Jambo muhimu ambalo umelizungumzia leo kwenye suala zima la utafiti mimi nadhani wadudu waliopo sasa ni tofauti na mazoea tuliyonayo. Mwaka huu tungetarajia kupata takribani tani laki 400, lakini naamini tunaweza tukapata 200 au 300. Madhara makubwa yametokana na viuatilifu ambavyo vimepatikana tukavisambaza vijijini bila kuwa na elimu nzuri kwa watumiaji wa hivyo viwatirifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana, kupitia Bodi ya Pamba usimamizi uongezeke. Wamefanyakazi kubwa sana na zao lilikuwa limepotea lakini tunaona matumaini makubwa sana ambayo sasa yanaweza yakatuletea fedha za kigeni nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye suala la mafuta, kwa sababu unapoizungumzia pamba unazungumza mbegu na unapata na mafuta. Kwa hiyo, naamini kabisa tukiwa madhubuti na tukiwa na usimamizi uliobora imani yangu kubwa kwamba tutapiga hatua kubwa sana. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, leo Mkoa wa Simiyu Kamati ya Siasa ya Mkoa ilikuwepo hapa, imekuja kushuhudia jambo kubwa Mheshimiwa Waziri alilolisema, la kufanya majaribio katika maeneo haya ya ushirika. Mimi sina tatizo na ushirika, ninachokuomba Mheshimiwa Waziri hakikisha unatafuta fedha tuwape washirika wa Mkoa wa Simiyu na mikoa mingine kama Kaku, kama Uchato na kama kule Bukombe ili waingie

kwenye soko watengeneze ushindani wa kwenda kufanyabiashara na sekta binafsi. Ukifanya hivyo utatengeneza ushindani mkubwa na imani kubwa…

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumtaarifu mchangiaji kaka yangu Njalu kwamba wananchi wa Mkoa wa Simiyu wanampongeza sana Mheshimiwa Rais pamoja na Waziri kwa kukubali mwaka huu kuwa na soko huria la zao letu la pamba kwenye Mkoa wa Simiyu, ambapo inapunguza sasa unyanyasaji ulikuwepo kwenye AMCOS zetu kwa kuwadhulumu fedha zao wakulima. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Njalu unapokea taarifa.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naye alitakiwa apate muda wa kuchangia, naipokea. Ni kweli jambo hili ni muhimu sana. N aamini Mheshimiwa Bashe kwa kufika mpaka kutoa maamuzi hayo alipoteuliwa kuwa Naibu Waziri mwaka 2019 madudu yaliyokuwepo kwenye Mkoa wetu wa Simiyu na kwa Tanzania kwa ujumla anajua na bosi wake siku moja aliomba kusema ushirika ufutwe. Kwa hiyo, ni jambo ambalo ameliona yeye kwa kulishuhudia nawala hajafuta na wala hatuzungumzi kufuta ushirika tunahitaji ni kuboresha wasiwe wagaragaja kama neno lake alivyokuwa akilitumia wakati akiwa hajawa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuwe na sera ambazo haziwezi kuyumbisha Taasisi za Fedha. Sera zilizo imara zilisimama zitatusaidia sana sisi kama nchi kuhakikisha uzalishaji wa mazao yetu tunayafanya yanapata tija na tunapata fedha nyingi za kigeni kupitia mazao hayo. Kwa hiyo naamini, kwa haya ambayo tunaendelea kuyazungumza na tunaendelea kuishauri Serikali wakiyasimamia vizuri tutakuwa na uzalishaji ulio na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumeona kuna watu wa makombati walikuwepo hapa, basi yale makombati yaende yakafanye kazi, ikibidi Mheshimiwa Waziri awafungie hata *GPS* ili tuwe tunawaona wakiwa mashambani kabisa kazi wanazokuwa wanazitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pikipiki nazo ziende vijijini, kuna hatari ya kuja kupasuka matairi tena, zikikaa zinapigwa jua muda mrefu tunakuta zinaharibika. Kwa hiyo, niendelee tu kusema kwamba kazi hii nzuri ambayo Waziri anaifanya, naamini kabisa kwamba tutafanya mazuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilianzisha Benki ya *TADB* na Benki ya *TIB Commercial Bank,* hizi zote zilikuwa na madhumuni yake. Mheshimiwa Waziri

ameizungumzia Benki ya *TADB,* jukumu lake kubwa ni kuhakikisha inasimamia kilimo. Sasa leo tunazungumzia *allegation* na vitu vingi na vingi. Kwa hiyo ningeomba Wizara husika hii Benki tuiangalie kwenye jicho la pekee ili itoe huduma kwenye jamii hii ambayo tunayoitarajia. Tukifanya hivyo, kwa sababu yenyewe haifanyi biashara kazi yake ni kuhakikisha inavyoelekezwa na Serikali inapeleka kusaidia pembejeo, umwagiliaji na vitu vingine vyote kadha wa kadha ambavyo vinawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitumia fursa hiyo na fedha tunazozitenga kwa Wizara zikienda, aliyokuwa anayasema Mheshimiwa Mwijage asubuhi yatatimilika, nchi hii ni tajiri, ina vitu vingi kila kona kuna uzalishaji wa kutosha. Miaka hii miwili bei za mazao yetu zimeendelea kukua kwa kasi ni kwa sababu uzalishaji tunao na watu wetu wanajituma. Nchi za wenzetu kuchuma ile pamba wanatumia mashine, lakini sisi wakulima wetu wanavuna pamba iliyo nzuri na iliyo bora zaidi, lakini nchi zingine kila kitu ni *remote, remote*. Kwa hiyo utaona bado tuna nguvu ya kutumia, kwa hiyo kama Taifa tuna jukumu, nguvu hii kuitumia hivi sasa ili kizazi kinachokuja kiweze kufaidika na haya tunayoyatarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya haya machache, naunga mkono hoja na nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Pia nawatakia kila la kheri wenye Wizara, mambo yaendelee vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga kwa mchango wako. Namwita Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna, wakati huo Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mheshimiwa Lucy John Sabu na Mheshimiwa Daktari Charles Stephen Kimei wanajiandaa.

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha sote kuwa hai. Nakushukuru pia kwa nafasi uliyonipatia. Nawapongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Makamu wa Rais, kwa majukumu yote ambayo wanatupigania Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, ni Amiri Jeshi wetu Mkuu ana majukumu makubwa anatupambania Tanzania. Tunamshukuru kwa yote. Nawapongeza pia Mawaziri kwa kazi wanayoifanya na pia naipongeza Wizara yote ya Kilimo na watendaji wote, nawapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 65 ya Watanzania ni wakulima, lakini walio wengi ni wakulima wadogo wadogo ambao sehemu kubwa ya wakulima hao wana changamoto. Changamoto hizo ni kama ukosefu wa wataalam, wana changamoto za mitaji midogo kadha wa kadha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia Mkoa wa Morogoro, wenzetu wana changamoto hizo nyingine, lakini sisi tuna changamoto kubwa zaidi.

Jamani Mkoa wa Morogoro ni mkoa ambao Mungu ametupendelea, ametupa fursa ya ardhi nzuri, lakini ardhi ile sisi inatutesa. Ardhi inatutesa sasa hivi imekuwa ni shubiri, lakini watu wa nje wanaona kama vile sisi ile ardhi inatusaidia, haitusaidii hasa kwa akinamama. Kwa nini nasema hivyo? Kwa sababu mwanamke anatoka nyumbani kwake anaenda shambani kwenda kulima, lakini mwanamke yule hawezi kulima kwa sababu anaogopa wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akifika shambani, wafugaji wakimwona kwenye shamba lake ambalo ameshalilimia, ameshalipalilia, ameshalifanyia huduma zote, mfugaji yule anakuja kulishia kwenye lile shamba hatimaye yule mama akiuliza kwa nini unalilishia, yule mfugaji anaweza akampiga, wanawafanyia vitendo vya udhalilishaji, hatimaye wakati mwingine hata kuwapotezea maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ni mbaya, hivi ninavyoongea hapa, asubuhi nimepigiwa simu kwamba mfugaji ameenda kupeleka mifugo yake kwenye shamba la mtu amekula heka 30, asubuhi ya leo. Sasa jamani tunajenga Tanzania ya aina gani? Mtu akienda shambani kwake nina mfano halisi, mtu ameenda, maskini, mkulima yule, ameenda amekodi shamba la 150,000, ameenda amelimwagilia mpunga umefika mkubwa anataka kuvuna, mwenye ng'ombe akapeleka kwenda kulishia wafugaji, kujitetea kwa nini unaenda kulishia shamba langu akampotezea maisha. Nafikiri hata kwenye vyombo vya habari mlisikia, ilikuwa ni tarehe 27/12/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo hali haijatokea sehemu moja, imetokea sehemu nyingi, imetokea katika Jimbo la Mlimba, Jimbo la Kilosa, Mvomero na Wilaya ya Morogoro Vijiji, Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki tarehe 8/5/2022. Serikali kwa nini kuwe na matatizo ya wakulima na wafugaji miaka nenda rudi, kwa nini kusiwe na amani? Yule mtu wa Morogoro alizoweya yeye anaenda shambani analima, lakini sasa hivi nini matokeo ya hiyo hali, matokeo yake ni kwamba wale watu umaskini tuliokuwa nao umekithiri, njaa inazidi kuwa kali na kipato kimekuwa duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali, chonde watuangalie ili tukomeshe hii hali ya wakulima na wafugaji. Nchi yetu ya Tanzania ni nchi ya amani, lakini kwa nini tufikie hapo kwenye kugombana. Watu wa Morogoro ni rahimu, wanawakaribisha wageni wote wanaokuja Morogoro hakuna ubaguzi, lakini tunapofika tushirikiane tuishi kwa amani. Akinamama wanadharaulika, wanadhalilika hasa, hawawezi kwenda mashambani, wajawazito wanawafanyia vitendo vya ovyo. Sasa naiuliza Serikali je, hii hali itaendelea hivyo mpaka lini? Tunasema kwamba vijana wanakimbilia mjini, mtu anaenda analima, shamba lake linaliwa, ataacha kwenda mjini, atakaa kijijini anafanya nini? Naomba Serikali waliangalie hilo kwa macho ya huruma, chonde chonde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema kwamba, sasa hivi tunataka maendeleo, ardhi tunayo, lakini maendeleo hatutapata, huwezi kupata maendeleo bila kufanya kazi. Unafanyaje kazi mtu, unalima lakini unachokipata hakuna na kwa vyovyote vile lazima kama mfugaji anakula mazao ya mkulima amani inakuwa haipo. Wale watu watakuwa hawafanyi kazi. Naomba majibu ya Serikali, waniambie kwamba je, wana mpango gani au wana mkakati gani kwa hatua hii iliyofikia ili tuweze kuwa na amani? Kwa maana tusipofanya hivi, tutazidi kukaribisha umaskini, tutazidi kuwa na vijana ambao Serikali imepanga mipango mizuri sana ya kuwawezesha, lakini watawawezesha kupitia nini na wakati sisi tunasema tunategemea kilimo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali ikomeshe hiyo migogoro, nafikiri itafika mahali itaonekana kwamba hawa wafugaji ina maana wana nguvu kuliko Serikali. La hasha siamini hilo, naamini Serikali ina nguvu kuliko wafugaji. Sasa inatosha, kama tulikuwa nyuma hatujaliona hilo tatizo, hilo tatizo lipo, Serikali tuamke sasa tulifanyie kazi, tulimalize, hatimaye wale watu waweze kufanya kazi turejeshe amani ambayo Tanzania tumeizoweya.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna kwa mchango wako.

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuongeza sekunde kama 40 hivi, ahsante sana.

Nilishamwita Mheshimiwa Aida Joseph Khenani.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi ili niweze kuchangia. Niunganie na Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa uwezo wake binafsi kwa namna ambavyo ameandaa Hotuba yake vizuri sana na mipango mizuri sana kwenye hotuba yake. Pia nimpongeze pia Naibu Waziri, tumeona namna ambavyo wanawajibika kwa muda mfupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache, leo nitakwenda kwenye *angle* ya tofauti, miaka yote sita nilikuwa najikita sana kwenye utafiti, nimeona wameongeza fedha kidogo. Naamini hakuna maendeleo ya kilimo bila kuwekeza kwenye utafiti, leo wamewekeza hiyo fedha, lakini kuwekeza ni jambo moja na kupewa fedha ni jambo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia namna ambavyo Waziri ameisoma hotuba yake na mipango yao ni mizuri sana, unaona kweli kwamba wameanza kusikiliza mawazo ya Wabunge. Leo nitajikita zaidi kwenye Wizara

ya Fedha na Serikali ni vizuri wakatuelewa. Wakati tunazungumza bajeti hii ambayo imesomwa leo, bajeti iliyopita mpaka Februari tukiwa tunakuja kwenye lile Bunge la Mwezi Februari, walikuwa wametekeza kwa asilimia 35 tu ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Hili jambo kama Wabunge hatuwezi kulifurahia, tukiidhinisha fedha ni vizuri ziende kama tulivyoidhinisha kama Bunge. Sasa kwa kuwa mipango ya Mheshimiwa Waziri ni mizuri na *figure* imepanda kidogo, sasa kupanda kwa *figure* ni jambo moja, lakini tunataka fedha hiyo iende kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitajikita katika mkulima wa kawaida kabisa anayetumia jembe la mkono. Nataka kuja kujenga hoja yangu kwa nini ruzuku ni lazima na siyo ombi kwenye mbolea. Mkulima wa kawaida kabisa kwa eka moja anakodi kwa Sh.50,000, mkulima huyo anaandaa hilo shamba kwa Sh.50,000 inakuwa Sh.100,000. Mkulima huyo kwenye ekari hiyo hiyo inabidi anunue mbegu mifuko mitano ambayo thamani yake ni Sh.62,500, mkulima huyo inabidi anunue mbolea mifuko mitatu kwa bei ambayo imepita sasa hivi ni Sh.360,000 kwenye eka moja, mkulima huyo huyo atafanya palizi mara mbili kwa Sh.100,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, kuna kuvuna, kupiga na kusafirisha kutoka shambani mpaka nyumbani jumla yake nimepiga kwa ekari moja peke yake anaweza kupata gunia 20, huyo wa Nkasi kwa gharama zote nilizosema hapa. Gunia 20 bei hiyo ambayo atakwenda kuuza kwa wakati huo ni Sh.35,000. Jumla ya mapato yake yote kwenye eka nzima ni 700,000; akiuza hayo mahindi gunia 20 wakati gharama zote alizotumia ni 742,000 hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuuliza Mheshimiwa Bashe, hii bajeti tunayotenga tunaenda kumlenga mkulima gani? Ni kweli tunataka kuwainua wakulima wadogo leo, waliokuwa wanalima kwa mkono, watoke wakanunue trekta? Bado najiuliza pamoja na *figure* yote hiyo bado hatumkomboi mkulima wa kawaida. Hivyo, nataka nishauri mambo yafuatayo:- *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza, pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri amesema ruzuku, sisi Wabunge tunasema ruzuku ni lazima na Wizara ya Fedha itoe fedha kumpatia Waziri wa Kilimo ili akatekeleze. Kumekuwa na utaratibu ambao siyo mzuri sana, yaani Waziri anakuja hapa anaeleza mipango yake, mwisho wa siku Wizara ya Fedha ndiyo inakuwa kikwazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo muda ambao mkulima anautumia kwanza anapoteza muda wake wa kutosha zaidi ya miezi mitatu kuandaa eneo lake, lakini kinachokwenda kumkwamisha ni hiyo mbolea, hivi nani anaweza leo kutumia 842,000 halafu kwenye eka moja hiyo akapata 700,000, ni mkulima gani ataenda shambani? Safari hii hali si nzuri sana, hali si nzuri sana na kwa sababu hali si nzuri, mwaka jana tumepiga kelele hapa,

tunamshukuru Mheshimiwa Rais alitoa fedha ikaenda kwa ajili ya ununuzi wa mahindi, lakini ule muda Serikali iliotoa fedha haikwenda kumlenga mkulima wa chini, ilikwenda kupeleka fedha ikaenda kununua kwa wale waliolangua kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka fedha iende mapema, lakini na mbolea iende mapema na si kwenda tu, lazima Mheshimiwa Bashe, abadilishe utaratibu na achunguze kwa kina nini huwa kinatokea kwenye mbolea. Waziri asipojua tatizo hata akiweka ruzuku bado mkulima wa kawaida hawezi kufaidika na hii ruzuku ambayo itakuwa imewekwa kwenye mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira haya ambayo tunayazungumza leo nataka nishauri. Jambo la kwanza kwa kuwa lazima tuwe na mbegu zetu sisi kwa sababu tunaingia kwenye ushindani wa masoko, lazima Wizara wapeleke fedha za kutosha kwa Wakala wa Mbegu. Hata hivyo, sisi tuna Taasisi za Serikali zikiwemo Magereza, Magereza wana maeneo makubwa tofauti na maeneo wanayoyatumia. Leo tunazungumzia uhaba wa mafuta. Mheshimiwa Waziri katika hili hatuhitaji muujiza, narudia tena kwa siku nyingine leo hatuhitaji muujiza, tunahitaji waliopo kwenye nafasi leo, waweze kuonyesha dhamira zao za dhati kwamba fedha, hata wakiamua leo kuwekeza kwenye Magereza tano tu, tunapozungumza uhaba wa mafuta leo hatutazungumza tena. Tutakuwa namna gani tuuze nje kwa sababu hizi taasisi nguvu kazi wanayo, ni wao kuwawezesha nyenzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Magereza kama ya Namanyele pale Kitete wako tayari kufanya kazi, ile ardhi imepimwa na hapa Waziri ametuambia vizuri, huwezi kuboresha kilimo kama hujawekeza kwenye kupima udongo. Tumeona ametueleza hapo kwamba kuna fedha imeenda kidogo, tuone kwenye kupima udongo, wakipima udongo, watajua ni mbegu gani inafaa kuweza kuzalisha kwenye hilo eneo na hiyo hatutafanya kama sasa hivi ambavyo tunavyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo mengi wakiona kwamba Singida wamelima vizuri alizeti, leo wamepata sisi tulipata shida ya mahindi, anaona ngoja nilime alizeti. Kama Wizara imefanya utafiti watamwambia eneo lako linafaa kwa ngano na sisi tunakutafutia soko, ndiyo wajibu wa Serikali kuwasaidia wakulima. Leo mtu akiingia kwenye kilimo inakuwa kama adhabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri akipewa fedha hii tunaamini mkulima yule wa chini ndiyo ambaye sisi Wabunge tunataka akafanikiwe. Kama ni ununuzi uanze leo, huu ni msimu wa mavuno, Nkasi tunataka tujue soko la uhakika la wakulima wa Mkoa wa Rukwa katika zao la mahindi, ile ndiyo siasa yetu, ile ndiyo pamba yetu, ile ndiyo madini yetu kwa Mkoa wa Rukwa. Hatutaki itokee kama mwaka jana na lazima utaratibu uwekwe, isiwe kwamba ikitokea balaa sasa ndiyo tunaanza kusema

tunamwomba Mheshimiwa Rais, hapana. Lazima tupate mpango wa Serikali, unapofika msimu wa mavuno Serikali wamejipangaje, soko liko wapi, kama hawawezi kununua, lazima mtafute soko nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wameenda kujenga kule Bandari, ukiziona zile Bandari Kabwe, Kalema hazionekani faida yake. tunataka tutumie zile bandari tupeleke mahindi yetu Congo na Burundi ili iwasaidie Watanzania wa Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Aida Khenani, kwa mchango wako.

Nilimwita Mheshimiwa Lucy John Sabu, wakati huo Daktari Charles Stephen Kimei, Mheshimiwa Francis Isack Mtinga na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud wanajiandaa.

**MHE. LUCY J. SABU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii ili niweze kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi. Kiupekee nimpongeze kwa kutoa pikipiki 7,000 na vitendea kazi kwa Maafisa Ugani, nina imani itawezesha kufanya kazi kwa weledi mkubwa na kuweza kuwafikia wakulima na kutatua changamoto zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 imeahidi ajira zisizopungua 8,000,000 na tunatambua sote changamoto ya ajira iliyopo kwa vijana. Nimepitia Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo, nimefarijika zaidi nilipoona vijana tumeguswa kupitia bajeti hii. Nichukue nafasi hii kuwapongeza Wizara ya Kilimo, kiupekee kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Hussein Bashe; Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara. Nina imani kupitia mradi huu ambao unaenda kuanzishwa hususan kwa vijana tutaweza kunufaika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze, kupitia bajeti tumeona kuna mradi unaenda kuanzishwa unaitwa Jenga Kesho Bora *(Building a Better Tomorrow)* Mradi mahususi kwa ajili ya vijana ambao wanaenda ku-*fund,* watatoa mtaji, watatota ardhi, watatoa mbegu, mafunzo, lakini pia watatafuta masoko kwa ajili ya bidhaa za mradi watakaouanzisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mradi huu, Mheshimiwa Waziri atakuwa shahidi wakati anautangaza kwenye mitandao ya kijamii, aliona namna gani vijana wengi wamevutiwa nao na wapo tayari kushiriki katika mradi huo. Nimefarijirika zaidi nimeona fedha imetengwa kiasi cha bilioni nne

ambayo itakwenda kuwasaidia vijana hawa ili waweze kufanya mradi huu kwa ubunifu wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ushauri wangu katika maeneo mawili hususan kwenye huu mradi. Nimeona mradi huu kwa majaribio utaanza Dodoma. Ningependa kushauri, Mheshimiwa Waziri tunaomba mradi huu usambae kwa nchi nzima ili vijana wengi waweze kunufaika. Pia tungependa kushauri hususan namna na utaratibu ambao utawekwa kwa ajili ya vijana au walengwa waweze kushiriki mradi huu, ningeshauri uwekwe utaratibu mzuri ambao vijana wengi waweze kuchaguliwa wale walengwa ambao kweli wanayo *interest* ya kufanya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii hususan kwa Mkoa wetu wa Simiyu nimpongeze Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa yeye ameshatoa mashamba na mwaka jana kuna vijana ambao walipewa mashamba na wameshaanza ninaomba tu Mheshimiwa Waziri ikikupendeza basi kwenye hiyo Bilioni Nne na Mkoa wa Simiyu uweze kutuona ili tuweze kunufaika na mradi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kuwaomba, niliona mwaka huu kwa mara ya kwanza kuna vijana walipelekwa kwenye maonesho ya Dubai na Uturuki, ninawaomba Wizara waendelee na utaratibu huu wa kuwajengea uwezo lakini vijana wengi waweze kujifunza wenzetu huko nje wanafanya kilimo cha aina gani ili tuweze kunufaika lakini pia vijana wengi waweze kujiajiri katika sekta hii ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, ahsante sana Mheshimiwa Lucy John Sabu lakini zaidi kwa kuzingatia muda. Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nianze kwa kwa kukushukuru wewe kwa kunipa fursa hii. Pia ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayofanya katika nchi yetu ikiwa ni pamoja na kutuletea bajeti hii ya kilimo ambayo ni ya kimapinduzi, nashukuru kwamba Mheshimiwa Waziri ametupitisha kwenye awamu tulizopitia za dira mbalimbali za kuendeleza kilimo, naamini mpango huu unaleta mapinduzi kwa sababu unazingatia mambo muhimu sana ya kimkakati na dira na naamini kwamba Awamu hii ya Sita itakwenda kubadilisha sasa kilimo hiki ambacho kitakuwa kimewaondolea asilimia zaidi ya 65 wananchi wetu wengi umaskini. Namshukuru pia Waziri na nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake pamoja na uongozi wa Wizara yote kwa kazi nzuri na kwa wasilisho zuri la bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na machache ambayo ni ya haraka haraka kwa sababu muda mfupi. Kwanza niseme kwamba ni vizuri katika kutekeleza tujue kwamba tunataka kupata tija ya haraka, kupata tija ya haraka ni lazima tuangalie Serikali ifanye tathmini ya mazao ya kimkakati kwa kila Mkoa. Siyo kila mkoa una *comparative advantage* zinazofanana. Unaweza ukazalisha mahindi kule Rukwa kwa bei nafuu sana ukayauza kwa tija sana kwa hiyo ikawa ni nzuri, lakini ukaanza kuweka tu kila zao liende kila mahali ukapeleke korosho kule Kilimanjaro itakuwa haifai. Kwa hiyo, lazima tuainishe kwamba Mikoa hii wale wenzetu walifanya hivyo, Mikoa hii kwa ardhi yake itafaa kwa mazao *one, two, three* au moja la kimkakati na lingine linaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Kilimanjaro sisi zao letu la kimkakati kiasilia lilikuwa ni kahawa, lakini kwa sababu ya uzembe tuliofanya hapo katikati huduma za kiugani zikapotea ile kahawa kule sasa imekuwa haioti tena, hasa kule Vunjo. Kwa hiyo, sasa tumeanza kuingia kwenye mazao mengine hasa *horticulture* mazao ya mbogamboga, matunda na maua na kadhalika. Kwa hiyo, sasa naomba hivi katika mpango mkakati huu uliokuja wa kujenga maghala madogo madogo ningeishauri Serikali iende iangalie yale maghala yaliyokuwa yanamilikiwa na Vyama vya Ushirika madogo madogo kwa kila Kijiji halafu ijaribu kuyaboresha yale maghala na kuyaboresha hasa siyo kuyaweka tena kuhifadhi kahawa ni kuhifadhi mbogamboga, ndizi ndiyo zinauzika ndiyo zenye tija, ina maana muweke majokofu kwenye yale maghala ambayo siyo makubwa lakini yanaweza kutosheleza kuhifadhi mazao haya ambayo sasa hivi ndiyo yamechukua nafasi ya kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba kwa vile sasa tulizembea kahawa ikafa kule kwetu, basi wale ambao wanaotaka kuendelea kuzalisha kahawa basi tuwape mbegu za kahawa, miche ya kahawa bure. Waziri alituahidi naamini itatokea hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuseme kwamba tatizo kubwa katika kilimo ni kwamba tunazalisha kabla hatujajua bei. Kwa hiyo mbolea ikipanda bei wewe unatumia gharama kubwa kununua mbolea ile lakini hujui kwamba utaenda kuuza namna gani, bei utakayopata ukiuza ile kahawa yako au mahindi ni shilingi ngapi. Mimi nafikiri kama mwenzetu alivyosema pale kwamba ni vizuri Serikali itafuta masomo halafu iwe inatoa zile bei, inatangaza zile bei ambazo imepata kule nje. Inatangaza bei elekezi kwa kusema kwamba ukilima mahindi au ukilima mbogamboga hizi au ukilima kahawa au pamba kwa msimu huu tuna kuhakikishia kwamba tumeshapata wanunuzi *contract buyers* ambao watakubali kukulipa shilingi fulani, kwa hiyo *margin* utakayoipata kwa *cost management* ambayo tumefanya utapata *margin* hii, na ukimwambia mkulima atanunua mbolea bila hata ruzuku kwa sababu anajua kwamba tayari ukifuata ile bei ya mbolea na *input* nyingine kwenye ile bei ambayo utapata ni faida. Sasa sisi tunazalisha halafu

tunakwenda kupata hasara hata ukiweka ruzuku halafu ukienda kuuza kwa hasara *it doesn't help* na tumeshapoteza ruzuku yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite kwa mfano sasa hivi suala zima la mahindi. *NFRA* ina mahindi mengi lakini bei za mahindi zimepanda zimefika mpaka shilingi 800 kule Arusha. Mimi nafikiri kwamba huu ndiyo wakati ambapo sasa *NFRA* isiuze kwa *middlemen* yale mahidi, mahindi yauzwe ili yamfikie mlaji moja kwa moja. Kwa sababu ukiuza kwa *middlemen* ina maana ile faida ya yale mahindi ambayo tumewezesha *NFRA* ikanunua itakwenda kwa wale wafanyabiashara wa kati. Kwa hiyo, naomba hilo lifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya kuangalia ununuzi, uuzaji wa mazao yetu kama pamba. Tunajikuta kwamba kwa sababu riba zilikuwa kubwa, zinaanza kushuka hapa lakini ni kwamba riba kwetu bado zipo juu sana na watu wanaouziwa mazao yetu ni wale ambao wana-*process* hapa kama pamba kutengeneza nguo. Kwa hiyo, tunaomba hivi ile Benki ya *TADB* iwe inawawezesha wale wanunuzi wenye viwanda vya ku-*process* mazao yetu hapa kupata mikopo kwenye riba kati ya Mbili mpaka Nne hivi ili waweze kununua kwa wingi na wakienda kuuza nje wao zile bidhaa walizo-*process* hapa waweze kuziuza kwa faida *in a way* ambayo ina ushindani, ndiyo tunasema sasa dira yetu sasa ni uchumi shindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kwamba hiyo haitawezekana kama watu watakopa wahifadhi hii pamba ya kuchakata mwaka mzima halafu riba inaongeza zile bei kwa hiyo baadaye itakuwa hawawezi kushindana wanapoenda kwenye soko la dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa naamni kwamba kweli bajeti hii ni bajeti ambayo ni tofauti, ni bajeti kabambe, ni bajeti itakayotekeleza dira ambayo inayosadikika. Isipokuwa naomba Mungu aniweke hai mpaka mwaka 2030 ili nione mafanikio haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana lakini pia Mungu amuweke hai na Waziri pia. Mheshimiwa Francis Isack Mtinga. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika bajeti ya Wizara ambayo tumezoea kusema uti wa mgongo lakini leo Mwijage ameongeza ni Bajeti ya Taifa, kwa sababu tunagusa wananchi wa Tanzania kwa asilimia kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niwape pongezi Mawaziri, Waziri wa Wizara hii na Naibu Waziri wake, hawa vijana mimi nawafahamu akili ya Mheshimiwa Bashe naijua vizuri, mimi nilikuwa bosi wake nikiwa Katibu Mkuu

wa Vijana, ana akili nyingi sana hapa ametumia robo tu. Kwa hiyo, nina hakika kama bajeti yake hii itatekelezwa yote tutafika mahali tutaongeza fedha nyingi zaidi kwa jinsi ambavyo wanaupiga mwingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mwanasheria Antony pia namfahamu, kwa kweli Mama amechagua vijana hawa ili baadaye tuwe na *model,* kwamba vijana wakipewa nchi au wakipewa kazi wanaweza kuifanya. Nami sina wasiwasi kabisa na ninyi vijana wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitagusa kwenye jambo ambalo linagusa sana Jimbo langu pia linagusa nchi kwa maana ya mbegu za mafuta ya kula na hususan alizeti. Tunalo tatizo kubwa la mafuta, tunalo ombwe kubwa la mafuta na tunaagiza nje ya nchi wakati sisi ni nchi ya wakulima. Katika kulima mbegu hizi Mkoa wa Singida na hususan Jimbo la Mkalama ndiyo uti wa mgongo haswa wa kulima zao la alizeti. Kwa hivyo, ninakuomba Waziri jambo ambalo ulilianza mwaka jana la kutoa mbegu kwa mkopo lilikuwa ni jambo zuri, katika bajeti yako umesema tena kwamba utatoa mbegu lakini ningeomba sasa niseme machache ambayo yalikuwa ni kasoro kidogo kwenye ugawaji wa mbegu zilizopita ili mbegu hizi utakazogawa sasa ifanyike kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni aina ya mbegu, wananchi walitegemea sana wapate *Highsun*, tunajua kwamba *Highsun* ni mbegu inayotoka nje ya nchi, umesema kwamba *ASA* watatutengenezea mbegu zetu wenyewe lakini ni *process* ambayo mbegu zitachukua muda kidogo, kama itakuwa bado katika msimu huu, ninaomba mbegu utakazoleta *highsun* iwepo kwa sababu wananchi wanahitaji *highsun* ili waweze kuzalisha mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbegu iliyokuja pia wameitoa kasoro kidogo, inatoa matawi mengi kwenye mti mmoja wa alizeti na vichwa vinakuwa vidogo, kwa hiyo, wananchi wangu hasa wa Mkalama ambao ni wakulima wakubwa wa alizeti wamelalamika na hii mbegu. Kwa hiyo, ninakuomba sana katika zoezi linalofuata hili tulirekebishe mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ugawaji wa hizi mbegu, ulitoa mbegu vizuri ukatupeleka Mkoani lakini hamkutoa waraka mzuri jinsi gani mbegu hii igawiwe. Sehemu nyingine Maafisa Ugani wakawa wanasema lazima ulipie kwanza, sehemu nyingine wanasema ukopeshwe, kwa hiyo kukawa na mchanganyiko hapa, hii imesababisha mbegu nyingi imebaki kwa sababu hakukuwa na waraka mzuri ulioeleza jinsi gani mbegu hii igawiwe au ikopeshwe. Kwa hiyo, nikuombe katika mbegu zinazofuata sasa jambo hili uliangalie kwa umakini sana ndugu yangu Mheshimiwa Waziri wa Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni miundombinu. Umesema hapa kutakuwa na miundombinu ya kutosha, ruzuku na kila kitu, lakini ndugu

zangu kutegemea mvua, mbegu hii ambayo imegawiwa pamoja na kasoro zake lakini nyingi imepelea mvua. Kwa hivyo, kilimo cha kutegemea mvua hakitufai kwa sasa katika nchi yetu hii ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna ardhi ya kutosha, mabonde ya kutosha, mfano mimi katika Jimbo langu la Mkalama ukienda Kata ya Mwangeza - *Dominic* pale kuna eneo wanalima vitunguu, wakipata bwawa wakichimbiwa visima pale wanaweza kuzalisha muda wote wa mwaka. Pia kuna *scheme* ya umwagiliaji pale Mwangeza imekufa muda mrefu ikifufuliwa ila katika hizo *scheme* ambazo umesema utaziweka naomba kabisa Mwangeza katika ufufuaji wa *scheme* usije ukaicha katika Jimbo langu la Mkalama. Hii itatusaidia sana kuhakikisha tunapata mbegu za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri *block farming* ulikuwa muumini wa hili jambo, ulipokuwa *backbencher* ndugu yangu Bashe, nikiwa mtaani kila ukisimama nilikuwa najua aidha utaongelea *block farming* ama utamuandama Makamu wa Rais sasa kuhusu kwenye mambo ya fedha akiwa Waziri wa Fedha, hizo zilikuwa ajenda zako. Sasa Mungu ni fundi kweli kweli alivyojua unasema sana mambo *block farming* akakupa Unaibu, lakini ukawa unasingizia huingii Baraza la Mawaziri, Mungu alivyofundi akakuongezea Uwaziri. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa usipoe Mheshimiwa Bashe ndugu yangu, *block farming* ndiyo itakuwa ukombozi. Umesema tu pale kutakuwa na *block farming* lakini kwenye alizeti hujasema vizuri. Mimi nikushauri kwamba angalau kila Kata katika nchi hii hasa kwenye Jimbo langu la Mkalama, kule kuna *block farm* ambayo wale Maafisa Ugani uliowapa nyenzo, uliowashonea na jezi na kila kitu anakuwa ofisi yake ni *block farm* iliyopo kwenye Kata. Wanaomiliki ile *block farm* wanakuwa vijana wa kike na kiume ndani ya Kata. Kwa hiyo, uta-*solve* mambo matatu hapa, kwanza utatengeneza ajira kwa vijana, pili utazalisha mbegu za uhakika na tatu utawapima vizuri Maafisa Ugani wako kwa sababu watakuwa na ofisi ndani ya Kata ambalo ni shamba kubwa la *block farm*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ninakuomba katika hizi *block farm* peleka kwenye Kata hasa hizi za alizeti hapo utakuwa umetusaidia sana katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile viwanda vyetu vya mafuta, viwanda vikubwa kama *Mount Meru* na viwanda vingine, hawana mashamba makubwa ya kulima wanategemea wakulima wadogo wadogo. Naomba ufanye kama yalivyo mashamba ya miwa kwenye viwanda vya sukari. Kiwanda kinakuwa kina shamba *outgrowers* wanajazia tu. Kwa hiyo, viwanda vikubwa wapewe hekta za kutosha hata 10,000, wapewe na waambiwe walime, kwa hiyo anakuwa na mbegu za kiwanda lakini wananchi wanakuja kujazia kwa hiyo viwanda vyetu vitafanya kazi

*throughout the year* na hii itatusababisha sisi tuweze kupata mafuta ya kutosha na tuokoe fedha zetu hizi ambazo tunazipoteza nyingi sana fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo linguine….

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru naomba niunge mkono hoja lakini nitakuona kuhusu suala la masoko Mheshimiwa Waziri ili tuliweke vizuri, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimuita Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud wakati huo wafuatao wajiandae. Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mheshimiwa Katani Ahmad Katani, Mheshimiwa Emanuel Peter Cherehani na Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii adhimu kumpongeza sana na kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa dhamira yake ya dhati kuhakikisha kilimo cha Tanzania kinakua na kuhakikisha kwamba sekta za uzalishaji zinapatiwa fedha ili kuinua uzalishaji nchini katika kupambana na hali ya uchumi wetu, kuingiza fedha za kigeni, kutatua matatizo ya wananchi wetu na hasa wakulima ili waweze kulima kilimo chenye tija na waweze kupata faida ya jasho lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo limedhirika wazi baada ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kukabidhi vitendea kazi kwa Maafisa Ugani wetu pamoja na vifaa mbalimbali ikiwemo vifaa vya kupimia afya ya udongo. Hiyo ni dhamira ya dhati na huo ni mwanzo mzuri wa kuona kwamba sasa tunakwenda kupiga hatua katika sekta hizi ya kilimo na uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo napongeza pia mpango wa Wizara ambao unakwenda kutoa ruzuku kwa wakulima wetu hivi karibuni. Pamoja na na kutoa hizo ruzuku bado naishauri Serikali kuwekeza zaidi kwenye viwanda vya mbolea vya hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji umeanza kwa kiwanda cha mbolea na vingine vilianza huko nyuma, naishauri Serikali iendelee na uwekezaji kwa wananchi wetu wa hapa ndani pia wawekeze kwenye sekta hii ya viwanda vya mbolea, kwa sababu, mbolea ni silaha kubwa katika kilimo popote duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakapotokea changamoto nyingine zozote duniani kwenye sekta hii ya mbolea basi na sisi tuwe na akiba yetu ya mbolea hapa nchini tuweze kukidhi mahitaji yetu ya wakulima wetu ndani ya

nchi, ikiwemo kupanda kwa bei ya mbolea mara kwa mara, kupanda kwa mambo mbengine yatakayojitokeza ya kimazingira na mabadiliko ya tabianchi, lakini na sisi tukiwa na viwanda vyetu vya mbolea hapa nchini, ambavyo vitakwenda kuzalisha mbolea zinazolingana na udogo wa nchi yetu kutokana na mazingira tofauti tofauti ya nchi yetu, itakwenda sana kumkomboa mkulima wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu, Mheshimiwa Waziri amegusia kuhusu kuzalisha mbolea asili, nami nakubaliana naye katika kuzalisha mbolea asili. Mbolea asili ziende pamoja na viuatilifu asili. Tunavyo viuatilifu vyetu asili na Wizara kupitia vitengo vyake vya utafiti vimeshafanya utafiti kwa baadhi ya viuatilifu, ni vema viuatilifu hivyo vikatangazwa wananchi wakavijua na kuweza kuvitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta hii ya kilimo kumeongezwa fedha kwenye utafiti, huduma za ugani, umwagiliaji, tunaomba katika fedha hizi zilizoingizwa nyingi kwenye bajeti hii ya kilimo, bado tunahitaji fedha zaidi za uwekezaji mkubwa katika kilimo. Fedha hizi zilizoingizwa zilizowekwa kwenye bajeti tunaomba zitoke kwa wakati, kwa sababu zinapotoka mwisho wa mwaka kilimo kinakwenda kwa miongo na bado hatujajiweka sawa kwenye umwagiliaji, hivyo inapokuja fedha miongo ile imeshapita, fedha zile zinakuwa sasa zimekuja mwisho. Tunaomba fedha zije kwa wakati zikafanye kazi kwa wakati kulingana na mazingira ya kilimo kwa Mikoa tofauti, hali ya hewa tofauti na kilimo tofauti katika mazingira tofauti.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea, niongelee kuhusu utoshelevu wa mafuta. Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imejipanga kuhakikisha kuna utoshelevu wa mafuta nchini. Nami naipongeza Wizara kwa mikakati mbalimbali. Tunaomba sote tu-*support* Wizara ya Kilimo kufuatia watendaji wake, tuunge mkono juhudi za Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo mambo ya mafuta, Wizara imewekeza hivi sasa kuliimarisha zao la nazi kwa kutoa miche 2,000. Miche 2,000 ni kidogo mno, kwa sababu kuna baadhi ya maeneo mafuta wanatumia tu kwa sababu hawana la kufanya, lakini matumizi makubwa ni nazi. Kwa hiyo, tukiimarisha hili zao la nazi, litakwenda kupunguza ule upungufu wa mafuta uliopo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna haja ya kujipanga katika mazao ya biashara na mazao ya kukidhi mahitaji yetu ya nchi. Kwenye mazao ya biashara tuangalie soko liko wapi? Mazao gani yana soko? Halafu turudi kwa wakulima, tuhamasishe wakulima wetu walime vipi. Hapo hapo tuimarishe uhifadhi na vifungashio ili mazao yetu yawe na ubora. Vifungashio pia ni sehemu ya kuvutia biashara kwani biashara ipendezayo ndiyo inunuliwayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiacha suala la vifungashio, sasa niipongeze Serikali kwa kuwekeza mtaji mkubwa kwenye Benki ya Kilimo. Benki hii itakwenda kumkomboa mkulima mdogo. Tunaiomba Serikali, kila inapoweza kuongeza mtaji kwenye Benki hii, iendelee na juhudi za kuongeza mtaji ili tuone wakulima wetu wananufaika na kuweza kukidhi mahitaji ya kilimo ikiwemo vitendea kazi ili wavutike na biashara hii ya ukulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubalina na Wizara katika kuuboresha ushirika, ufanyiwe kazi kwa haraka kutatua zile changamoto na pia kutazama udhaifu uliopo kwenye ushirika na kuyaboresha kwa muda huu muafaka ili ushirika uweze kumkomboa mkulima wetu mdogo ambaye anahitaji sana nguvu ya kusaidiwa na Taasisi hii ya Ushirika ambayo ndiyo taasisi tunayoiona kwa sasa inayoweza kumpunguzia matatizo mkulima katika kuhifadhi mazao yake ambayo yanapotea na pia kumtafutia soko la uhakika katika kuuza mazao yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana juhudi zinazofanywa na Wizara kuwekeza Ofisi za Umwagiliaji katika Halmashauri au Wilaya zote za Tanzania. Tunachoomba kwa Mheshimiwa Waziri, hao wahusika wapewe ushirikiano na Wizara na Taasisi zilizopo katika maeneo husika ili waweze kufanya kazi zao kwa uadilifu na kumsaidia mkulima katika sekta hii ya umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikimalizia, niseme kilimo ni biashara, kilimo ni utatuzi mkubwa kwa wananchi wa Tanzania. Naiomba Serikali, kila itakapokuwa na uwezo, basi iwekeze katika sekta hii ya kilimo. Tumpe moyo Mheshimiwa Rais wetu, kwa dhamira yake ya dhati ya kuinua sekta hii na Mheshimiwa Waziri anajipanga vizuri, tunaomba tumpe *support* kabisa ili tuweze kumkomboa mkulima mdogo aweze kupata tija kwa anachokivuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud. Nilimwita Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa jioni hii kuchangia Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nimshukuru Rais wetu wa Awamu ya Sita kwa busara na hekima ya kuwagawia wakulima wetu wa korosho pembejeo bure, kitu ambacho kimesababisha katika Wilaya yetu ya Tunduru kuongezeka kwa uzalishaji kutoka tani 14,000 mpaka kufika tani 25,000. Tunashukuru sana, lakini kipekee tumshukuru Waziri, tulipompa wazo hili kwa kweli alilichukua, akalibeba, akamshirikisha Rais, akakubali matokeo yake jambo hili likatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kutekelezeka kwa jambo hili, kuna jambo naomba Waziri unisikilize kwa umakini. Utaratibu wa ugawaji umekuwa tatizo katika vijiji vyetu. Ugawaji uliotumika msimu uliopita walipewa mamlaka watu wa ushirika peke yake na matokeo yake malalamiko yamekuwa mengi kwa wakulima, kwani wale waliofaa kupewa pembejeo hawakupewa. Kwa hiyo, naomba sana safari hii ugawaji huu ushirikishe Serikali za Vijiji, Serikali za Kata, muunde tume, kamati kwenye vijiji na ikiwezekana basi wale wanufaika watakaopata pembejeo zile basi wapitishwe na Mkutano Mkuu wa Vijiji ili kila mmoja ajue ni nani amenufaika na ikiwezekana mbandike wale wanufaika kwenye mbao za matangazo kila kijiji ili ionekane namna ambavyo pembejeo zile zimegaiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, jambo hili ni muhimu ili kuondoa lawama ambazo zimetapakaa katika vijiji vyetu kwa namna ambavyo hatukutenda haki katika kugawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, hili suala la pembejeo lipo kwenye jambo letu lile la *Export Levy.* Nakuomba Waziri, sikusikia jambo la *Export Levy* kulirudisha kama wadau walivyokuwa wamekubaliana. Wewe unafahamu *Export Levy* ilianzishwa na wadau wa zao la korosho ili kulifanya zao hili lifanye kazi vizuri, lihudumiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unafahamu mara ya mwisho tumeondoa *Export Levy,* uzalishaji ulipaa na ukaja kushuka baada ya kuondoka mpaka kufikia asilimia 33. Ili pembejeo tuweze kugawa bure, ni sehemu ya *Export Levy.* Kwa sasa *Export Levy minimum* ni Dola 160 kwa tani, kwa maana ya kilo moja shilingi 372/= ni *Export Levy* ambayo inakwenda Serikalini. Tunaomba Sheria ile ya asilimia 65 irudi kuhudumia zao la korosho. Hata wakulima sasa hawataweza kukatwa ile shilingi 50/=; shilingi 25/= ya kuhudumia Bodi ya Korosho na shilingi 25/= ya kuhudumia utafiti, itatokana na ile *Export Levy* na mambo mengine yatakwenda vizuri. Naomba sana hii Sheria tusiisahau, tuirudishe, tufanye kazi iliyokusudiwa na wadau kwa ajili ya kuhudumia zao la korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, Mheshimiwa Waziri nikushukuru sana kwa kumteua Mrajisi wa Ushirika ambaye ana moyo wa kuusaidia Ushirika. Ushirika ndiyo kiini pekee cha kuweza kumsaidia mkulima, lakini Ushirika huu unakwamishwa na watu wa chini, kwa maana Mrajisi na *Head Office* wana nia nzuri ya kuwasaidia wakulima, lakini watendaji walioko chini, kwa kweli imekuwa ni tatizo. Nadhani mara ya mwisho nilikwambia yaliyotokea Tunduru, kuna wadau walikubaliana kuchangia Timu ya Tunduru korosho kupitia tozo kwenye Vyama vya Msingi, ambapo kila Chama cha Msingi kinachangia Shilingi 2/= kwa kila uzalishaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TAMCO* nao Chama Kikuu kinachangia shilingi 2/=, wasafirishaji wa korosho wanachangia shilingi 2/= lakini mtunza ghala anachangia shilingi 1/=. Kwa bahati mbaya, ndiyo maana nazungumza

kwamba watendaji walioko chini, hawaisaidii Serikali kwa maana ya Tume ya Ushirika kufanya kazi vizuri kwa maendeleo ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile hesabu inayokusanywa kwenye Vyama vya Msingi, kwenye Chama Kikuu haioneshi mahali popote kwenye hesabu zao za vitabu. Kwa maana hiyo, ni kwamba kama haioneshi kwenye hesabu zao na ile hesabu haipelekwi kwa wananchi wakajua kwamba Chama chetu cha Msingi kimechangia kiasi kadhaa kwa ajili ya maendeleo ya michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri uende ukakague Vyama vile vya Msingi kuona fedha hii inakwenda wapi? Kule inakokwenda haifanyiwi hesabu ya aina yoyote. Sasa hivi huu ni msimu wa nne, wamekusanya lakini haioneshi kwenye vitabu vyao, wala hawasomi hesabu kwa wanachama wao kuonesha fedha hii inachangwa na imepelekwa kwenye michezo. Naomba sana jambo hili limekuwa ni kero kwa wananchi wa Tunduru, hawaelewi ni kwa nini hawataki kuonesha hesabu hii kwenye Vyama vya Msingi na kutoa ripoti kwa wenye Vyama? Huko inakokwenda, anakagua nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana jambo hili Mheshimiwa Waziri alichukulie kwa umakini zaidi kwa sababu wananchi wa Tunduru bado wana kilio na jambo hili ingawa tulianzisha wenyewe kwa mapenzi mazuri ili kuhakikisha kwamba timu yetu inasonga mbele kwa ajili ya maendeleo ya Tunduru, lakini bado hili jambo halijakaa vizuri mpaka sasa hesabu hakuna, na huko inakokwenda hiyo fedha, hesabu haioneshwi, na hakuna mtu yeyote, vikao hawafanyi. Hili jambo hili ni kero kwa wananchi wa Tunduru, naomba tuweze kuhakikisha kwamba linafanyiwa kazi. *(Makofi)*

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa. Ndiyo Mheshimiwa.

**T A A R I F A**

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji anayeongea, amezungumza vizuri, lakini taarifa ama mapato ya timu ya mpira yoyote, hayasomwi kwa wananchi ama wakulima isipokuwa yanapelekwa kwa Wajumbe wa Timu ama *management,* kwa timu zote Tanzania nzima, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpakate, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni sahihi, taarifa ya timu inakwenda kwa wadau, lakini fedha hii inachangiwa kutokana na zao la korosho ambalo wananchi wanachangia.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Pamoja na kwamba muda wako umekwisha, nimekuongeza dakika nyingine ili uweze kuweka hoja yako vizuri.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba aelewe kwamba, ninachokisema, Vyama vya Msingi vina wanachama wake ambao ni Wajumbe halali wa Mkutano Mkuu; hawajaambiwa mapato yao, sehemu ya ushuru ya shilingi 65 inakwenda kuchangia mpira, na watoe hesabu kwamba mwaka huu tumetoa shilingi fulani. Ndiyo tunayotoa hii bajeti kwamba mwakani tutachangia shilingi fulani kutokana na makisio yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo makisio hayaonekani kwenye vitabu vyovyote vya Vyama vya Msingi. Kwa maana hiyo, wanachama ambao ni wananchi wa kawaida wanapata mashaka, fedha hii inakusanywa kwenye Vyama vya Msingi, wale wakulima hawaambiwi. Hatutaki hesabu ya mpira, tunataka hesabu kwenye Chama cha Msingi ioneshe, Chama cha Msingi kinachangia Shilingi ngapi kwenye maendeleo ya michezo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate. Nilimwita Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani, wakati huo Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma na Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya wanajiandaa.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu. Vile vile nakushukuru wewe kwa kunipa fursa. Nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitamshukuru kwa dhati kabisa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan hususan kwa sisi wakulima wa korosho kwa kutupa pembejeo bure kwa mara ya pili mfululizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi inayofanywa na Waziri wa Kilimo wa sasa, kama bajeti hii ambayo leo anaiomba ya Shilingi bilioni 751 itatoka kutoka Wizara ya Fedha, naamini Taifa hili kwenye kilimo tunakwenda kufanya mapinduzi makubwa sana. Tunajua dhamira yake ya dhati, yeye na Naibu wake pamoja na watendaji wake wa Wizara ya Kilimo, kuanzia Katibu Mkuu Mzee Andrew Masawe; Naibu Katibu Mkuu, Profesa Siza, wanafanya kazi kubwa kuhakikisha wakulima wa Tanzania wanakwenda kupata tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye korosho, Waziri amefanya jambo kubwa na sina namna zaidi ya kumpongeza. Mwaka huu tarehe 5 Mei, 2022 kwenye Kijiji changu kimoja, Kata yangu moja ya Nanyanga amefanya uzinduzi pale wa upuliziaji wa korosho. Kampuni moja inayoleta dawa; kampuni ya *Benz* imejitolea kutoa mafunzo kwa wakulima jambo ambalo

halikupata kutokea. Hii inaonesha *commitment* ya Waziri na wazabuni walioleta dawa kuonesha namna gani viuatilifu vyao vina ubora. Wameamua kwenda kutoa mafunzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Wizara kwamba mafunzo yale yasiwe zimamoto, yaende kusambazwa nchi nzima, ikiwezekana kwa wazabuni wote wa dawa, ili kama kuna mkulima atashindwa kupuliza dawa vizuri, tujue kwamba Serikali iliwajibika pamoja na wazabuni waliwajibika. Jambo mlilolifanya ni kubwa na hili lifanyeni sehemu zote zinazolima korosho, mtakuwa mmesaidia wakulima sana, maana watu wanapata elimu ya upuliziaji. Maana yake mnapoleta viuatilifu hivi vina mabadiliko ya majina, wakati mwingine wakulima hawajui kwamba zile dawa *ingredients* ni sawa, wanadhani labda dawa zina matatizo. Mnapoamua kuleta wazabuni, wakaamua kutoa mafunzo, mnakwenda kuongeza uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Waziri, kama watafanya jambo lile mwaka huu wa 2022, mwaka jana, 2021 waliongeza uzalishaji kwa asilimia 40, mwaka huu wanakwenda kuongeza kwa asilimia 100. Lifanyeni kwa nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kulikuwa na uzinduzi wa ugawaji wa pembejeo, umesimamiwa na Mkuu wetu wa Mkoa wa Mtwara, lakini ukiusoma mwongozo uliotolewa na Bodi ya Korosho, wanaokwenda kusimamia ugawaji, Wenyeviti wa Serikali ya Vijiji hawamo; Madiwani ambao ndio Wenyeviti wa Kamati za Maendeleo ya Kata hawamo. Ushauri wangu kwa Serikali Mheshimiwa Waziri, huwezi kwenda kusambaza pembejeo ukamtoa Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji. Yeye ndio anawajua wakulima halisi kuliko hata watu wa Vyama vya Msingi. Watu wa Vyama vya Msingi wakati mwingine kwa sababu ya ukata, wanaweza kuchomekea mkulima ambaye hayupo ilimradi mtu apate chochote maisha yaende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapomshirikisha Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji, unapomshirikisha Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Kata ambaye ni Mheshimiwa Diwani, maana yake mnakwenda kutengeneza uwiano wa kujua kwamba mazao haya dawa hizi zinakwenda kumfikia nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kabisa Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji ndio anawajua watu wa eneo lile. Mheshimiwa Diwani wa Kata husika ndio anawajua watu wa eneo lile. Leo mnaandaa Kamati za Ugawaji wa Pembejeo Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji hayumo na Diwani wa Kata hayumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha kesho hapa, atoe tamko kabisa kwa nchi nzima, Wenyeviti wa Serikali ya Vijiji Waheshimiwa Madiwani ni lazima wawepo kwenye ugawaji wa pembejeo na wawepo kwenye mfumo ule. Naomba sana kwenye jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ana kazi kubwa sana na namna pekee ya kusaidia mzigo huu, ni lazima akae na Naibu Waziri wake na Naibu Waziri ni Mwanasheria. Sheria za Ushirika ziko ovyo. Mwaka 2021 Waziri amekamata watu na pembejeo Tunduma. Matokeo yake kwa sababu tuna sheria ambazo haziwasaidii, wale watu ni wahujumu uchumi kama wahujumu uchumi wengine. Pembejeo za bure zinapotolewa na Mheshimiwa Rais, dhamira yake ni kumsaidia mkulima. Anapopatikana mtumishi mmoja, anakwenda kuiba pembejeo, unakwenda kuikamata Tunduma, unamfungia ofisini kwako mpaka saa 7.00 usiku, haitakusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iletwe sheria hapa mahususi kabisa tutakayokwenda kuipitisha Wabunge, mtu anayekwenda kuhujumu pembejeo za mkulima, huyu awe ni mhujumu uchumi kama mhujumu uchumi mwingine. Hata ikiwa ni mifuko miwili, tutawasaidia wakulima na tutakomesha huu wizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashawishi Wabunge wenzangu, tumekaa hapa, Maafisa Ugani wetu wote wanasimamiwa na TAMISEMI, lakini ndio Maafisa Kilimo tuliokuwa nao vijiji vyote na kata zote. Naomba Wabunge wenzangu tuone namna ya kuisaidia Wizara, Maafisa Ugani wote warudi Wizara ya Kilimo, wasimamiwe na Wizara ya Kilimo. Hii itatusaidia sana. Mtakapotoa maelekezo yataenda moja kwa moja kuliko *contradiction* ambayo sasa tunaipata. Wako TAMISEMI, mnatoa maelekezo wakati mwingine watu wanashindwa kutekeleza majukumu yao kwa sababu hawajui wawajibike kwa nani. Kumbe ni watu walipaswa kwenda Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Kuchauka.

**T A A R I F A**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji. Ni kweli jambo analolizungumza kuhusu Maafisa Kilimo, kwani wao sasa hivi ndio Watendaji wa Kata. Yaani kwenye Mtendaji wa Kata, Mtendaji wa Kijiji akiondoka, nafasi inazibwa na Afisa Ugani kwa sababu ndio wanaoonekana wako *lose,* hawana kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Katani unapokea taarifa?

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa kwa mikono miwili kabisa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye suala la utafiti. Mimi nikupongeze Waziri, nimeona mmeongeza kutoka shilingi bilioni 7.35 mpaka shilingi bilioni 11.65. Kwenye jambo hili kwenye korosho tunakuta mnaweka

fedha ambazo zinakwenda kwenye utafiti. Sasa kama huku mmeongeza fedha zinakwenda kwenye utafiti, tunataka kwenye mjengeko wa bei sasa tusione makato yanayokwenda kwenye utafiti tena, maana hapa tunashawishi Wabunge wenzetu tupitishe bajeti hii.

Mheshimwia Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Mwijage, hii ni bajeti ya Taifa. Unapozungumza kilimo ambacho kinakwenda kuwanufaisha Watanzania zaidi ya asilimia 65 ni eneo ambalo angekuwepo Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Mchemba hapa, ningemwomba sana kaka yangu, katika Wizara ambazo bajeti zake alipaswa fedha zake apeleke zote, basi Wizara ya kwanza ingekuwa Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana huko aliko, wasaidizi wake kama wapo, namwomba sana Waziri wa Fedha, namwomba sana Waziri wa Fedha, namwomba sana Waziri wa Fedha, Wizara hii ya Kilimo bajeti hii iliyopangwa ipelekwe yote tumpime Mheshimiwa Bashe kwa fedha ambazo mtakuwa mmempa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wamezungumza wenzetu vizuri sana, kwa namna ulivyoichakata bajeti hii ya kilimo, kama mtapata fedha na ikasimamiwa vizuri, ndiyo kitakuwa kipimo sahihi, lakini kama tutapeleka fedha asilimia 46, asilimia 50, hatutampima Mheshimiwa Bashe wala Mheshimiwa Mavunde pale. Maana watakuwa na utetezi kwamba tuliomba Shilingi bilioni 751, tumepata Shilingi bilioni 300 na ngapi. Tumpeni Shilingi bilioni 751, tunaporudi mwakani hapa tuwe na kitu cha kumwuliza kwamba uliomba shilingi bilioni 751, umepewa, kilimo kimefika wapi? Uzuri wake wewe una makisio. Kila mahali ulipokwenda umeweka matarajio yako, umeweka maoteo yako. Maoteo yako hayatakwenda kutimia kama hizi fedha ambazo umeomba hazitakuja kutolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumwomba tena Waziri wa Fedha, kwenye jambo hili tujitahidi na Waheshimiwa Wabunge kuhakikisha fedha za Wizara ya Kilimo zisipungue japo shilingi ili tupime utekelezaji mzuri wa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, sasa aanze kuchangia.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nikuombe radhi sauti yangu sio rafiki kulingana na hali ya hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa nafasi hii ya pekee ya upendeleo ya kuweza kujadili

kwa mara ya kwanza Wizara ya Kilimo. Nimpongeze sana pia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wetu Samia Suluhu Hassan, kwa upande wa kilimo ametusaidia sana sisi wakulima. Kwa mara ya kwanza katika nchi ya Tanzania tumeweza wakulima wa pamba kupewa mbegu zenye thamani ya bilioni 16 bure bila kukatwa chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye upande huohuo wa pamba Mheshimiwa Rais ametoa dawa zenye thamani ya za zaidi ya bilioni 36 kwa nchi nzima, mikoa yote, ya zao la pamba bure, haijawahi kutokea. Kwa hiyo, niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Naibu Waziri wa Kilimo, pamoja na Makatibu Wakuu na watumishi wote kwa kazi nzuri wanayoitendea nchi yao, wanayowatendea wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimshukuru sana Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Tanzania, Dkt. Benson Ndiege. Kwa mara ya kwanza mwaka jana alipeleka magari saba kwa warajisi wasaidizi wa mikoa, amepeleka pikipiki 135 kwa Maafisa Ushirika. Hii yote ni kwaajili ya kuboresha wakulima, kwaajili ya kuboresha sekta za wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka niende moja kwa moja kwenye mchango wangu. Cha kwanza kabisa pamoja na mazuri yote wanayoyafanya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na viongozi wote, bado tuna changamoto kwenye Sheria ya Ushirika. Sheria ya Ushirika bado inahitaji marekebisho makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia bajeti ya Mheshimiwa Waziri yote sijaona mahali ambapo anaweza akaileta Sheria ya Ushirika Bungeni iweze kujadiliwa, iweze kupitiwa pamoja na Sera ya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunajivunia Mheshimiwa Bashe kuwepo pale na umahiri wake wa kazi, lakini bado uwezo wa utendaji wake wa kazi unaweza ukapotea kwa sababu, bado sheria ya ushirika si pana. Tunaomba sana hili suala la ushirika na Sheria ya Ushirika iletwe Bungeni ili tuifanyie marekebisho na tuweze kuiboresha ili iwe na makucha kwa ajili ya kushughulikia wabadhirifu wa fedha na mali za wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ugawaji wa pembejeo kama kwenye bajeti ilivyoandikwa; nataka nijikite kwenye mfumo mzima wa usajili wa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, Serikali inajitahidi sana kupeleka mbegu pamoja na dawa, lakini tuna changamoto ya kutowatambua tunaowahudumia. Tunatumia makisio ya tunaowahudumia lakini bado hatujawatambua tunaowahudumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Wizara imetoa pikipiki 6,000 kwaajili ya kwenda kwa wakulima wetu, lakini leo hii ukitaka uwaulize hata maafisa ugani wanahudumia wakulima wangapi hawawezi kukwambia. Mimi nilikuwa nashauri, na hata kwenye bajeti sijaiona; tupate mkakati mzuri wa kuwatambua wakulima, wa kuwajua wakulima mahali walipo na kuhakikisha kwamba mkulima wa Imala Makoye anayelima pamba yuko maeneo gani? Analima eka ngapi? Anazalisha kiasi gani? Pamoja na kwamba, tunapima udongo, lakini suala la kujua na kutambua mahitaji yake ni suala la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoa mfano hata sisi kwenye zao la tumbaku, kwenye zao la tumbaku mkulima huwezi kumpelekea bidhaa kama haumtambui. Pembejeo zote zinazotoka kwenye sekta ya tubaku zinakuja zinamlenga mkulima moja kwa moja kwa sababu tayari yuko kwenye usajili; ana namba yake, ana kitambulisho chake na anajua anacholima leo analima nini na anazalisha kiasi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukirudi kwenye zao la pamba ndio maana hata pembejeo zinazoenda kwenye zao la pamba matokeo yake tunakutananazo sokoni kwenye magulio kwa sababu, tunawapelekea watu tusiowafahamu. Tumeangalia kwenye bajeti sijaona kitengo ambacho kimeandaa kuwahudumia na kuwezesha bodi za mazao ziweze kuwa na nguvu. Tumeangalia bodi za mazao hazijatengewa fedha, tunaomba suala hili liangaliwe vizuri. Tuna Bodi ya Pamba; Bodi za Pamba, Tumbaku pamoja na Korosho zinafanya kazi nzuri sana, lakini hatuoni fedha gani zinapelekwa kushughulikia kuwezesha hizi bodi za mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mfano tosha sisi kwenye upande wa masoko ya tumbaku. Masoko ya tumbaku ili tuweze kupata madaraja *classifier* ni Mteuzi Mfawidhi wa Bodi ya Tumbaku. Na Mteuzi Mfawidhi wa Bodi ya Tumbaku wakati mwingine hana usafiri wa kwenda sokoni, usafiri anaotumia anabebwa na gari la mnunuzi ambaye wanaenda kushindana kwenye bei ya mkulima, nai atatendewa haki? Sidhani kama mkulima anaweza akapata haki wakati mwenye kutenda haki amepewa lifti na mnunuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba hili suala la fedha na bajeti kwa upande wa bodi zetu za mazao liweze kuimarishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa upande wa Jimbo la Ushetu. Nilitaka nimuombe Mheshimiwa Waziri, upande wa Ushetu tunazalisha sana mazao ya tumbaku, pamba, mahindi, tmpunga, karanga pamoja na dengu. Ningeomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha bajeti yake, kwa sababu Halmashauri ya Ushetu hatuna maghala na hivyo tunapoteza mazao mengi sana kwa sababu ya kukosa maghala na tumeshatenga eneo la zaidi ya ekari 600 kwa ajili ya kujenga maghala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa sababu tunazalisha mpunga na tunalisha nchi za mazaiwa makuu, Mkoa mzima wa Shinyanga pia unalishwa na Halmashauri ya Ushetu. Nchi za Kongo zinanunua mazao yao Ushetu, nchi ya Rwanda inanunua mazao yake Ushetu na wenzetu wa Burundi na Uganda wananunua mazao Ushetu. Tunaomba Mheshimiwa Waziri tuletewe maghala katika Halmashauri ya Ushetu, lakini pia tunahitaji eneo la umwagiliaji. Tumetenga zaidi ya ekari 3,500 kwa ajili ya umwagiliaji kwa kilimo cha mpunga. Tunaomba hili Mheshimiwa Waziri atakapokuja aje nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nijikite pia kwenye suala la utafiti. Tuna taasisi ya utafiti wa zao la tumbaku inayoitwa *TORITA*, sijaona fedha zinazopelekwa kwenye utafiti hasa kwenye upande wa *TORITA*, inatafiti sana suala la mbegu. Tuna changamoto kubwa sana ya mbegu za zao la tumbaku. Mbegu tunazozitumia kwenye zao la tumbaku wanao-*supply* ni wanunuzi wenyewe. Sasa tunaomba, kwa sababu tuna taasisi ya utafiti ambayo inasimamia zao la tumbaku, tunaomba fedha ziweze kuelekezwa kwenye taasisi ili mbegu za tumbaku zizalishwe hapa nchini, wakulima wengi wazalishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kuingiza kampuni nyingine ya ununuzi wa tumbaku na kuwasha kiwanda cha *TLTC*. Hili tumpongeze sana Mheshimiwa Waziri, wakulima wetu walikuwa na hali ngumu sana ya wapi wauze tumbaku. Na mwaka huu ameahidi kununua zaidi ya kilo milioni 10, na msimu unaukuja ataongeza kilo milioni 30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe tu, nchi za wenzetu, kwa mfano Malawi wanazalisha zaidi ya kilo milioni 230 kwa mwaka na bei yao ni kuanzia dola tatu mpaka dola nane. Zimbabwe wanazalisha zaidi ya milioni 200 mpaka milioni 300 na bei yao ni kuanzia dola tatu mpaka dola nane, iweje sisi Tanzania tumekuwa kisiwa? Wastani wetu wa bei ni dola 1.4, umezipanga sana ni dola 2.2. Niombe kwamba, Waziri kupitia Wizara yake ya Kilimo ateuwe wataalamu na Bodi ya Tumbaku waende kwenye nchi za wenzetu hizi ili kuona wanatumia mfumo gani kupanda kutoka dola tatu mpaka dola nane ilhali sisi tunahangaika na wastani wa dola moja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiendani na gharama za uzalishaji. Gharama za uzalishaji na bei ya pembejeo imepanda kwa kiasi kikubwa sana lakini bei ya tumbaku inazidi kuporomoka. Ningeomba sana hili Mheshimiwa Waziri aliangalie sana kwa sababu bodi zipo na viongozi wa ushirika wapo, waweze kutembelea kwenye nchi jirani waweze kuona wenzetu wanatumia mfumo gani kuweza kupata bei nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa ninamuita Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma aweze kuchangia.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia kwenye sekta hii ya Wizara ya Kilimo. Kwanza kabisa naunga Taarifa yote ya Kamati ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais, Mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa mambo yote anayoyafanya. Na tatu, nataka kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Hussein Bashe, pamoja na Naibu Waziri, Makatibu wote pamoja na wafanyakazi wote wa sekta ya Wizara ya Kilimo. Pia, bila kuwasahau kamati yangu nzima, wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo kwa kazi nzuri waliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwapongeza wakulima wote wa Tanzania kwa kazi wanayoifanya ya kutupatia chakula tunachokula kila siku. Kwa kusema hayo ninasema kuwa maendeleo ya uchumi tukubali kuwa yanatokana na sekta za uzalishaji ikiwemo sekta ya kilimo. Kwa pamoja tukishikamana na kilimo tukakipa kipaumbele namba moja naamini umasikini utapungua kama hautakwisha kwa watu wote hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa bajeti. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kukiona kilimo na kukipa kipaumbele kwa kuwaongezea Wizara fedha kutoka bilioni 274 mpaka bilioni 751. Mheshimiwa Rais tunakupongeza sana kwa kuliona hili na Mwenyezi Mungu azidi kukubariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya Kamati na madhumuni ya Serikali, hasa Wizara ni kukibadilisha kilimo kikawa kilimo cha mageuzi chenye tija na chenye biashara. Kilimo ni ajira, kinaleta chakula, ni lishe. Kilimo ni kila kitu. Huwezi kukaa bila ya kula ukadhani kuwa utaishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kusema mambo muhimu yanayopaswa kufanyika kwenye kilimo, nikianza na utafiti. Mheshimiwa Waziri naomba; hela zimetengwa za utafiti, Waziri mmepewa hela nyingi, hizo hela kuna vituo mbalimbali vya utafiti ambavyo tunaviita *TARI* pamoja na vyuo vingine vikuu kikiwepo Chuo Kikuu cha Sokoine na pia Chuo Kikuu cha Nelson Mandela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *TARI* ihakikishwe kuwa ni fedha kiasi gani inapelekwa kwenye kila kituo cha utafiti. Tafiti mbalimbali zimefanyika, na tafiti hizo ziwwafikie wakulima. Kuna tafiti rafiki ambazo ziko kwenye kituo cha Kibaha ambako wanafanya tafiti za *biological control* ambazo bado hazijawafikia wananchi. ninaomba hizo ziweze kuwafikia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninaweza kuongea ni kwenye huduma za ugani. Huduma za ugani nakuhakikishia haiajawahi kutokea. Maafisa Ugani walikuwa hapa, naamini wengine bado wako hap ana wengine wananisikia. Ninachokiomba maafisa ugani fanyeni kazi. Mmepewa vitendeakazi, mmepewa pikipiki, kila mmoja atapata pikipiki yake, pikipiki 7,000 zimetolewa, visikwambi vimetolewa, *extension kit* imetolewa, pia mmepewa na vi-*sample* vya kufanyia *sampling* na ubora wa udongo kila Halmashauri. Kwa hiyo, nawaomba ninyi maafisa ugani fanyeni kazi tuweze kuona matokeo ya kilimo, kilimo kiweze kubadilika na kilimo kiweze kuwa cha tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa huduma za ugani ni mambo mengi yametolewa haijawahi kutokea, hawajawahi kupata vifaa kama hivyo. Kwa hiyo, waweze kuwafikia wakulima, siyo kukaa nyumbani bila kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni umwagiliaji. Wewe mwenyewe ni shahidi, watu wote ni mashahidi. Mnaona kuwa kwa upande wa tabia-nchi hasa kwa sasahivi, kama ninavyosema, unaona kuwa hakuna mvua, lakini kusema ukweli watu wengi wamelima na haya mazao ya mafuta ya alizeti mnayoyasema pamoja na mawese yamelimwa, lakini ni ukame. Dawa yenyewe ni umwagiliaji, lakini kusema ukweli mpaka sasahivi sehemu tunayoimwagilia ni sehemu ndogo. Sehemu inayofaa kumwagiliwa ni kubwa ambayo sasahivi tunamwagilia asilimia 2.5 tu ndiyo inayomwagiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hamjui hela zimeongezwa za umwagiliaji, lakini ni asilimia 2.5 tu ndiyo inayomwagiliwa. Naamini kuwa mmejikita kweli, pesa zimetolewa, kwahiyo simamieni umwagiliaji. Ili tufanikishe kilimo chetu lazima umwagiliaji upewe kipaumbele kwa hiyo, angalieni umwagiliaji kusudi tuweze kumwagilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye mbegu. Kwenye mbegu, mbegu zinazalishwa na mbegu zinazalishwa na *ASA*…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ishengoma, mda wako naona kama umeisha.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kidogo. Niongezee dakika moja. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, haya nakuongeza dakika moja basi ili uweze kumalizia. *(Makofi)*

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa upande wa mbegu, uzalishaji wa mbegu ambao unafanya kusambazwa na *ASA*, na hasa sanasana tumeona wamesambaza mbegu za alizeti pamoja na mbegu za mahindi. Naomba wakulima tutumie hizi mvua chache ambazo zitakuwa zinanyesha, lakini sanasana kumkomboa mkulima ni kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba sana tena sana tuzingatie kilimo, kwa pamoja naamini tutatok. Hakuna kitu chochote kitatutoa kwenye umasikini bila ya kuangalia kilimo. Kwa hiyo, kilimo kipewe kipaumbele kusudi kiweze kututoa na sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siachi kuongelea Morogoro. Kwenye mabonde mengine ya Morogoro, mkoa ambao unazalisha chakula kwa wingi, yapewe kipaumbele. Ingawaje Serikali naiona kwenye umwagiliaji, lakini kwenye mabonde yote ambayo yako Mkoa wa Morogoro yaweze kuzalisha kwa wingi yaweze kuulisha Mkoa wetu wa Morogoro pamoja na mikoa mingine Tanzania kwa ujumla nan chi nyingine zinazofuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninaunga mkono hoja, ahsante sana nawashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Prof. Shukrani Elisha Manya, wakati huo Mheshimiwa Kirumbe Shabani Ng'enda, Mheshimiwa Deus Clement Sangu na Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea wajiandae.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi njiweze kuchangia katika Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema tu kwamba sisi ni sehemu ya Umoja wa Nchi za Afrika ambao katika makubaliano ya Azimio la Malabo tulikubali kwamba, asilimia 10 ya bajeti iweze kutengwa kwa ajili ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa kutenga bilioni 751.12 niongezeko la asilimia 255 ikilinganishwa na bajeti iliyopita. Ongezeko la asilimia 255 ni kweli kwamba ni la kupongezwa, linaonesha utashi na azma ya Mheshimiwa Rais ya kuboresha kilimo. Na tunatamani kwamba sisi kama *signatories* wa *Malabo Declaration* tufikishe asilimia 10, kwa sababu hii bilioni 751 ni asilimia 1.83 ya bajeti, ni kama tumeanza sasa kuipukuchua. Kwa hiyo tuombe sana kwamba, hebu matokeo yatakayotokana na ongezeko kubwa hili yasababishe Serikali kuona kwamba inafikia kiwango ambacho sisi tumekuwa tukikubaliana na wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sisi katika Kamati ya Kilimo tunaamini kwamba, kama kilimo kikipewa msukumo mkubwa kama ambavyo

tumekubaliana, tunaamini kwanza nchi itajitosheleza kwa chakula na kubakiza ziada kubwa kwa ajili ya kuuzwa nchi za nje. Yaani watu wataamini kwamba, kama kuna dhiki na dhahama mahali fulani basi Tanzania ni mahali pa kukimbilia. Lakini pia uchumi wa wananchi mmoja mmoja na uchumi wa Taifa utakua kwa kiasi kubwa sana na nchi itakuwa inatatua tatizo la ajira kwa vijana. Na inawezekana hata tatizo la machinga ambalo limekuwa ni gumzo katika nchi likaondoka kwa sababu ya kuweka msukumo mkubwa katika kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna jambo tumejifunza sana kutokana na *crisis* ya Ukraine na Urusi ni kwamba kama nchi tunapaswa kujitegemea kujitosheleza kwa mazao ya chakula yale ya msingi lakini na mafuta ya kula. Hilo nadhani lisiondoke katika vichwa vyetu, tumejifunza kwamba wakati wa *crisis* ni muhimu sana uwe unajitosheleza kwa mahitaji yale ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo napenda kutambua na kupongeza jitihada za Serikali na azma ya Mheshimiwa Rais kupitia Wizara ya Kilimo kwamba imeamua kwa dhati kuimarisha utafiti, lakini pia kupima afya ya udongo. Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na uongozi wote wa Wizara niwapongeze sana kwa msisitizo wa kusema kwamba watatoa ruzuku katika mbegu bora na kutoa ruzuku katika mbolea. Haya mambo yalipaswa kufanywa zamani, lakini kwa sababu tumekuwa na mwanzo basi tuendelee hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nina hoja fulani ninayotaka kuiweka hapa, kwamba historia inakupa namna ya kujifunza kwa ajili ya leo, lakini pia na kwa ajili ya kesho na kwa sababu hii ni historia ya nchi yetu ukiangalia katika kilimo kumekuwa na *cycle* fulani ambayo nataka kuiweka hapa kama hoja yangu ya msingi. Hoja hiyo ni kwamba, nchi inaanzisha zao fulani inaliita zao la kimkakati na Serikali inatia nguvu, watu wanalima kwa nguvu zote lakini baada ya muda unashaanga tu kwamba zao lililokuwa la mkakati zao hilo linakufa. Halafu Serikali inakuja kulifufua tena na mfano ni zao la mkonge na zao la ngano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwamba baada ya mageuzi haya ambayo tumeyaanzisha sasa, hii *cycle* ikome, ifikie mahali tunaposema kwamba tunazalisha parachichi, tunazalisha ngano, tunazalisha zao Fulani, basi sisi tuwe kinara ili wakati wa *crisis* watu wajue kwamba tukienda Tanzania tunapata haya mazao. Kwa hiyo hiyo *cycle* ya kuanzisha, kufa, kufufua, kuanzisha, haitufanyi tukawa na maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni *block farms.* Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwamba katika hili natambua kabisa kwamba ni jambo la msingi, lakini hebu tuone kwamba vijana tena vijana halisi wanaoonekana ndiyo, waingie hapa pamoja na umuhimu wa kuwepo wawekezaji wakubwa lakini vijana tunajua kwamba watakuwa hawana mitaji, lakini Serikali inapaswa iwape upendeleo ili vijana hawa ndiyo waingie

katika *block farms* kwa kufanya hivyo tutakuwa tumeondokana na tatizo la ajira za vijana ambao wanamaliza *level* mbalimbali za elimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kwa sababu ya muda ni kwamba kilimo ni ushindani na nchi jirani sisi tunapopanga hapa kwamba tuimarishe kilimo chetu na nchi jirani wanafanya hivyo hivyo na masoko yetu ni hayo hayo. Napendekeza hiki kitengo kisiwe ni Kitengo cha Utafiti lakini Wizara iwe na Kitengo cha *Intelijensia* kuangalia mwenendo wa masoko ili kwamba kama kunatokea tafrani mahali fulani basi kitengo hiki kinaweza kikatoa *information* ya namna ya kwenda. Kwa hiyo hiki tuweze kukifanya na tukifanya hivyo naamini kwamba nasi tutaendelea kuwa washindani katika soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hivyo, naomba kuunga hoja mkono ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Profesa Shukrani Elisha Manya kwa mchango wako mzuri.

Nilimwita Mheshimiwa Kilumbe Shaban Ng'enda ili aweze kuchangia.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nafasi hii ya kuchangia katika Wizara nyeti ya Kilimo na pia nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza kabisa naungana na wote waliotoa sifa nyingi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wizara nzima kwa kazi kubwa wanayoifanya. Bahati nzuri mimi Mheshimiwa Hussein Bashe namfahamu kabla hajawa Mbunge, kabla hajawa Waziri na namfahamu jinsi alivyo mahiri kwa jambo lolote ambalo anakusudia kulisimamia. Kwa hiyo naendelea kuwatia moyo ili kazi iweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya yote tunamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ameona umuhimu mkubwa wa kuongeza nguvu kwenye bajeti ya Wizara ya Kilimo. Ukurasa wa 71 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia kilimo cha umwagiliaji na ukiangalia bajeti nzima hii kuna mambo matatu ambayo naweza nikasema yamepewa nguvu kubwa sana kwenye bajeti hii. Kwanza, ni kilimo cha umwagiliaji; Pili, ni mkakati wa kupambana na tatizo la upungufu wa mafuta nchini kwa kuongeza nguvu katika kutoa mbegu, na Tatu ni kuongeza nguvu katika huduma za ugani yaani kwa kuwaongezea nguvu wataalam kwenye masuala ya utafiti na masuala ya kuwawezesha wataalam. Napongeza sana hatua hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye ukurasa huu amezungumzia mradi wa umwagiliaji wa Bonde la Mto Luiche lililoko katika Jimbo langu la

Kigoma Mjini. Huu mradi umeshafanyiwa upembuzi yakinifu kwa asilimia 100 na sasa unakwenda kwenye hatua ya utekelezaji. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, wananchi wangu wamekaa kwa muda mrefu tangu waliposikia mradi huu umepata ufadhili kutoka *Kuwait Fund,* wanasubiri kwa muda mrefu lakini wanaona kama unasuasua. Nimwombe kama alivyoahidi kuhakikisha kwamba mwakani hatua zote zinakamilika na mradi ule unapata mkandarasi. Mradi huu utakwenda kunufaisha wananchi wa maeneo ya Mgumile, Totwe, Nyaruboza, Kabogo, Kangona na Kafumbatwa. Hawa wananchi wote wa maeneo haya wanasubiri kwa hamu siku nyingi mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nataka nilizungumzie ni kilimo cha michikichi. Tuna upungufu wa tani kama 400,000 za mafuta ambazo tunataka tuzizalishe humu nchini. Eneo moja ambalo Serikali imelenga la kuzalisha ni kwenye kilimo cha michikichi na kilimo cha michikichi asili yake hasa ni Kigoma, hata hao *ma-giant* wa kuzalisha michikichi huko Malyasia tunaambiwa mbegu wameitoa Kigoma. Sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri, Waziri Mkuu ameweka juhudi kubwa sana kwa niaba ya Serikali, amekuwa akifuatilia sana, lakini kilimo hiki cha kuwapa wananchi miche ya kulima heka moja au heka mbili hakiwezi kututoa hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri, Serikali lazima iwekeze katika jambo hili ili kuokoa pesa za kigeni tunazozitoa kwa ajii ya mafuta. Imewekeza katika mbegu tunashukuru na watu wa *TARI* wamefanya kazi nzuri ya utafiti wa mbegu na watu wa *ASA* wamefanyakazi nzuri sana nawapongeza ya kuzalisha mbegu. Hata hivyo, nasema twende mbele zaidi, tufike mahali tuwakopeshe wananchi, Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza ilikuwa imeanza mpango mzuri kabisa, inasema inaandaa maeneo, inapanda miche kama ni heka tano au heka kumi, halafu inamkabidhi mwananchi kuendeleza lakini alipie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali iamue kwa makusudi kabisa kuingia katika kilimo kikubwa kitakachotutoa kwenye tatizo hili. wananchi wale wakikopeshwa, wakaandaliwa mashamba, wakakabidhiwa wayatunze, naamini kabisa tutatoka kwenye tatizo la mafuta tulilonalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla niseme, juhudi za Wizara wananchi wanazikubali, lakini tukiongeza kasi hapo tutalitoa Taifa letu katika matatizo ya mafuta, Kigoma peke yake inaweza ikakidhi mahitaji ya mafuta haya iwapo michikichi itapandwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda.

Sasa namwita Mheshimiwa Deus Clement Sangu aweze kuchangia.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa fursa hii ili niweze kuchangia kwenye Sekta muhimu sana ya Kilimo. Kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri Bashe na Naibu wake kwa kazi nzuri wanazofanya pale Wizarani. Katika Wizara hii nitakuwa na mambo muhimu matatu: Kwanza nitaongelea kampuni yetu ya mbolea ya Taifa kwa maana ya *Tanzania Fertilizer Company;* muda ukiniruhusu nitaongelea Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko; na mwisho kabisa nitamkumbushia Mheshimiwa Bashe ahadi zake alizotupa wakati alipofanya ziara Mkoani Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Kampuni yetu ya Mbolea, Mheshimiwa Bashe anajua wazi na kwenye bajeti yake leo hii amesema kwamba wanaenda kuiongezea uwezo Kampuni yetu ya Mbolea ya Taifa kwa maana *Tanzania Fertilizer Company* bilioni 6.0. Hata hivyo, nimkumbushe, kampuni yetu hii bilioni 6.0 aliyotaja hapa leo, ni *token* tu, tuna tatizo kubwa na ndiyo *instrument* kubwa ya nchi hii ambayo itatusaidia katika ku-*stabilize* bei za mbolea nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mwaka 2008 tulipoiacha hii kampuni ikafa kwa sababu ya mbolea ya ruzuku isiyolipika, tukaitwisha mzigo wa madeni mengi, hii kampuni ya mbolea ikafa, tumewaacha *private operator* wana-*operate* soko la mbolea, tatizo lake ni nini? Wanaweza wakafanya *curtail***,** wakafanya *inflation* na ndiyo maana unaona bei ya mbolea nchini imekuwa haitabiriki. Kama kampuni yetu ingeweza kuwa na fedha, kama kampuni yetu ingekuwa ina uwezo, tungeweza angalau kama Serikali tukasimama, wakati wa migogoro na shida ya mbolea kama leo, kampuni hii wangeweza wakafanya kazi hiyo pasipo tatizo lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ninavyoongea Waziri ametaja bajeti yake bilioni 6.0, wakati huo hii kampuni inawadai watu, Serikali bilioni 3.0, vyama vya ushirika bilioni 2.0, watu *private* zaidi ya bilioni 10 na na kitu. Kwa hiyo jumla ya bilioni 19 ziko kwa watu. Mheshimiwa Waziri anahangaika tumpitishie bilioni 6.0 hizi, lakini kuna bilioni 19 watu wapo, hawajafa, wapo na wanaendelea kuwepo. Mheshimiwa Waziri atumie Serikali ina mkono mrefu, watu warudishe bilioni 19 tufufue kampuni yetu ya mbolea kwa sababu bila hivyo tatizo la mbolea litatusumbua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wamesema kwamba hatuna hata *stock* ya mbolea, lazima tuwe na *buffer stock* ya mbolea kwa sababu bila hivyo ukitegemea *private operator* wao wanafanya kwa kufuata *theory* ya *just in time*. Akileta mbolea anauza, hawezi kuweka *stock* ya miaka miwili au mitatu kwa sababu yeye siyo shughuli yake, yeye anataka apate faida kwa wakati huo, akishapata faida anaachana na mambo hayo. Hivyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri aende kufanya shughuli hii ya kuwafuatilia wale waliochukua bilioni 19 kwenye kampuni yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimshukuru pia Mheshimiwa Rais kwa mara ya kwanza ameonyesha nia njema na kampuni hii. Amelipa madeni bilioni 9.0 kwenye Benki ya Exim, lakini bado tunadaiwa bilioni 15 kwenye mabenki mengine. Mheshimiwa Waziri aende kupambana kwa namna yoyote, tutakapoenda kupeleka ruzuku ya bilioni 250 alizotaja hapa, kampuni yetu iwe imefufuka nayo ishiriki ili isaidie ku-*regulate* suala la mbolea. Wananchi wangu kwa mfano Mkoa wa Rukwa tumehangaika, tumeshindwa hata kulima mahindi kwa sababu mbolea ilikuwa juu. *DAP* tulikuwa tunanunua mpaka mfuko mmoja Sh.150,000; UREA imeenda Sh.85,000, bei ni kubwa, wananchi waliamua waachane na mahindi. Hivyo, Nimwombe sana Mheshimiwa Bashe, nataka nijue atakapokuwa anahitimisha atupe *strategy,* aachane na hiyo bilioni 6.0, ni namna gani anafufua Kampuni yetu ya Mbolea ya Tanzania. Hilo ni jambo la kwanza nilisema nitalisemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni Bodi yetu ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko. Inatusaidia sana kutafuta masoko, tumepata masoko ya mazao kule Sudan ya Kusini, Rwanda, Zimbabwe, Comoro na DRC. Sasa suala la DRC kwa kwetu Mkoa wa Rukwa ndiyo soko letu la Jirani, lakini linakumbwa na vikwazo vingi sana kwa sababu lazima tupite Zambia na pale Zambia nao ni *competitor* wetu kwenye zao la mahindi wanatuwekea *trade embargoes* ambazo zinafanya biashara ile iwe ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshauri Mheshimiwa Bashe kupitia Wizara ya Mambo ya Nje, yeye mwenyewe na Ubalozi wetu wa Zambia, waende wakaongee na Serikali ya Zambia watupunguzie hivi vikwazo kwenye mazao, yaani mfanyabiashara akitoka na mazao kwa mfano Songwe, Rukwa akifika tu Zambia wanaweza wakamweka hata wiki mbili au wiki tatu. Mambo mengine kama samaki na mazao mengine hawana shida, ila zao moja tu la mahindi ndiyo kikwazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe na Waziri analijua vizuri jambo hili, kupitia ubalozi wetu, Wizara ya Mambo ya Nje, tukafanye kupitia diplomasia yetu na nchi jirani ya Zambia wasitunyanyase kwenye zao la mahindi, kwa sababu wamekuwa wakitoa visingizio kwamba mahindi yetu yana sumu, wafanyabiashara wanapata hasara wakiwa hapo hapo na mwishowe wanakata tamaa, kwa hiyo mazao yetu hayapati fursa ya kwenda huko DRC pale Lubumbashi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili kwenye hii Bodi ya Mazao Mchanganyiko, nimefanya utafiti na mpaka tukafanya mazungumzo na Jimbo jirani la *Out Katanga,* wametushauri jambo moja hii habari ya kupita nchi za jirani ndiyo maana tunapata mateso, tukae na Wizara ya Fedha, tutafute mwekezaji, tutengeneze zile kilometa 720 ambazo zitatupeleka Lubumbashi, ambayo itatupa fursa sasa ya kufunguka kwa Bandari ya Kasanga, Bandari ya Kalema na Bandari ya Kabwe, tutaenda kwa urahisi kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukipata mwekezaji atawekewa *fee* ya barabara ambayo *return* yake haifiki hata miaka mitano, yule mwekezaji pesa itarudi na barabara ile itafungua Mkoa wa Rukwa, Katavi na Kigoma. Nimwombe sana Mheshimiwa Bashe, haya manyanyaso ninayomwambia ya kupitia nchi za jirani sasa tukafungue. Tumewekeza bandari nilisema hata kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, bandari zile zinabaki kuwa *idle*. Twende tukamalize tu kilomita 720 tuunganishe pale Bandari ya Moba, upande wa pili wa Zambia, tukafike Lubumbashi ili ghala lile linalotunza zaidi ya tani 2000 kule Lubumbashi liwe na *impact* na Bodi ya Mazao Mchanganyiko waone tija kwamba kweli tumeenda kusaidia kutafuta masoko kwa ajili ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo nataka niongelee pia ni kwamba, hii bodi tumeipa majukumu mazito ya kuchukua viwanda vilivyokuwa chini ya *NMC*. Ili viwanda hivi viweze kuongeza thamani ya mazao ya wakulima wetu na nimwombe Waziri, mikoa mingine imeweka vinu vya kusindika mpunga, mahindi, lakini Mkoa wa Rukwa sijaona. Nimwombe sana Mheshimiwa Bashe na amekuja pale, tupate na sisi kiwanda walau cha kusindika mpunga, tupate viwanda vya kusindika mahindi ili tuongeze thamani ya mazao yetu ambayo yatafanya wananchi wetu wapate urahisi wa kupata masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna shida moja na naomba hii Waziri wa Fedha popote alipo anisikie. Bodi ya Mazao Mchanganyiko wameandika *proposal* kuomba kuendeleza hivi viwanda na ile *proposal* inataka tu *approval* kutoka Wizara ya Fedha. *Approval* ile imekuwa na vikwazo na ile siyo *government guarantee* ni *just a government concept,* wana-*approve* tu, wanatupa fedha na ile fedha haina *impact* yoyote kwenye deni la Taifa, yenyewe inaenda kufanya jambo moja kwamba mnakuwa na *partnership* na Benki, *CPB* na Benki wana-*operate* kiwanda, Benki ikipata *revenue* yake wanawaachia kiwanda kinakuwa cha kwenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwomba sana Mheshimiwa Bashe, watakapokuwa hata kwenye Baraza la Mawaziri amweleweshe vizuri najua ndugu yangu Mheshimiwa Mwigulu Nchemba ni *Economist* anajua, hili jambo halina *impact* yoyote kwenye deni la Taifa, ni jambo tu la ku-*approve,* wachukue hizo fedha, wajenge viwanda vya kuongeza thamani za mazao kwa mwananchi ili tuweze ku-*compete*. Mwezi Machi Mheshimiwa Waziri alikuwa yuko kwenye maonyesho ya Dubai *expo,* sasa masoko yatakuja mengi, baadaye hatutaweza ku-*compete* kwa sababu hatuna *value addition* ya mazao yetu. Nimwombe sana Waziri, hili jambo ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu na la mwisho sasa, nimkumbushie ahadi alizokuwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha, malizia kwa dakika chache malizia.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi zote za Mheshimiwa Bashe nitampelekea kwa maandishi na nitataka kujua *status* ya hizi ahadi alizoahidi zitaishaje, maana ana ahadi kama 10, naona ametekeleza mbili tu, ahadi nane bado namdai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Deus Clement Sangu.

Nilimwita Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea, wakati huo Profesa Patrick Aloyce Ndakidemi, Mheshimiwa Denis Lazaro Londo na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika wanajiandaa.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii, lakini kabla nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na nguvu. Pia niungane na wenzangu kumshukuru Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuleta maendeleo nchini kwetu. Kwa kipekee pia niwashukuru Mawaziri wetu, ndugu yangu Bashe pamoja na kaka Anthony kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya kuendeleza Sekta hii ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda nina mambo mawili tu ambayo nataka kuchangia leo. La kwanza, ni skimu za umwagiliaji; kwenye Jimbo langu la Korogwe Mjini nina skimu tatu za umwagiliaji. Skimu hizo ni Mahenge, Gou pamoja na Kwamgumi. Kimsingi Jimbo langu ni kati ya majimbo ya mjini wengi tunajishughulisha na biashara, kilimo siyo sana kwa hiyo skimu hizi ni skimu ambazo tunazitegemea kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, skimu hizi zimekuwa na matatizo kwa muda mrefu, watu hasa wa Mahenge na Goho ambao wapo kwenye Kata ya Kwamndolo wamekuwa wakilima mara nyingi mpunga lakini wanapata mafuriko, kwenye miaka mitano tumepata mafuriko zaidi ya mara tatu, nguvu zote walizozitumia kuandaa mashamba hadi wanakaribia kuvuna mafuriko yanakuja mpunga ule unakwenda na maji wote, kwa hiyo ni hasara kubwa wanaipata, kwa juhudi kubwa ambazo wanaziweka kuleta chakula ambacho kinalisha Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana niliiomba Wizara hii na ilinikubalia kwamba itaenda kutujengea skimu zetu, wakasema wataanza na skimu ya Mahenge. Tarehe 5 Julai, 2021 ilitoka *list* ya skimu ambazo zitaenda kufanyiwa kazi mwaka huu tulionao wa fedha na Mahenge ikiwa skimu Namba Nne kwenye hiyo *list*, lakini jambo la kushangaza juzi wametoa *list* ya

skimu ambazo zinaenda kufanyiwa kazi na skimu yangu ya Mahenge haipo. Hili jambo limesikitisha sana wananchi wangu pia limenisikitisha mimi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu gani kimetokea tuliambiwa tunaenda kujengewa skimu ile, nilienda nyumbani Jimboni kwangu nikawatangazia wananchi kwamba hasara sasa ni basi, Serikali imepanga kujenga skimu hizo na tunasubiri fedha kwa mshangao mkubwa *list* inatoka ya skimu za…

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

**T A A R I F A**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba nimpe mzungumzaji taarifa kwamba siyo skimu ya Mahenge tu hata skimu ya Kwamkumbo na ipo barua ya *commitment* ya Wizara na Tume ya Umwagiliaji kuwa skimu za Mahenge na Kwamkumbo lakini kwenye tangazo la zabuni hazipo, naomba nimpe taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kimea unaipokea taarifa.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mikono yangu yote miwili napokea taarifa ya Mheshimiwa Timotheo Mnzava, Mbunge jirani wa Korogwe vijijini. Kimsingi ninajua jitihada kubwa za Kaka yangu Mheshimiwa Bashe, nafamu ni rafiki yangu sana na yeye anafahamu lakini najua jitihada za Ndugu yangu Mheshimiwa Antony najua wanafanya kazi kubwa, lakini kwa hili kesho ninatarajia kushika SShilingi hadi watuhakikishie na watupe majibu kamili kitu gani kinaenda kufanyika. Maana siwezi tena kwenda kurudi Jimboni kwangu mwaka jana niliwaambia inatekelezwa sasa ninawaambia nini, kwamba Serikali haina fedha wakati mwaka jana kulikuwa na *list* ya skimu 10, mwaka huu zimeletwa *list* ya skimu 13 za kutengenezwa ya kwangu haipo narudi nawaambia kitu gani wananchi wa Korogwe? Kwa hiyo ninatoa taarifa kwamba kesho nitashika Shilingi mpaka nitakapohakikishiwa siyo ahadi kuhakikishiwa kwamba skimu ya Mahenge itawekwa kwenye *list* na wananchi wangu wa Mahenge wataenda kujengewa skimu mwaka huu, ninashukuru kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili na la mwisho ambayo ninapenda kuchangia, kilimo kwenye nchi hii, vijana wanatakiwa kuji-*engage* sana kwenye kilimo lakini changamoto kubwa inayowakumba vijana pia wananchi wetu wa vijijini ni ukosefu wa fedha mitaji, benki zetu zimekuwa haziwezi kukopesha vijana kwa ajili ya kutokuwa na vigezo hasa dhamana. Ninashauri Wizara yetu ianzishe mfuko ambao utakuwa na kazi kubwa mbili. Kazi ya kwanza kusimama kama dhamana hasa kwa vijana wetu wanaomaliza shule, wanaotaka kujiingiza kwenye kilimo hawawezi

kukopesheka kwa hiyo mfuko huo usimame kama dhamana ili waweze kukopeshwa. Pia Wizara imefanya kazi Serikali imefanya kazi kuomba benki nyingi kupunguza riba lakini baadhi ya Benki bado riba ipo juu, kwa hiyo huu mfuko pia utumike kama sehemu ya kupunguza riba, kama benki inakopesha asilimia 10 tunataka vijana wetu wakopeshwe kwa asilimia saba ili asilimia mbili mfuko huu ufanye kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona nchi nyingi zimefanya hivyo nikikutolea mfano nchi ya Ghana ina mfuko huo ambao moja unasimama kama dhamana kwa ajili ya wakopeshwaji lakini namba mbili ku-*reduce interest rate* endapo benki itakuwa *willing* kukopesha wakulima lakini *interest rate* zipo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni hayo mawili, lakini kikubwa sana ni skimu yangu ya Mahenge, kesho nitashika Shilingi endapo hili halitajibiwa, siyo kujibiwa tu Waziri aje na *commitment* kwamba skimu ya Mahenge itaenda kufanyiwa kazi mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na Mungu awabariki, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea kwa msisitizo wako wa skimu ya Mahenge. Nilimuita Mheshimiwa Prof. Patrick Alois Ndakidemi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami nianze moja kwa moja kwa kumpongeza sana Waziri wetu wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Bashe na Naibu Waziri Mheshimiwa Antony Mavunde pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Kilimo kwa kazi nzuri wanayoifanya. Watendaji hawa ni watu wenye busara kubwa sana wamekwenda kwenye meza ya majadiliano, wamekaa na Wizara ya fedha na wadau wengine wa maendeleo, wakashawishi mpaka bajeti ya kilimo ikaongezeka kutoka Shilingi 294,000,000,000 hadi Shilingi 751,000,000,000 sawa na ongezeko la takribani asilimia 155 na hii ni 1.8 *percent* ya bajeti yote ya Taifa, hongereni sana Waziri na wenzako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Wabunge wote, Wabunge wote huku ndani tulipiga kelele kwamba bajeti iongezeke na kwa namna ya pekee pia nimpongeze na kumshukuru Mheshimiwa Mwigulu Nchemba kwa kusikiliza kilio cha Wabunge wote na kwa sababu tumeona kabisa alikuwa na nia nzuri na bajeti imeongezeka, tunashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naendelea kuishauri Serikali kwamba tukienda na Azimio la Malabo tulitakiwa tuwe na angalau asilimia 10 ya Bajeti ya Taifa iende kwenye kilimo lakini hii 1.8 ni bado tungefurahi sana 4.1 *trillion* ambayo ndiyo asilimia 10 kufuatana na Azimio la Malabo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaendelea kusema kwamba bado ni muhimu Serikali iongeze hii bajeti kwasababu Kilimo kinaajiri asilimia 65 ya Watanzania wote, kilimo kinachangia asilimia 27 kwenye Pato la Taifa, kilimo kinachangia asilimia 25 ya fedha za kigeni, kilimo kinatulisha watu wote nchi hii. Kwa hiyo naomba sana Serikali ifikirie kuongeza hii bajeti kama walivyokubaliana Marais kwenye lile Azimio la Malabo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utakuwa kwenye maeneo matatu ambayo ni suala la mbolea, maparachichi na nitaongelea changamoto za Jimboni kwangu ikishindikana nitaishia nitakapoishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu kitunguu na nyanya ilivyo ni muhimu sana katika kukaanga chakula na kuandaa chakula kizuri, mbolea ni *component* muhimu sana kwenye kuongeza tija uzalishaji kwenye Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika msimu uliopita wote tumeona kwamba bei za mbolea zilikuwa kubwa kidogo, Wabunge wengi wamesema zilipanda kutoka Shilingi 50,000 kwa mfuko wa kilo 50 hadi kufikia Shilingi 150,000 kwenye baadhi ya maeneo, hili lilikuwa ongezeka kubwa kusema kweli karibia asilimia 200 ya nyongeza ya bei ya mbolea. Wakulima wengi walishindwa kununua mbolea na msimu huu hali ya kilimo sidhani kama itakuwa kama tulivyozoea kwasababu ya wakulima wengi watakuwa wamekwazika kwenye bei ya mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu zipo sababu ni nyingi ambazo zimesababisha mbolea ikapanda bei, tunaona kule China waliweka lock down na Urusi wana vikwazo vya uchumi kwasababu ya vita wanavyopigana na Ukraine kwa hiyo vitu vingine ni nje ya uwezo wetu na hii imesababishia bei ya mbolea katika soko la dunia ikapanda na hata hapa Tanzania sisi hatujawa *insolated* tuna-*face the same problem*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo pamoja na kwamba tuna matatizo lakini kama nchi ninashauri Serikali lazima ifanye vitu fulani ili tuondokane na hii changamoto. Ushauri wangu wa kwanza kwa Serikali Waziri katika hotuba yake amesema wana-*plan* kuwasiliana na Wizara ya Nishati ili kile kiwanda cha kutengeneza *urea* kiwepo, hili ni jambo muhimu sana. Kama *intercom* wame-*invest* Dola Bilioni 180 wakaweka kiwanda, jamani mbolea ni suala la usalama wa Taifa letu. Kama hakuna chakula hakuna usalama hapa, mimi ninaishauri Serikali kabisa kwa nia nzuri wakae chini waangalie namna ya ku-*invest,* gesi yetu ya asili tunayo tutumie ile gesi tutengeneze mbolea yetu wenyewe ili tujihakikishie usalama wa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi kama China huwa zina-*plan* wanaweza wakawekeza hapa au tukanunua kutoka China tukatengeneza mbolea yetu wenyewe, kwa hiyo ushauri wangu wa kwanza kwa Serikali ni kuwekeza kwenye kutengeneza mbolea yetu wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa pili, ninaishauri Serikali ihamasishe Vyama vya Ushirika wanunue mbolea kwa pamoja, *(bulk procurement)* kwa kufanya hivyo tutapunguza gharama za kuingiza mbolea nchini na bei inaweza ikashuka ikawa afadhali kidogo, tunaona kule kwenye Tumbaku wanafanya hivyo na mambo yanakwenda vizuri. Ushauri wangu wa tatu ni kuishauri Serikali ikiwezekana watoe bei elekezi ya mbolea ili kila mtu asiwe anajipangia tu bei ya mbolea lakini tuwe na bei elekezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa Nne ni kuishauri Serikali ikiwezekana kupitia utafiti tuwahamasishe wakulima wetu watumie mbolea za asili ili wale ambao hawataweza kununua mbolea watumie mbolea za samadi, mboji na kadhalika. Na ushauri wa mwisho kwenye hili suala la mbolea ni…

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cherehani taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninampa taarifa mzungumzaji kwamba kwenye upande wa tumbaku tunao umoja wa wakulima wa Tumbaku unaitwa *TSJE* ndio maana tunanunua mbolea kwa mfumo wa Pamoja, basi tungeomba na mazao mengine waweze kuunganisha umoja wao ili waweze kuagiza mbolea kwa pamoja na bei inapungua, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Unaipokea taarifa hiyo Mheshimiwa Profesa.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea kwa moyo mmoja. Ushauri wangu wa mwisho ni kuishauri Serikali ikiwezekana wakae wapunguze tozo ambazo siyo muhimu kwa wakati huu. Kwa mfano, tozo za ushuru za usafirishaji na uingizaji wa mbolea zikipunguzwa zinaweza zikatoa nafuu kwa wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili ni kwenye zao la Maparachichi. Kama tulivyosikia watu wengi wanazungumzia maparachichi yanalimwa kwenye maeneo mengi hapa nchini, hii ni *hanging fruits* tukiitumia hii fursa vizuri ile *target* ya Mheshimiwa Waziri ya kuhakikisha kwamba mboga mboga na matunda yanachangia Dola Bilioni Mbili kwenye Pato la Taifa tutaifikia vizuri. Kwa hiyo ninaendelea kuishauri Serikali isimamie na isukume wahakikishe kwamba angalau tunaunda vikundi vya kupanda parachichi pamoja, wauze pamoja, tuvune pamoja ili tuweze kulijaza soko na kwa kufanya hivyo nawaomba wananchi wangu kwenye Jimbo la Moshi vijijini maeneo ya Uru, *Old* Moshi, Kibosho, mpaka Mabogini kule, tuingie kwenye hii biashara kwasababu Waziri ameshasema hapa kwamba kuna miche 20,000 atakayotoa ili na sisi tunufaike na hili jambo lenye heri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni changamoto kwenye Jimbo langu. Mheshimiwa Waziri tuna changamoto ya miche ya kahawa, wachaga kule sasa hivi tumechacharika tunataka kupanda kahawa tuchangie kwenye Pato la Taifa, kwa hiyo nikuombe ile miche ambayo unatoa usitusahau. Kuna maeneo yangu ya Uru, Kibosho na *Old* Moshi tupo tayari kulima kahawa na ndizi, ile miche utakayoleta tunaomba utusaidie ili na sisi tuchangie kwenye Pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili ni miundombinu ya …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi nilikuongeza muda wako umalizie changamoto za Jimboni, naona umeshaielezea vizuri au kuna kitu unadhani umekisahau.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia.

**MWENYEKITI:** Sawa.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mifereji ya asili na miundombinu ya umwagiliaji tuna eneo kama hekta 4,060 kwenye eneo la Mabogini, Arusha Chini, na Mandagamnono kwa hiyo tukiboreshewa mifereji ya asili na miundombinu ya umwagiliaji tutachangia vya kutosha katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Profesa Ndakidemi kwa mchango wako, ulipokuwa unaongelea masuala ya parachichi na wananchi wa Mufindi nao walikuwa wanafurahia uendelee kuongea tu, maana wanajua unawasemea na wao kwa sababu na wao wanazalisha kwa wingi sana parachichi. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, nilimuita Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo wakati huo Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga na Mheshimiwa Ighondo Ramadhani Abeid wanajiandaa. *(Makofi)*

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika bajeti ya Kilimo, pia nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kututunuku uhai na nishukuru Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuunga mkono jitihada za Bunge la 12 ambalo limejipa agenda ya kufanya mapinduzi ya kweli ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ya Shilingi Bilioni 751 ambayo ni ongezeko la zaidi ya asilimia 200 ni kiashiria kwamba Rais wetu ana imani kubwa na Bunge hili na yupo pamoja nasi na kwasababu tumejipa agenda

ya kufanya mapinduzi ya kilimo basi huu ni uungwaji mkono wa aina yake, nami naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Rais wetu kwa imani hii ambayo anatuonesha na ushirikiano ambao anatupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wangu walikuwa wanauliza kwamba ndiyo watumishi wameongezewa mshahara kwa asilimia 23.3 sisi wakulima tumepata nini? Jibu wamepata leo kwenye bajeti hii ya Wizara ya Kilimo, kwamba Serikali yetu inapeleka Bilioni 751 kwa ajili yao na fedha hizi zinaenda kuleta mabadiliko ya kweli katika uchumi wao. Ninampongeza Rais wetu na nimpongeze pia kwa suala la kuongeza mshahara kwa watumishi hasa hawa wa kilimo ambao ninaamini ongezeko la mshahara huu unaenda kuwapa *incentive* ya kwenda kuji-*engage* kikamilifu katika kufanya mapinduzi ya kilimo hasa katika maeneo ya pembezoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze na utafiti, kwenye bajeti ya kilimo Waziri wetu Profesa Mkenda alizungumza kwamba ametenga Bilioni Mbili kwa watafiti wetu ambao wanakwenda ku-*publish* kwenye *journals* za kueleweka. Kwenye tafiti za kilimo bado tupo nyuma sana na ndiyo maana mwaka jana tulitenga Bilioni Tano na mwaka huu tumetenga Bilioni Tano kwa ajili ya kuaziga viuatilifu nje. Fedha hizi kama tungekuwa tumewekeza walau Bilioni Moja au Mbili kwa ajili ya utafiti wa viuatilifu naamini kabisa tusingefikia mahali ambapo tunatenga zaidi ya Bilioni Tano kwa ajili ya kuagiza nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo tunahitaji kupata mbegu bora, jana tulizungumzia kwa hisia kuhusiana na afya ya akili lakini unapozungumzia kilimo afya ya udongo ndiyo kila kitu, lakini kuna tafiti ngapi ambazo zimejikita kuangalia afya ya udogo katika maeneo mbalimbali? Hiyo ni changamoto ambayo naomba Wizara ya Kilimo ichukue kwa uzito wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katikati ya miaka ya 70 kuna nchi ndogo kule Amerika ya Kusini ilitusaidi yenyewe ikiwa katikati ya vikwazo na hali ngumu ya kiuchumi, ilitujengea shule Nne kule Kibiti, Ruvu, Ifakara na Kilosa. Shule hizi zilikuwa za kilimo na zilijengwa kama msaada wakati Serikali hiyo ikiwa katika hali ngumu sana ya kiuchumi. Shule hizi sijaona kama kuna mpango unaoeleweka katika miaka ya karibuni kurudisha hadhi yake ya kuzalisha Wataalam wa Kilimo katika elimu ya sekondari. Ninaomba Mheshimiwa Waziri wakati unafanya majumuisho ujikite katika kutuambia nini mpango wa Wizara yako kushirikiana na Wizara ya Kilimo na TAMISEMI katika kurudisha hadhi ya shule hizi za sekondari ambazo zilijikita kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo tuna kitu kinaitwa *skills development levy* ambayo ni asilimia Nne inatoka katika *private secto,r* fedha hizi lengo lake ni kujenga uwezo kwa vijana wetu, lakini sioni matumizi yake fedha hizi katika ujenzi wa *skills* katika vyuo vya kati. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo muangalie namna bora ya kushirikiana na Wizara ya Elimu kuangalia vyuo vyetu vya *VETA* kuzalisha wataalam wa kati

kwenye kada ya kilimo, pamoja na kuimarisha vyuo vyetu vya kilimo kwenye tafiti na vitu vingine. Kubwa kuliko yote ni taasisi zetu za *TARI* na *ASA* hali yake ni ngumu na kwasababu tunaagiza mbegu kwa kiasi kikubwa tunao wajibu wa moja kwa moja kuziwezesha taasisi katika hizi ku-*develop* ama kufanya tafiti za mbegu ili tupunguze utegemezi wa mbegu kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna jambo ambalo tumejifunza kwenye vita hii ya Ukraine ni kwamba kujitegemea ni muhimu hasa katika sekta ya kilimo pia kama kuna jambo ambalo tumejifunza hawa watu ndiyo wazalishaji wakubwa wa mafuta na ngano. Sasa Serikali tumejipanga vipi kutumia fursa hii, kwasababu kule kuna wawekezaji ambao uzalishaji wao umekuwa *destructed* na hii vita. Tuwakaribishe kama wawekezaji huku, wanayo *knowledge,* wanazo *skills* na wanayo mitaji. Tumejipanga vipi kuhakikisha kwamba kwa sababu soko la Ulaya katika maeneo hayo limevurugika, tuwavutie huku waje ku-*boost* sekta ya kilimo katika maeneo yetu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo wakati nikiwa mdogo pale Halmashauri ya Mji wa Morogoro magari yote yalikuwa yanaandikwa Ofisi ya Mkurugenzi *except* gari moja tu ambalo lilikuwa linabeba takataka lile halikuandikwa kabisa, halina maandishi yoyote ambayo yanaeleza gari linamilikiwa na nani. Waswahili wanasema ukitaka kumuua mbwa mpe jina baya ukimwita *queen* au *prince* huwezi kumuua, ukimuita *snake* ama *cobra* utamuua tu bila shaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika sekta ya mbogamboga ambayo ni maarufu wanaita mali kuoza, sekta hii ni muhimu sana kwasababu imeajiri vijana wengi, akina mama wengi lakini haipewi msukumo. Ndio maana unasikia bodi ya Mkonge, Bodi ya Kahawa lakini huwezi kusikia Bodi ya Mbogamboga, Bodi ya Matunda, huwezi kusikia kwa sababu imeshaitwa mali kuoza, lakini hilo ndilo eneo ambalo linaajiri vijana wetu wengi, katika mazao ambayo tunasafirisha sana nje ni mbogamboga na matunda, lakini huwezi kuona msukumo wa dhahiri ambao umejikita katika kuonesha kwamba tunaenda kuchukulia sekta hii katika uzito wake.

Hilo ndiyo eneo ambalo linaajiri vijana wetu wengi na katika mazao ambayo tunasafirisha sana nje ni mbogamboga na matunda, lakini huwezi kuona msukumo wa dhahiri ambao umejikita katika kuonyesha kwamba tunaenda kuzichukulia sekta hii katika uzito wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana *TAHA* kwa sababu imelibeba sana zao la matunda na mbogamboga lakini pamoja na yote hayo, tunahitaji Serikali kuwezesha sekta hizi hasa kwa kuondoa kodi kwenye *cold storage* na *facilities* ili mkulima mdogo aweze kuhifadhi matunda yake ambayo yanaitwa mali kuoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, bajeti yetu inapaswa kujikita sana katika umwagiliaji. Tuna hekta zaidi ya milioni 29 ambazo zinafaa kwa kilimo cha umwagiliaji, lakini mpaka sasa eneo ambalo tunamwagilia ni ekari 727,280 sawa na asilimia 2.5. Huu ni utani, huu ni mzaha. Katika nchi ambayo tumejizatiti katika kuleta mapinduzi ya kilimo, hatuwezi tukawa na hekta zaidi ya milioni 29 ambazo zinafaa kwa umwagaliaji, tunaenda kukomea kwenye hekta 700,000 ambayo ni asilimia 2.5. Lazima tuonyeshe *seriousness* kwenye hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo anapofanya majumuisho atuambie nini mpango mkakati wa Serikali yetu katika kuhakikisha kwamba tunaenda kuboresha kilimo chetu hasa katika eneo la umwagiliaji? Katika hili napendekeza kuangalia nafuu ya kodi kwenye pampu ndogo ndogo kuwawezesha wakulima wetu katika maeneo ya vijijini kwa ajili ya kulima, lakini pia kutoa nafuu ya kodi kwenye mitambo ya kuchimba visima pamoja na uchimbaji wa mabwawa. Ukiweka kodi pale unaweza ukapunguza thamani kwa kutoa asilimia 30 mpaka 40, na hii inaweza ikaboresha suala zima la utengenezaji wa miundombinu hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, uvunaji wa maji ya mvua. Tunatumia fedha nyingi kuboresha barabara zetu na miundombinu yetu, vile vile fedha ambazo tunatumia kukarabati miundombinu ambayo imeondolewa na mafuriko zinaweza zikawa nyingi ukilinganisha na fedha ambazo tungewekeza kujenga mabwawa ya kuvunia maji kwa ajili ya kulinda miundombinu hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoka Dar es Salaam mpaka hapa, utakuta mashimo mengi sana kwenye *SGR*. Yale mashimo yanafaa kutengeneza mabwawa ambayo yanaweza yakatunza maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo, naomba kutoa rai kwa Wizara ya Kilimo kuyaangalia mabwawa haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, nilimwita Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, aweze kuchangia.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu ya kilimo. Nianze kumpongeza sana mdogo wangu Mheshimiwa Bashe na Naibu Waziri na Watendaji wote katika Wizara hii. Kwa kweli wameonyesha njia, tunaona mambo yanakwenda vizuri, wamefanya ushawishi mkubwa, wamekuwa wasikivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile namshukuru Mheshimiwa Rais toka mwanzo kabisa kwa kuonesha nia ya dhati kabisa na kutekeleza nia hiyo ya

dhati kwa vitendo. Tulilalamika sana hapa Bunge lililopita kuhusiana na mbolea tukamwona Mheshimiwa Rais kwa nafasi mbalimbali kupitia Waziri Mkuu akatuambia asingeweza kulitekeleza jambo lile kwa sababu muda ulikuwa ni mfupi na fedha zilikuwa hakuna. Akatuahidi, analishughulikia. Tunamshukuru sana kwamba ameweza kulishughulikia hili jambo kwa wakati. Tumetoa ahadi majimboni kwamba linashughulikiwa na kwa kweli limeshughulikiwa. Ahsante sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa kuongelea mambo mawili; moja, ni kilimo cha biashara au ushindani ambacho ndiyo dira ambayo ndiyo inaonekana tunakwenda kwenye mazao ya kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema, kilimo cha ushindani au cha kibiashara tunapokiongelea tunaangalia ni namna gani tunafika kwenye soko. Vile vile tunaangalia vitu viwili; tunaangalia ubora na gharama. Ubora huo tunaupata kwa gharama gani? Sasa kuna mambo ambayo tumshukuru sana Mheshimiwa Bashe pamoja na Naibu Waziri na Wizara nzima, kuna mambo ambayo yapo ndani ya uwezo wao wameanza kuyafanya na tumeyashuhudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulizungumzia ubora kwamba lazima uanze kwenye miche, kwenye kitalu. Tulisema sana mwaka 2021 kwenye bajeti iliyopita na kweli wamelitekeleza, tumeona wazi kabisa wameanza mafunzo, wameanza kuwatambua wazalishaji wa miche na wengine wengi wamekuwa hapa kwenye *training* na wengine tumewaona hapa walikuja Bungeni kwa ajili ya kuangalia kinachoendelea hapa. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kutekeleza hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna mambo mengine ambayo nadhani pamoja na kuangalia ubora, bado tulikuwa tunamwomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuona ni kwa namna gani; kwa sababu kwa kweli kwenye mazao ya mbogamboga na parachichi lazima tukubali kwamba ubora ndiyo utakaotutoa. Hizo Shilingi bilioni mbili anazoziongelea Mheshimiwa Waziri au Wizara hatutaweza kuzipata kama hatutakuwa na ubora kwenye soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna mambo ambayo ni ya muhimu sana kuyaangalia kwenye soko ikiwa ni pamoja na kuangalia uthibiti wa ubora. Tulikuwa tumeongea hapa ni vizuri tukawa na *agency* au tukawa na chombo kitakachosaidia kwenye kuthibiti ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua na ninafurahi kwamba hata hilo nalo Mheshimiwa Waziri ametuonesha wazi kwamba lipo katika mchakato. Tunaomba likamilishwe mapema. Hatutaki chombo hiki kiwekwe kwa ajili ya kuingilia biashara, lakini tuna uhakika chombo hiki ni muhimu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba hakutakuwa na mazao ambayo yatakwenda sokoni

bila kuwa na ubora. Tuna uhakika chombo hiki kitapewa *mandate* zaidi ya kuhakikisha kwamba hili zao lenyewe linakuwa *promoted. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema, kuna mambo ambayo Mheshimiwa Bashe na Wizara yake hawana uwezo na ni mambo ya muhimu sana ya kutelepeka kwenye soko. Zao hili la parachichi na mazao ya mbogamboga yanalimwa kwenye mashamba, lakini yanachukuliwa na wachukuzi, yanasafirishwa na wasafarishaji mpaka yanafika kwenye masoko, lakini ni mazao ambayo yapo *sensitive,* yanataka ubora wa hali ya juu, pia ni mazao ambayo yanapoteza ubora kwa haraka sana. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba yapo mambo lazima tuyafanye kwa umakini na kimkakati na hasa yale yanayohusiana na miundombinu kwa ujumla. Wengine wanasema kwa jina rahisi *logistics*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli napenda kusema, tukianza na barabara, tuna vizuizi bado vinasumbua wasafirishaji wa mazao ya mbogamboga na mazao ya parachichi. Ukienda ma-*gate* fulani fulani, na kuna *gate* moja lipo pale Iringa, wana maswali mengi sana ambayo yanaonesha bado hawatambui kwamba maswali hayo hayasaidii sana kwa sababu mchukuaji amechukua *perishable goods* na maswali yanayoulizwa hayapo *relevant.* Kwa hiyo, naomba Wizara zinazohusika ziweze kutusaidia kwenye hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo makubwa sana yapo kwenye maeneo ya Mamlaka zetu za Usafirishaji za Anga na Mamlaka ya Bandari. Kwa kweli kama tupo kwenye ushindani tutambue kwamba tunatakiwa kufanya kazi kubwa sana katika Mamlaka ya Bandari. Nafahamu kuna kazi kubwa inafanyika, lakini bado wana mambo mengi ya kufanya tukilinganisha na wenzetu, bado tupo nyuma sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukiangalia kwenye maeneo yetu ya *Airport* bado *cold rooms facility* hazina uhakika. Ukienda Songwe ambako kuna uzalishaji mkubwa wa parachichi *Southern Highlands* kwa mtu ambaye atataka kusafirisha kwa haraka, atapeleka Songwe *Airport.* Hatuna *cold room facility* pale au kama zipo, bado zinatengenezwa na zinakwenda pole pole sana. Ipo haja ya kuharakisha zoezi hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye Bandari yetu ya Dar es Salaam, hakuna *dedicated berth,* ipo ya *export* kwa ujumla, lakini kwa vitu ambavyo ni *perishable* hakuna *dedicated berth.* Ukienda kwa wenzetu ambao tunashindana nao wana *berth* zaidi ya tatu, nne, mpaka saba ambazo zipo *dedicated* kwa *perishable.* Wafanyakazi kwenye hizo *berth* akili yao yote kila wakati inafikiria ni namna gani wa-*facilitate* mzigo uondoke ili uweze ku-*maintain* ubora wake. Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo Wizara ya Kilimo wanatakiwa wasaidiwe kimkakati kama nchi tuhakikishe kwamba tunafikia hilo lengo linaloongelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiangalie soko la nje tu kwenye mazao ya mbogamboga na parachichi, tuangalie na soko la ndani. Ipo haja ya kuwa na mkakati wa kuhakikisha zao la parachichi hata hapa ndani linapewa elimu ya kutosha, watu wafahamu, siyo kulima na kusafirisha tu, tunaweza tuka-*process* zao la parachichi hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeongolea *gap* la laki nne, mafuta hatuna ya kutosha, tunahitaji mafuta. Parachichi inawezekana. Kuna watu duniani wana *technology* ya kuzalisha parachichi kwa wazalishaji wadogo. Njombe sasa hivi tuna viwanda tisa vya *packing* na *exporting* ya parachichi. Viwanda vyote hivyo vinamilikiwa na watu toka nje, ukiacha kimoja tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Waziri, tuliangalie hili kwa makini sana. Nafahamu nchi ina mkakati wa kuwa na *packing facility* lakini tuelewe kwamba tupo kwenye ushindani. Hawa wenzetu wenye viwanda wakiwa na mazao kule kwao, mazao ya wakulima huku hawatayachukua kwa muda, watayaacha, wata-*process,* wata-*export* mazao yao. Kwa hiyo, ni vizuri tukahakikisha kwamba na sisi tunafanya hiyo shughuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwenye umwagiliaji; parachichi inahitaji maji kama vile chai. Tulipokuwa tunaongea mwaka 2021 hapa, namshukuru Mheshimiwa Waziri na timu yake wameweza kuwa na mkakati mzuri wa kufanya umwagiliaji. Sina uhakika ni kwa kiasi gani mkakati huo wa umwagiliaji unakwenda vile vile kwenye maeneo. Imeongelewa Njombe kwa ujumla, Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha hapa naomba nielewe anaongelea maeneo gani huko Njombe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake kuna maeneo ambayo ni ya *flat,* lakini maeneo mengi ya uzalishaji ya parachichi ni maeneo ya milima ambayo unaweza ukafanya umwagiliaji kwa urahisi sana. Ni kutafuta bonde la asili linazibwa, unapata maji mengi yanatawanywa, yanakwenda mbali, yanakamata wakulima wengi kwa pamoja. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile muda hautoshi, niongelee chai kwa haraka haraka…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanyika muda wako umekwisha.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi naomba ni-*windup.*

**MWENYEKITI:** Sasa naona umegusia chai hapo. Mheshimiwa dakika moja basi, angalau. *(Makofi)*

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye chai tumeona matunda mazuri na tumeona mikakati mizuri, lakini bado napenda kusema, tuna Bodi ya Chai, tuna Wakala wa Chai. Kwa kweli pamoja na kazi wanazozifanya zinaonekana ni nzuri, lakini bado *mandate* zao hawazitumii vizuri. Kwa mfano, wakulima wa chai bado mpaka sasa wananyonywa sana kwa maana ya kwamba hawalipwi kwa wakati na wanadai madeni. Bodi ya Chai tuna uhakika inatakiwa iwasaidie hawa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi ni hawa watu *Tea Agency*. Hawa watu wa *Tea Agency* wanatakiwa waelewe kwamba zao la chai siyo lazima lilimwe na watu wakubwa. Unaweza ukawa na wakulima wadogo ambao wanaweza wakazilisha chai ikapelekwa na maisha yao yakawa mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema, hawa watu wa *Tea Agency* wamepata muda, walikwenda…

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakagenda taarifa. Unataka kumuongezea taarifa kwenye dakika yake moja ya nyongeza siyo! Maana muda wake ulishaisha.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa.

**MWENYEKITI:** Eee!

**T A A R I F A**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa mzungumzaji, anasema Bodi ipo vizuri, wakati huohuo anasema hawafanyi vizuri. Bodi haisimamii chai vizuri, aseme wazi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanyika, unapokea taarifa.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa kwa maana ya kwamba wana kazi nyingi ambazo wamezifanya na ni nzuri, lakini wana maeneo bado wako *very weak* hawa watu wa Bodi, na mojawapo ndilo nililolisema hilo la kwamba hawasimamii wakulima kupata fedha zao wanazozidai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuongelea suala la wakala kidogo tu. Nipende kusema…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanyika nakushukuru sana kwa mchango wako, muda wako umekwisha.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Namwita Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga aweze kuchangia.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi nami niweze kuchangia hotuba ya Bajeti kwa Wizara ya Kilimo ya Kaka yangu Mheshimiwa Hussein Bashe na Mheshimwia Anthony Mavunde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia namfahamu Mheshimiwa Hussein Bashe tangu mwaka 2008 akigombea Uenyekiti wa Umoja wa Vijana na baadaye Umakamu Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana kama Katibu Mkuu wetu Isack alivyosema. Sifa pekee ambayo naweza kuisema ni kwamba ni mtu ambaye ni mgumu kubanduka katika jambo la ukweli analoliamini. Wakulima wa nchi hii wana imani kubwa kwamba kwa sifa hiyo, basi kilimo kimepata tiba ya kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Mwenyezi Mungu aijalie nchi yetu iepukane na majanga na Mheshimiwa Rais akusanye mapato ya kutosha ili bajeti ambayo Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ameiomba aipate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, napenda kushukuru kwamba juzi nilisimama hapa katika Wizara ya Maji kuzungumzia mambo ya wakulima wangu wa Muwa. Napenda kutumia nafasi hii kushukuru Waziri Mheshimiwa Bashe na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, kaka yangu Martine Shigela kwa kutatua changamoto ile. Sasa hivi wananchi wangu wa Kata ya Sanje huko ni shamrashamra kwamba jambo lao limesikika na utatuzi umepatikana, wanaendelea na uvunaji wa miwa na tarehe 19 wanaanza kuingiza miwa katika kiwanda cha Ilovo kwa ajili ya uzalishaji wa sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitagusia kama mambo manne ama matatu kutokana na muda. Mkoa wetu wa Morogoro ni ghala la Taifa. Kwa hiyo, tunamwomba Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe atusaidie sana tafsiri ya ghala la Taifa, kwa kuwa Mkoa wa Morogoro ni Mkoa mzuri sana una ardhi nzuri sana inayofaa kwa kilimo cha kawaida na inafaa kwa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa yetu ya mkoa, juzi tuliambiwa tuna hekta karibu laki 300 zinazofaa kwa umwagiliaji, lakini nasikitika kidogo kuna miradi imeanzishwa na Serikali na inakwama Morogoro haiendelei, hasa ya umwagiliaji. Nitakutajia baadhi hapa ili Mheshimiwa Waziri unisaidie kuinukuu na wale wanaopulizapuliza usije Kilombero, washindwe, walegee,

uje uione hii miradi na uone jinsi fedha za Serikali zimewekwa na miradi haijakamilishwa, wananchi wanapata adha kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Skimu ya *Mang'ula Youth,* fedha za Serikali zimeenda pale, mradi haujakamilika. Tuna *Mark* Magombela, tuna mradi wa Kisawasawa, Serikali ilipeleka fedha lakini haijapeleka fedha za kumalizia. Wakulima hawana pa kuhifadhi mazao yao kama Msalise na Mkula. Maeneo mengine wameomba Shilingi milioni 280 kumalizia na maeneo mengine wameomba Shilingi milioni 150 kumalizia, lakini fedha hazijaenda. Kwa mfano, Mkula wawekezaji wamejenga maghala makubwa kabisa, na mwekezaji kafunga hajamaliziwa fedha yake na wakulima wanashindwa kuhifadhi mpunga wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama tunasema Mkoa wa Morogoro ni ghala la Taifa na tunaweza kuzalisha; unajua karibu 50% ya hitaji la mchele tu la ndani ya nchi yetu, Mkoa wa Morogoro peke yake unaweza. Sasa kama miradi hii haitafanyiwa kazi, kwa vyovyote vile ni wazi kwamba hatutaweza kuwa ghala la Taifa kikwelikweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Kibaoni pale karibu na Ifakara Mjini kuna hekta karibu 10,000 Lungongole ambazo zinafaa kwa kilimo, lakini bado upembuzi yakinifu unasuasua kutokana na ufinyu wa fedha. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri utusaidie ili tuweze kutafsirika kama Mkoa wa Morogoro ni ghala la Taifa. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Mheshimiwa Waziri pamoja na sifa tunazosema kwako na msimamo wako, katika muda atakaokujalia Mwenyezi Mungu kuongoza Wizara ya Kilimo, itakuwa ni aibu kubwa sana ukiacha nchi hii inaagiza sukari kutoka nje. Itakuwa aibu kubwa kweli kweli! Sisi Morogoro hasa Kilombero kama wakulima wa muwa, nami nimekuwa nikipiga kelele kila siku kuhusu wakulima wa muwa na mambo ya ushirika; nitasema baadaye kuhusu ushirika. Sukari, sukari, sukari, ni aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kuzungumza habari ya *importation of sugar,* najua ni vita kubwa hii ya uingizaji wa sukari. Kwa msimamo wako tunajua uta-*control,* isiue kilimo chetu cha ndani cha miwa. Maana yake sisi tulienda Kilombero na Waziri aliyepita akaona miwa karibu 200,000 inabaki. Yaani nchi hii tunaingiza sukari na juzi nimemwona Rais Museven anazindua Kiwanda cha Sukari kitakachozalisha tani 5,000 kwa siku, yaani cha kawaida tu. Sisi tuna-*import sugar* wakati tuna ardhi ya kutosha, tuna kila kitu cha kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, achana na ardhi, miwa imeshalimwa tani 200,000 kiwanda hakina uwezo. Waziri akaenda akatoa *statement* pale wawekezaji wa Ilovo wakakubali kufanya *expansion* ya kiwanda. Mpaka sasa hivi imeishia kwenye ku-*clean layer* tu, wanasema tunaogopa.

*Importation of sugar;* kwamba kuna mashaka kwamba sukari itaingizwa bila utaratibu. Tutawekezaje hapo *500 billion?* Mheshimiwa Waziri tuatilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda kile na upanuzi huo usipofanyika, na hata nimemwona Balozi Mpungu amezungumza kwenye vyombo vya habari akielezea mashaka yake katika uwekezaji ule. Miwa tani 200,000 itaendelea kubaki; na mpaka Magereza walikuwa wanaendelea kulima miwa, na matokeo yake ni kwamba wananchi malalamiko yao yataendelea, na nchi yetu itazidi kuingiza sukari kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua uingizaji wa sukari na vibali hivi vina faida yake, lakini ni wazi kwamba nchi hii hatutakiwi kuingiza sukari kutoka nje. Sisi tunatakiwa kuzalisha sukari kuuza nje. Nimeona hata wawekezaji wa Kagera wale, wakina Nasoro wa Kagera wanahangaika na maeneo tu, wapewe maeneo waweze kulima miwa wazalishe sukari. Wapeni maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wilaya ya Kilombero upande wa Mlimba kule Mofu kuna hekta 10,000 za Bodi ya Sukari zinamilikiwa. Unatafuta mwekezaji mdogo azalishe sukari. Kwa hiyo, katika uongozi wako *legacy* mojawapo ni kuhakikisha utamu wa nchi hii kwa wananchi katika chai unazalishwa na unatosheleza wenyewe humu humu ndani na unakuwa wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu; ukiwa Naibu Waziri wakulima wangu wameshasafiri na mabasi hapa mara tatu au mara nne ukawapokea wakilalamikia makato ya kodi ya 2% na ulitoa *statement* kwamba hela yenu mtarudishiwa. Mpaka sasa hivi hawajarudishiwa. Wakulima wa Kilombero wanauza sukari, hawauzi miwa. Ndiyo mkataba wa kiwanda na wakulima. Wakulima, unalima muwa wako, kiwanda kinavuna, kinaenda kinachakata, kinauza, kikishauza, kikishatoa gharama zote, ndiyo mkulima analipwa na kodi imekatwa. Mkaja kuanzisha 2% ya kwenye mazao, wamekatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alitoa *statement* kwamba ile pesa itarudishwa, haijarudishwa. Sasa huko mbele tukiwa na nia ya kushika Shilingi tutakuwa tunakukosea adabu, lakini ukweli ni kwamba unajua mwenyewe wanakaa mwezi, wanapanda basi, wanakuja kufuatilia *two percent* yao. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa ahadi zenu hizo mhakikishe kwamba fedha zao mnazirudisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema *Doctor* hapa mtaalamu wa ushirika, fanya mabadiliko katika ushirika; na hii hafumbifumbi macho, mimi mwaka 2021 nimefuatilia matatizo ya ushirika. Nimeenda pale kusaini kitabu kwa Mrajisi Taifa hapa mara 11, watu wanaingilia hapa wanatokea hapa. Fanya mabadiliko katika ushirika, lete *modal.* Yupo Mheshimiwa Dkt. Cherehani hapa, ukikaa naye, unajua ana utalaamu wa ushirika, anaweza

kukusaidia mawazo. Watu wanalalamika sana kwenye ushirika, na taarifa ya Waziri Mkuu hapa Bungeni inatosha kukupa picha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu anasema vyama 6,013 vilivyokaguliwa, vyama 357 pekee ndiyo hati zake zinaridhisha. Kuna watu wa Ushirika tuna Mrajisi tuna nani, na Morogoro wana matatizo makubwa, mimi siumi maneno na mwaka jana iliundwa tume mpaka leo taarifa inafichwafichwa, siumi maneno kama Mkoa wa Morogoro Ghala la Taifa Ushirika hawajatimiza wajibu wao na vyama hivyo katika vyama 6,013 na sisi tumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawahami, watu hawarekebishwi, watu hawabadilishwi kama mikoa mingine tunavyoona. Ukisema wanasema Mbunge una ajenda binafsi, haiwezekani Waziri ukaja hapa ukatuambia Waziri Mkuu katoa taarifa kasema vyama 6,013 Waziri Mkuu wa nchi hii, vyama 357 pekee ndiyo vina hati ya kurizisha, Waziri ukileta *statement* yako hapa lazima utujibu taarifa hiyo wa Waziri Mkuu wewe unaishughulikia kwa namna gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kengele imepigwa, nakushukuru naomba kusisitiza kuunga mkono bajeti lakini kusisitiza kwenye ruzuku ya mbolea, chonde chonde wakulima wangu wa mpunga, wakulima wangu wa miwa wanataka ruzuku katika mbolea. Mwaka huu jasho limewatoka kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga kwa mchango wako. Mchangiaji wetu wa mwisho Mheshimiwa Ighondo Ramadhani Abeid namuita aweze kuchangia.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia na mimi fursa angalau nitoe na mimi mchango wangu katika hii sekta muhimu ya kilimo na pia niwasemee wananchi wenzangu wa Jimbo la Singida Kaskazini ambao kwa asilimia kubwa wanategemea kilimo katika maisha yao ya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kutoa pongezi na shukrani nyingi sana kwa Waziri wa Kilimo pamoja na Mheshimiwa Rais kwa kutoa angalau bajeti ya shilingi bilioni 751 kwa ajili ya kilimo. Hii ni hatua kubwa lakini hatua ya pili ni utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pia shukrani na pongezi kwa Mheshimiwa Waziri kwa hatua yake ya kufika Jimboni kwangu Singida Kaskazini. Mheshimiwa Waziri alifika katika bonde kubwa na zuri sana la umwagiliaji pale Msange, akaenda Mughamu na akatuahidi kwamba sasa

tutakwenda kupona kwa kutuletea mradi mkubwa wa umwagiliaji katika maeneo yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *project* ile tayari imeshafika hatua kubwa ya *feasibility study survey* na bwawa pamoja na eneo lenyewe la mradi liko tayari kwa maana ya mashamba, kikubwa sasa tunachosubiri ni fedha kwa ajili ya kuweka miundombinu ile kazi iweze kuanza. Ninamuomba sana Mheshimiwa Waziri aendelee kulimulikia macho kwa karibu sana eneo lile ili kuwakomboa ndugu zako wale wa Singida Kaskazini ambao walifurahi sana siku ile ulipokuja wakaona kabisa kwamba upele sasa umepata mkunaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo na pamoja na ujio wa Mheshimiwa Waziri aliienda kwenye maeneo machache sana mawili tu ya umwagiliaji katika Jimbo la Singida Kaskazini, lakini yako maeneo mengine ambayo tungependa sana afike ili aje aone na kutupa moyo aweze kuwahamasisha Wanasingida Kaskazini kwa kilimo cha umwagiliaji. Kuna maeneo kama vile Mtambuko mabwawa makubwa yana maji muda wote wa mwaka, lakini hayatumiki ipasavyo kwa ajili ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Bwawa la Masoweda, Kisisi kuna Mikuyu na Endeshi, maeneo haya ninaomba sana nimuombe Waziri pamoja na Wizara kwa ujumla wayamulike eneo la Mkoa wa Singida kwa kiwango kikubwa ni kame, lakini tumepata baraka hii ya *water bodies* ambazo yapo muda wote. Niombe sana maeneo haya yatazamwe ili yaweze kuwasaidia na kuwakomboa wananchi wetu ambao kwa kiwango kikubwa wanategemea kilimo, lakini kilimo chenyewe siyo cha uhakika kwa sababu wanategemea mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo niipongeze tena Wizara na hasa Mheshimiwa Waziri kwa kutuletea mbegu hizi za kisasa za alizeti. Tunaipongeza sana Serikali na ni hatua nzuri lakini kwa upande wa Mkoa wa Singida mbegu hizi hazijafanya vizuri sana kwa sababu ya mvua. Mbegu zimekuwa za bei nzuri lakini sasa mvua imetuangusha ndiyo maana nasisitiza kwenye eneo la umwagiliaji ili hizi mbegu ambazo tumepewa kutoka shilingi 35,000 kwa kilo sasa hivi ni shilingi 3,500 lakini hazijaweza kutusaidia sana kwa sababu ya kukosekana mvua ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nisisitize kwenye hizi mbegu ufanyike utafiti sasa tupate mbegu zinazohimili ukame, zinazochukua muda mfupi na zinazotoa mazao mengi ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia pembejeo zingine, tumepata mbegu nashukuru na naendelea kuomba huu mpango uendelee na uboreshwe. Lakini kwenye eneo la pembejeo ninaomba sasa tujielekeze kwenye mbolea. Mbolea hivi sasa mathalani *Urea* mfuko mmoja ambao ulikuwa unauzwa shilingi 60,000 leo unauzwa shilingi 110,000; *DAP* ambayo

ilikuwa inauzwa shilingi 75,000 leo inauzwa shilingi 110,000 ni gharama kubwa sana kwa mkulima hii. Haiwezi kumsaidia na hatuwezi kuwakomboa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Serikali iweke ruzuku kwenye mbolea na pembejeo zingine za kilimo, madawa mengine, viuatilifu lakini pia hata matrekta leo tumeona jeshi la kilimo hapa Bungeni wamepewa pikipiki, wamepewa mpaka vishikwambi, lakini mkulima anatumia jembe la mkono. Haiendani, tunataka hivi vitu viende sambamba tumboreshee mazingira mtendaji kwa maana ya mtumishi, msimamizi lakini hata mkulima naye pia tumtazame, tumboreshee mazingira yake ya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, sana, sana tuhakikishe tunaondoka kwenye jembe la mkono, jembe la asili ambalo halijatupa tija tangu tumepata Uhuru tunalima na jembe la mkono mpaka leo tunalalamika njaa, tunalalamika hatutoshelezi kwenye uzalishaji ni kwa sababu hatujawekeza ipasavyo kwa mkulima. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekuacha, lakini malizia.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, niombe sana kwenye eneo la upungufu wa watumishi hasa Maafisa Kilimo katika Jimbo langu la Singida Kaskazini tunavyo vijiji 84, kata 21 lakini tuna Maafisa Ugani na Kilimo ni 13 tu. Kwa hiyo, niombe sana vijiji vingi havina Watendaji, havina Maafisa Ugani hawa, wataalam kwa hiyo, wakulima wanajilimia hawana mwongozo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, baada ya kusema hayo, ninayo mengi na nitayawasilisha mengine kwa maandishi. Niombe sana Wizara hii *next time* iongezewe muda. Muda wa dakika tano hizi hatuwezi kuishauri Serikari ipasavyo, tutaishia kupitiapitia tu juu juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninashukuru sana na ninaunga mkono na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa mijadala yetu kwa siku ya leo na hapa kuna wageni naomba niwatambulishe.

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Hussein Bashe ambaye ni Waziri wa Kilimo ambao ni Viongozi wa Dini ya Kiislam kutoka Mkoa wa Mwanza wakiongozwa na Sheikh Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Sheikh Hassan Kabeki, karibuni sana viongozi wa dini kutoka Mwanza kwa kuja kushiriki katika Bajeti hii ya Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Pia tunao wageni watano wa Mheshimiwa Neema Mwandabila, Mbunge ambao ni Viongozi wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) kutoka

Mkoa wa Songwe wakiongozwa na Mweka Hazina wa Mkoa, Mwalimu Salim Simba, karibuni sana Viongozi wa Chama cha Walimu. *(Makofi)*

Aidha, kuna tangazo hapa kutoka kwa Katibu wa Bunge ambaye anawajulisha Waheshimiwa Wabunge kuwa kesho Jumatano tarehe 18 Mei, 2022 kutakuwa na semina kwa Wabunge wote kuhusu masuala ya bima inayotolewa na Shirika la Bima la Taifa na masuala ya Diplomasia na Itifaki itakayotolewa na Chuo cha Diplomasia. Semina hii itaanza saa 7.30 mchana katika Ukumbi wa Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge wote mnasisitizwa kuhudhuria semina hiyo ni muhimu sana kufika kwa sababu mambo ya Itifaki, *does and don't* inapatikana hapo pia. Saa 7.30 mchana kesho ili kujua Itifaki, Itifaki mbalimbali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa *session* ya jioni, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho asubuhi saa tatu kamili.

*(Saa 1.45 usiku Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatano, Tarehe 18 Mei, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*